

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 17 Februari, 2022

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Mapendelekezo ya Nyongeza ya Bajeti ya Mwaka 2021/2022.

MHE. JAPHET N. HASUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kazi nzuri, Wenyeviti wanafanya kazi nzuri ya kugawana majukumu.

Katibu!

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Maswali; Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 149

**Ongezeko la Kiwango cha Mkopo kwa Vijana,
Wazee na Wanawake**

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kiwango cha mkopo wa 10% kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa mikopo inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kusaidia makundi haya kuendasha shughuli zao za ujasiriamali na kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haijaweka mpango wa kuongeza asilimia ya mikopo hiyo. Aidha, tathmini ya kina inafanyika ili kubaini mafanikio na changamoto zilizopo ili hatua stahiki zichukuliwe katika kuboresha mikopo hiyo.

SPIKA: Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakangata, swal la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Spika, ahsante, ninashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swal langu la kwanza ni, kwa sababu wanawake au makundi haya kwa sasa hivi yanapata mkopo kwa kiwango kidogo sana kiasi kwamba mkopo huo hauwasaidii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kiwango hicho kutoka milioni mbili na laki tano kwa kila kundi mpaka milioni kumi ili waweze kufanya vizuri kwenye biashara zao?

Mheshimiwa Spika, swal la pili; Serikali sasa ina mpango gani wa kuwajengea mafunzo na uwezo kabla makundi haya hayajapewa mkopo?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, makundi haya ambayo ni ya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu yanakopesha asilimia 10, kwa maana ya 4:4:2, lakini kiwango cha ukopeshaji hakijaainishwa, inategemea aina ya shughuli ya ujasiriamali, si kila kikundi kinakopesha milioni mbili na laki tano. Kila kikundi kinakopesha kuliangana na uhitaji wa biashara yao, lakini pia uwezo wa kurejesha fedha zile baada ya kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, na Serikali imetoa tamko kwamba tunahitaji kuona vikundi nya wajasiriamali wanakopeshwa fedha zenye kiwango ambacho kinaleta tija ya kuwawezesha kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine badala ya kutoa fedha kidogokidogo ambazo kwanza haziwawezeshi kiuchumi, lakini pili inakuwa ni changamoto kuzirejeshwa. Kwa hiyo, maelekezo haya yametolewa, na Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ameelekeza na sisi Ofisi ya Rais TAMISEMI tunalitekeleza.

Mheshimiwa Spika, na nichukue nafasi hii kutoa maelekezo kwa halmashauri zote kuhakikisha kwamba wanatoa fedha yenye tija badala ya kutoa fedha kidogo kidogo kwa vikundi nya wajasirimali.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mafunzo umewekwa vizuri. Maafisa Maendeleo ya Jamii katika hamashauri zetu wanawajibika kwanza kuwajengea uwezo kwa maana ya mafunzo pamoja na kuwatemeblea na kuhakikisha kwamba wanafanya biashara zao, na zoezi hili ni endelevu. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Waliokuwa Bungeni kabla yetu waliona busara kwamba asilimia 10 iende kwa wanawake, na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

baadae sasa makundi yale yalivyobainika ikaonekana ile ile asilimia 10 igawanywe kwa walemavu na vijana.

Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wanawake wakabaki na ile asilimia 10 na yale makundi mengine yakapatiwa asilimia yao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, suala la kisheria hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mikopo ya Ujasiriamali iliyopitishwa na Bunge hili mwaka 2019 inaelekeza asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Ni kweli kwamba tulianza na asilimia 10 kwa wanawake, lakini baada ya tathimini ya makundi yenye uhitaji wa kujengewa uwezo wa ujasiriamali yaliongezeka makundi ya vijana pamoja na makundi ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, makundi haya yote ni muhimu kujengewa uwezo katika jamii yetu. Hata hivyo tunachukua wazo lake kuendelea kufanya tathmini. Lakini kabla hatujafikia hatua hiyo tunafanya tathmini ya ufanisi, changamoto na mafanikio ya hii asilimia 10, kwa maana ya 4:4:2, na baada ya hapo tutaona maeneo gani tuboreshe ili tuweze ku-*accommodate* mawazo ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Wambura, swalii la nyongeza.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kuna zile fedha za marejesho za miaka iliyopita ambazo huwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zinajeshwa ambazo inaonekana kwamba kila halmashauri inakuwa na utaratibu wake.

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali kuhusiana na hizi fedha zinazorejeshwa ambazo zingeweza kuongeza kiasi cha wanaokopa wakapata fedha nydingi zaidi? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swalii la Mheshimia Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya fedha za marejesho ya asilimia 10 zimefunguliwa akaunti zake mahsusii, kwa hiyo wajasiriamali wanaporejesha fedha zile zinatakiwa kuingizwa kwenye akaunti mahsusii ya marejesho ya mikopo ya asilimia 10. Akaunti ile ni *revolving fund*, maana yake baada ya kurejeshwa zinatakiwa kuendelea kuwakopesha vikundi vyaa wajasiriamali. Kwa hiyo, matarajio ya Serikali ni kwamba akaunti zile kila baada ya mwaka wa fedha zitakuwa zinaendelea kuongezeka na kutakuwa na fedha za kutosha zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilitoa maelekezo, na hakuna halmashauri inayotakiwa kwenda kinyume na maelekezo haya. Nitoe wito kwamba halmashauri zote ni lazima zihakikishe kwamba akaunti za marejesho zinafanya kazi, na fedha zile zikirejeshwa ziendelee kukopesha wajasiriamali wengine.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, sasa aulize swalii lake.

Na. 150

**Hitaji la Vituo vya Afya Eneo la Nsemulwa na
Mwamkulu – Mpanda**

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Vituo vya Afya eneo la Nsemulwa na Mwamkulu katika Manispaa ya Mpanda?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Nsemulwa ambapo hadi kufikia Februari, 2022 shilingi milioni 250 zimeshatolewa. Ujenzi wa majengo matatu ya wagonjwa wa nje, maabara na wodi ya wazazi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepeleka fedha shilingi milioni 250 katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mwamkulu ambapo ujenzi wa jengo la *OPD* umefikia hatua ya lenta na maabara umefikia hatua ya umaliziaji.

SPIKA: Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, swali la nyongeza.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa muda huu wa maswali madogo mawili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya nyongeza. Ninaishukuru sana Serikali kwa fedha hizo zilizotolewa, na hivi karibuni tulipata milioni 300, nasema ahsante kwa Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya Mwamkulu fedha zilizotolewa zina uwezo wa kujenga *OPD*. Ni lini Serikali itatuongeza fedha ili tuweze kumalizia majengo mengine?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Kituo cha Afya cha Illembu kilibahatika kupata fedha shilingi milioni 400, lakini fedha zile hazikulenga vifaa tiba. Ni lini Serikali itatusaidia fedha ili tuweze kununua vifaa tiba?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee shukrani nyingi za Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wa Manispaa ya Mpanda ambazo amezielekeza kwa Serikali yetu inayochapa kazi, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan. Na ni kweli, hakuna jimbo ambalo halijapata vituo vya afya na zahanati. Kazi inaendelea na tunaona wananchi wetu wananaufaika na miradi hii ya afya.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki cha Afya cha Mwamkulu kimepewa milioni 250, na maelekezo ni kujenga majengo matatu. Jengo la *OPD*, maabara pamoja na kichomea taka. Kwa hiyo milioni 250 si ya kujenga *OPD* peke yake, na hiyo ni *standard* kwa milioni 250 zilizotolewa nchini kote. Awamu ya pili tutapeleka fedha tena kwa ajili ya kikamilisha majengo yaliyobaki yakiwemo wodi, majengo ya upasuaji na majengo mengine muhimu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la vifaa, Serikali imeweka utarartibu, kuanza baada ya kukamilisha miundombinu hiyo, kwa awamu tutapeleka fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba ili kuwezesha vituo vyetu kufanya kazi vizuri zaidi. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mwaka 2017/2018 Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa anazindua Siku ya Ushiriki wa Afya Duniani katika Jimbo la Ushetu katika Halmashauri ya Ushetu, Kata ya Ulowa, aliwaaahidi wananchi kuwajengea kituo cha afya, lakini hadi leo ni miaka mitano kituo hicho hakijaanza kujengwa.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga Kituo Cha Afya kwa wananchi wa Ulowa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ahadi zote za viongozi wetu wa Kitaifa ni kipaumbele katika utekelezaji, kikiwepo Kituo cha Afya katika Kata ya Ulowa. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie kwamba Serikali imechukua mahitaji na ahadi hii, na tunatafuta fedha, wakati wowote kupitia fedha za tozo tutaleta pale milioni 250 ili Kituo cha Afya cha Ulowa kianze kujengwa. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

MHE. PRISCUS J. TARIMO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ninaomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya pale Moshi Mjini, kwa sababu ilishapitishwa kwenye bajeti na wengine wameshapata?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Priscus Tarimo Mbunge, wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha Serikali imetenga shilingi bilioni 14 kwa ajili ya hospitali za halmashauri 28 katika hamashauri ambazo hazina kabisa hospitali za halmashauri Ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Moshi. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha lengo la Serikali ni kuleta fedha hiyo, milioni 500, ili kazi ya ujenzi iweze kuanza. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Kunambi, swali la nyongeza.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba imeanza ujenzi wa Kituo cha Afya kwa mapato ya ndani, na jengo la wagonjwa wa nje (*OPD*) limekamilika. Sasa ni nini mpango wa Serikali kuisaidia halmashauri hiyo kukamilisha majengo yaliyobaki? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge, kama ifuatavyo: -

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa ujenzi wa vituo vyatya unahusisha nguvu za wananchi katika michango yao na kujenga vituo hivyo. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwanza kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo hili la Mlimba, ambako Mheshimiwa Kunambi ndiye Mbunge, kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wameifanya ya kujenga kituo cha afya. Nimhakikishie, kwa awamu tutatafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunakamilisha miundombinu ambayo inabaki.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijijini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu.

Na. 151

Uchakavu Mkubwa wa Miundombinu ya Shule Kongwe za Msingi

MHE. YAHYA A. MHATA K.n.y. MHE. MAIMUNA S. MTANDA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ukarabati wa shule za msingi kongwe ambazo zimechakaa na majengo yake ni mafupi ulikinganisha na yanayojengwa kwa sasa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa shule kongwe za msingi zilizo katika hali ya uchakavu. Kazi ya

kuzikarabati shule hizi ilishaanza kupitia miradi mbalimbali ya elimu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali ya shule za msingi nchini. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali kupitia Programu ya *EP4R* (Lipa Kulingana na Matokeo) imeendelea na ujenzi wa vyumba vyaa madarasa ya shule za msingi 1,970, matundu ya vyoo 5,303, nyumba za walimu wa msingi 17. Ujenzi huu ni kwa ajili ya kuboresha mazingira ya miundombinu ya shule za msingi zikiwemo shule kongwe ambazo zina miundombinu chakavu. Vilevile kupitia Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 (*TCRP*), Serikali imejenga vyumba 3,000 vyaa madarasa katika vituo shikizi 970.

Mheshimiwa Spika Serikali kupitia Mradi wa *BOOST* utakaotekelwa katika shule za msingi inatarajiwa kujenga madarasa 12,000 katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 na itaendelea kutumia fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri kujenga na kukarabati shule za msingi kongwe nchini.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Mhata, swalii la nyongeza.

MHE. YAHYA A. MHATA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Wilaya hii ya Newala ni kati ya wilaya kongwe hapa nchini na shule zake mfano Shule ya Makukwe II, Nakaako na Babati ni shule ambazo zina hali mbaya na mapaa yake yake yanavuja hivi sasa. Kipindi hiki cha masika, vijana wetu wanatosoma katika mazingira magumu sana. Swalii la kwanza, Serikali itakuwa tayari kuzifikiria shule hizi katika mwaka ujao wa fedha kuipangia bajeti ya kutosha ili kufanya ukarabati?

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili; linakwenda ndani ya jimbo langu. Katika Kata ya Mikangaula, Wilaya ya Nanyumbu kuna shule ya Mikangaula ambayo ina wanafunzi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

1,500 na kuna darasa lina wanafunzi 300. Kwa kutambua adha hii wananchi wa Kata hii wameamua kutumia nguvu zao ili kujenga madarasa katika vijiji vingine. Je, Serikali ipo tayari kushirkiana na wananchi wa Kata hii kuipatia fedha ili vijiji hivi ambavyo vimetoa nguvu zao waweze kupata fedha na kuwanusuru wananchi wao? (*Makofii*) Je, ni lini Serikali itakabidhi majengo yaliyokuwa ya Hospitali ya Muhimbili kwa Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo ili kupunguza uhaba wa majengo katika Hospitali hiyo.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimweleze tu kwamba Serikali ipo tayari kuingiza katika mpango Halmashauri ya Newala na kuhakikisha hizo shule kongwe zote zinafanyiwa ukarabati. Hapa nimweleze tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpaka sasa hivi tathmini ya awali tumeshapata tathmini ya Shule 750 za Msingi Kongwe ambazo zimejengwa kabla ya mwaka 1950, yaani kabla ya uhuru wa nchi yetu ambazo tunatakiwa kuzifanya tathmini.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wetu ni ndani ya miaka mitano shule zote kongwe nchini tutazikarabati kwa kujenga madarasa mapya, ndio maana katika mwaka wa fedha 2022/2023 tuna ujenzi wa madarasa kwenye Shule za Msingi 12,000 nchi nzima kwa ajili ya kwenda kufanya hayo maboresho. Kwa hiyo, tuko tayari kwa hilo ikiwemo na katika eneo la jimbo la Mheshimiwa katika Kata ya Mikangaula ambayo umeianisha kwamba tutaingiza katika mpango na tutawapatia fedha ili kumalizia hayo majengo. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat Hanje, swalil la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa lengo ni kuboresha elimu yetu nchini. Ni kwa nini sasa Serikali isipandishe hadhi Shule ya Sekondari Sepuka ambayo ipo Jimbo la Singida Magharibi ambayo kwa sasa ndiyo shule kongwe kuliko shule zote katika Tarafa ya Sepuka ambayo imebeba nusu ya Kata za Jimbo la Singida Magharibi? Ahsnate.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba ombi la Mheshimiwa Mbunge ni Shule ya Sepuka sijajua ni sekondari ama msingi, lakini naamini ni Sekondari kwenda Kidato cha Tano na cha Sita ambao wanataka tupandishe hadhi na kuwa kidato cha tano na cha sita kwa sababu inapokea wanafunzi kutoka maeneo mbalimbali. Moja ya mpango wa Serikali ni kufanya upanuzi wa shule za sekondari za Kata 100 katika mwaka 2022 ili tuongeze wigo wa kuongeza wanafunzi wa kwenda kuijunga na kidato cha tano na cha sita.

Mheshimiwa Spika, naamini kama lipo katika mpango, basi maana yake tutalifanya kazi katika mwaka huu fedha 2022/2023, lakini kama halipo maana yake tutalifanya kazi katika mwaka wa fedha unaokuja 2023/2024. Kwa hiyo, nitayapitia ili niweze kujiridhisha nione kama halipo katika mwaka huu, kama litakuwepo mwakani maana yake tutaliingiza, kwa hiyo ni hilo tu. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

MHE. MICHAEL C. MWAKAMO: Mheshimiwa Spika, hali ilivyo kwenye Wilaya ya Newala ni sawasawa na Kibaha Vijijini

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwenye shule za Dutumi, Madege na Magindu. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati sahihi na kule kulifanyia ukarabati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumjibu Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba mwakani tuna madarasa zaidi 12,000 kwa ajili ya ukarabati wa shule za msingi nchini. Kwa hiyo, naamini kwa sababu moja ya utaratibu wetu ni kuhakikisha kwamba tunayafikia majimbo nchini, llikwemo Jimbo la Kibaha Vijijini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aondoe wasiwasi kwa sababu tutaweka katika mpango na wananchi wake watapata hiyo faida ya yeye kuwepo ndani Bunge. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kasalali Mageni, swali la nyongeza.

MHE. KASALALI E. MAGENI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa shule ya Sekondari ya Sumve ni moja ya shule kongwe ambayo ina historia kubwa sana kwenye nchi yetu ambapo mama Maria Nyerere alipata elimu yake pale na ni shule ambayo imechakaa sana. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuipa kipaumbele shule hii ya Sumve Sekondari katika kuanza ukarabati wa shule kongwe katika bajeti inayokuja?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumjibu kwa kifupi sana Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kasalali kwa swali lake; ni kwamba shule alioitaja Sumve ambayo ina historia kubwa amesema tuipe kipaumbele basi na mimi nilipokee ombi lake tutazingatia, tutampa kipaumbele na kama tutakavyowapa Wabunge wote katika Bunge hili. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya Mheshimiwa Muharami Shaabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo sasa aulize swali lake.

Na. 152

Kukabidhi Majengo Yaliyokuwa Hospitali ya Muhimbili kwa Hospitali ya Wilaya Bagamoyo

MHE. MUHARAMI S. MKENGE aliuliza:-

Je ni lini Serikali itakabidhi majengo yaliyokuwa ya Hospitali ya Muhimbili kwa Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo ili kupunguza uhaba wa majengo katika Hospitali hiyo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt Godwin Mollel, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shaban Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba majengo hayo yanayomilikiwa na Chuo Kikuu cha Afya Kishiriki cha Muhimbili (*MUHAS*) na chuo kimekuwa kikiyatumia majengo hayo kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Chuo kikuu *MUHAS* bado kina mipango ya uendelezaji na upanuzi wa eneo hilo ili kutimiza majukumu yake, katika kuzalisha wataalam wa afya nchini.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika: Serikali tayari imepeleka fedha shilingi milioni 300 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la huduma za dharura kwenye Hospitali ya Bagamoyo na hivyo naomba majengo ya Chuo Kikuu MUHAS yaendelee kutumika kwa shughuli za ufundishaji na utafiti kwa wanafunzi wa Chuo cha MUHAS. Hata hivyo uwepo wa Chuo cha MUHAS ni fursa kwa ukuaji wa Hospitali ya Bagamoyo na ni fursa kwa watu wa bagamoyo kitiba na kiuchumi. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Muharami Mkenge, swalii la nyongeza.

MHE. MUHARAMI S. MKENGE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini majengo yale ni zaidi ya miaka 10 sasa yamekaa hayana matumizi yo yote. Swalii la kwanza; je, MUHAS lini wanaanza huo upanuzi wao wa hayo maeneo?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa nini wasiwaazime Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo yale majengo yakatumika kwa Hospitali ya Wilaya ili mradi majengo yale yapate kutumika, yasiendelee kuharibika? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anawakilisha wananchi wa Bagamoyo. Ameuliza swalii ni lini wataanza kufanya upanuzi na kuyatumia, nafikiri yanatumika wakati wote lakini nitakwenda tutembelee mimi na yeye na tuweze kuwasiliana na utawala wa MUHASili tuweke mkakati mzuri wa kuhakikisha wanashirikiana ofisi ya Mbunge na wananchi wa Bagamoyo na Chuo cha MUHAS.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili, ninachowea kumwambia ndugu yangu ni kwamba, kikubwa kwa wananchi wa Bagamoyo, Chuo Kikuu kila Mbunge hapa angetamani Chuo Kikuu kiwepo ndani ya Jimbo lake. Chuo Kikuu kuwepo ndani ya Jimbo lako ni fursa kubwa sana. Kwa hiyo, kikubwa mimi na yeye tutakachokifanya ni kujenga

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uhusiano na Hospitali ya Wilaya na Chuo Kikuu cha MUHASili wawewe kushirikiana na kufanya kazi pamoja na kufufua yale majengo ili hospitali ya Mheshimiwa iweze kupanuka, lakini manufaa ya watumishi yapatikane. Kwa upande wa hospitali ya wilaya lakini manufaa yanayotokana na Chuo Kikuu yapatikane kwa watu wa Bagamoyo. Tutakwenda kusista umuhimu wa mahusiano. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Singida Mjini hatuna Hospitali ya Wilaya na ipo ahadi ya Serikali ya kukabidhi majengo ya Hospitali ya Mkoa wa Singida kwa Hospitali ya Wilaya. Sasa nataka kujuua ni lini ahadi hii itatekelezwa? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge, swali lake, kama lifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza alivyo na taarifa na tulivyotembelea mimi na yeye kwenye hospitali yake ya mkoa juzi, tumeona majengo ambayo yanajengwa hospitali mpya ya Mkoa wa Singida. Siyo muda mrefu mpaka mwezi Julai majengo yale yanakwenda kukamilika na hospitali ya mkoa itaondolewa kwenye eneo iliyokuwepo halafu na kuwaachia wilaya hiyo iendelee kutumia hospitali iliyoko pale. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, swali la nyogezza.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza Chuo cha MUHAS kimedahili wanafunzi wengi sana kiasi kwamba wanafundishwa somo hilo hilo kwa session mbili kwa siku. Je, Serikali inaonaje sasa ikachukua hatua ya haraka sana kuhakikisha kwamba haya majengo ambayo yanamilikiwa na Serikali yakatumika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

haraka ili wanafunzi wakayatumia ili kuweza kupunguza hiyo changamoto?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Nahato, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba ndiyo maana nikamwambia Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swalii la msingi uwepo wa majengo yale kule Bagamoyo ni fursa kwake; na sababu mojawapo ni hilo analolisema Mheshimiwa Mbunge kwamba wanafunzi sasa wamerundikana pale Muhibili na somo lilelile linaingia darasa hilo hilo mara mbili na wanafunzi wa *session* tofauti, lakini darasa lilelile.

Kwa hiyo, kimsingi tutakwenda kufanya haraka na tutakwenda kushauriana kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023, fedha ziweze kuweza kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu ili kuweza kukarabati majengo yaliyopo Bagamoyo na haya Mlonganzila iweze kutumika ili wanafunzi wa MUHAS waweze kufundishwa kwa wakati mmoja.

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 153

Akinamama Kufanya Biashara Zenye Tija

MHE. MWANTUMU DAU HAJI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia akinamama wafanyabiashara ili wafanye biashara zenye tija?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exaud Kigahe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuhamasisha wafanyabiashara wadogo wakiwemo akinamama kufanya shughuli zao katika maeneo rasmi na kuchukua vitambulisho vya wajasiriamali na kurasimisha biashara zao. Mikakati ya Serikali ni kuendelea kuwasaidia akinamama wafanyabiashara kupitia mikopo inayotolewa na Mifuko ya Uwezeshaji ukiwemo Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wananchi (*NEDF*) chini ya Shirika letu la Kuendeleza Viwanda Vidogo (*SIDO*) na Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wajasiriamali (*SME Credit Guarantee Scheme*) unaoratibiwa na pia *SIDO* kwa kushirikiana na Benki ya *CRDB*.

Mheshimiwa Spika, pia tunaendelea kuboresha na kujenga miundombinu ikiwemo majengo ili wapate sehemu tulivu za kukuza biashara zao. Kuanzia Julai, 2015 hadi Machi, 2021, Serikali kupitia Mfuko wa Dhamana ya Mikopo kwa Wajasiriamali pekee imekwishawapatia akinamama wafanyabiashara mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 310. Aidha, Wizara inakamilisha mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003 ili iweze kuendana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi ya sasa. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini napenda kumuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia soko lenye uhakika na tija nchini?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganisha akinamama kwenye mitandao ya wafanyabiashara duniani? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mwantumu kwa vile ambavyo anawasemea sana akinamama ili kuhakikisha nao wanajikomboa katika kufanyabiashara katika mazingira mazuri. Lengo la Serikali, kwanza ni kuhakikisha wafanyabiashara wote wakilwemo akinamama wanazalisha bidhaa zao katika ubora. Kwa hiyo, la kwanza tunalofanya kuhakikisha tunawapa mafunzo ili kuhakikisha wanazalisha bidhaa zenye tija.

Mheshimiwa Spika, pili, kupitia taasisi zetu tunawaunganisha kwenye masoko mbalimbali kupitia maonesho ambayo yanaandaliiwa na *TANTRADE*. Pia kwenye kuhakikisha wanaingia kwenye mtandao wa wafanyabiashara duniani kwa kupitia *chamber* ya wafanyabiashara wanawake *Tanzania Women Chamber of Commerce* tumekuwa tukiandaa kwa kushirikiana na Serikali, ziara kwenye Maonyesho ya Kimataifa ikiwemo ile iliyofanyika mwaka 2018 kule China ili angalau kuwapa uelewa mpana kwa wafanyabiashara wetu akinamama katika masoko ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pia zaidi sasa tumeanzisha biashara mtandao kupitia *TANTRADE* na Posta ili iwasaidie kufanya biashara kwenye mtandao na hivyo kujiongezea kipato. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Robert Maboto, swali la nyongeza.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ROBERT C. MABOTO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali ililipa eneo la Viwanda na Uwekezaji pale Bunda Mjini kwa muda mrefu na wananchi wakahama kwenye eneo lile, lakini leo wameanza kurejea kwenye eneo lile. Ni nini mpango wa Serikali katika kulitumia eneo lile?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Robert Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli eneo lile ambalo lilo pale, lipi chini ya EPZA kwa maana ya maeneo ya uwekezaji huru kwa ajili ya mauzo nje. Serikali tunaendelea kutafuta fedha ili tuweze kuyaendeleza maeneo yote ambayo yapo chini ya EPZA likiwemo eneo hili la Bunda Mjini.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutalitekeleza au tutaanza kulifanyia kazi hivi karibuni katika eneo hilo la Bunda Mjini. Nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Paresso swalii nyongeza.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalii dogo nyongeza. Tuna Mifuko mingi sana ya uwezeshehaji wanawake na vijana kiuchumi na mifuko hiyo imekuwa kwenye Wizara mbalimbali ndani ya Serikali:-

Kwa nini Serikali sasa isifikirie angalau kuwa na mifuko miwili ambayo itatosheleza mahitaji ya walengwa kwa maana ya wanawake na vijana? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Paresso kwa sababu anauliza swali la msingi sana kuona namna ambavyo tunaweza kupunguza wingi wa Mifuko hii ambayo inahudumia wananchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, tunalipokea wazo hili na Serikali ipo kwenye michakato kuona namna gani ya kuunganisha mifuko inayotoa huduma zinazofanana ili kuweza kuifanya iwe na tija kwa ajili ya kuwasaidia wananchi ikiwemo akina mama, vijana na walemaru. Kwa hiyo, tunachukua mawazo yake, nasi tunaendelea kuyafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Bahati Ndingo, swali la nyongeza.

MHE. BAHATI K. NDINGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuiuliza Wizara, kutokana na athari za UVIKO-19 nchi yetu pia imekumbwa na ongezeko la mfumuko wa bei:-

Je, Wizara imefanya tathmini gani kuona athari ambazo wafanyabiashara wamepata; na wana mkakati gani kuhakikisha hali ya mfumuko wa bei nchini unakwenda kurekebishwa? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara majibu.

NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bahati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli sote ni mashahidi kwamba kumekuwa na athari kubwa kutokana na janga hili la ugonjwa wa UVIKO-19, katika bidhaa mbalimbali kwa maana

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya kupanda bei. Serikali inafanya jitihada za makusudi kuona namna gani tunasaidia viwanda na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali ndani ya nchi pamoja na kuweka vivutio na kupunguza gharama za wale ambao wanaingiza bidhaa mbalimbali zinazotumika kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nadhani mtaona kwa makusudi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuangalia hili, aliweza kuangalia pia eneo la mafuta ambayo ni sehemu nyeti sana inayoongeza gharama za bidhaa kwenye usafirishaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na mambo mengine tunaangalia kwa namna gani tutasaidia wazalishaji ili waweze kuzalisha kwa bei nafuu, na pia mnyororo mzima wa usafirishaji wa bidhaa za ndani na zile zinazotoka nje ya nchi. Nakushukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 154

Mkanganyiko wa Fidia Barabara ya Tanga – Pangani

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali kutokana na mkanganyiko uliotokea kuhusu fidia katika barabara ya Tanga – Pangani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tanga – Pangani yenye urefu wa kilomita 50 ni sehemu ya barabara ya Bagamoyo kuanzia Makurunge – Saadani – Pangani hadi Tanga ambayo ina urefu wa kilomita 256. Awali Benki ya Maendeleo ya Afrika ilionesha nia ya kufadhili barabara yote ya Bagamoyo kuanzia Makurunge – Saadani – Pangani hadi Tanga urefu wa kilomita 256.

Mheshimiwa Spika, aidha, mfadhili alitoa sharti la kulipia fidia kwa mali zote zitakazoathiriwa na mradi ndani na nje ya eneo la hifadhi ya barabara. Hivyo, uthamini wa mali zitakazoathiriwa na mradi ulifanyika kwa kuzingatia sharti hilo. Wananchi walifahamishwa kwenye mikutano ya uelimishaji umma na kujulishwa kuwa endapo mfadhili hataendelea na nia hiyo na Serikali ikajenga kwa fedha za ndani, wale wenye mali zilizopo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara hawatalipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hiyo, na kwa kutochelewesha mradi, Serikali ilianza ujenzi kwa sehemu ya Tanga, hadi Pangani urefu wa kilomita 50 kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka, 2017 ujenzi wa aina yoyote hauruhusiwi ndani ya eneo la hifadhi ya barabara. Hivyo, wananchi waliofanya maendelezo ndani ya eneo hilo hawastahili kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuata matakwa ya sheria za nchi wale wote ambao walikuwa ndani ya eneo la hifadhi ya barabara, hawakustahili kulipwa fidia na waliondolewa kwenye orodha ya malipo kabla ya taarifa ya fidia kuwasilishwa kwa Mthamini Mkuu wa Serikali. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, swalii la nyongeza.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi la fidia lilianza mwaka, 2012 mpaka 2013 kama sikosei na *verification* imekuja kufanyika mwaka 2015; na mpaka wananchi kulipwa, wamelipwa mwaka 2021 ambayo ni takribani miaka tisa:-

Je, Serikali haioni haja wale ambao hawakulipwa kwa mujibu wa Sheria yetu ya Barabara ya 2007, ukiwaacha pembeni kulingana na sheria ya awali ya masharti ya *ADB* kufutwa machozi kwa kuzingatia kwamba wamekaa miaka tisa bila kufanya maendeleo yoyote? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii langu la pili; kwa kuwa malalamiko ya kupotezewa muda mwingu wananchi yapo Tanzania nzima kwenye suala zima la kulipwa fidia:-

Je, ni lini Serikali itaileta Sheria ya Barabara ya Mwaka, 2007 *Act (No. 13)* tukirekebishe kifungu Na. 16 ili kuweze kuongeza muda wa kuwalipa fidia wananchi? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge*, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuwapigania haki wananchi wa Mkoa wa Tanga ambao anawatetea.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la kwanza, naomba nimjulisse Mheshimiwa Mbunge kwamba katika fidia za wananchi hawa wapo ambao waliridhika na wamechukua fidia, lakini wale ambao hawakuridhika, suala hili walilifikisha Mahakamani. Kwa hiyo, naomba nisiitolee maelezo zaidi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili kuhusu mMarekebisho ya sheria, naomba niseme tumelichukua na tutakwenda kulifanya kazi. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Sanga, swalii la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa barabara ya kutoka Nyigu kwenda Mgololo ambako ndiko kuna kiwanda kikubwa cha karatasi ambaao ni uwekezaji mkubwa sana; na ni barabara ya uchumi ambayo imekuwa ikiwasaidia sana wananchi wa eneo hilo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Eng. Msongwe* majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hii ni muhimu sana na mbaao nydingi tunazoziona zinapita kwenye hii barabara. Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili amekuja ofisini kama yeye kuliongelea.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizi ni barabara za kimkakati. Kwa hiyo, namwomba yeye pamoja na wananchi wavute subira kwamba, kulingana na umuhimu wake na jinsi inavyoliingizia Taifa fedha nydingi, basi itakuwepo kwenye mpango ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, mlisosimama nawaona lakini niwakumbushe tu swalii la msingi linahusu fidia. Mheshimiwa Anatropia Rwehikila.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ujenzi wa barabara ya Mgakorongo kwenda Murongo tathmini imefanyika na wananchi wamekuwa wakisubiri fidia kwa muda mrefu, kiasi kwamba wanashawishika kufanya maendeleo:-

Je, ni lini fidia zitaanza kutoka ili wananchi waweze kuhamia sehemu nyingine waendelee na maisha yao? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wanaohusika na barabara hii ya kuanzia Omugakarongo, Kigarama hadi Murongo; hii barabara ipo kwenye maandalizi ya kutangazwa zabuni. Barabara hii kabla haijaanzwa tutahakikisha kwamba wananchi hawa kipaumbele ni kuwalipa fidia. Kwa hiyo, kabla hatujaanza kujenga, wananchi kwanza watalipwa fidia na ujenzi wa hiyo barabara utaanza. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda swali la nyongeza.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, limeshajibiwa.

SPIKA: Aah, lilishajibiwa la kwako! Sawa, ahsante sana. Mheshimiwa Eric Shigongo swali la nyongeza.

MHE. ERIC J. SHIGONGO: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa changamoto wanayoipata wananchi wa maeneo ya Tanga na Pangani ni sawa sawa na matatizo walijonayo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wananchi wa Buchosa ambao ahadi ya Serikali ilikuwa ni kujenga barabara kutoka Sengerema, Nyehunge mpaka Kahunda, lakini wananchi wale wamesimamisha shughuli zao wakisubiri fidia na ujenzi uanz:-

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuwaambia wananchi wa Buchosa ni lini fidia zitalipwa na lini barabara itaanza kujengwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara anayoitaja ya Sengerema – Nyehunge hadi Kahunda yenye kilomita zisizopungua 82 ipo kwenye maandalizi. Kama nilivyosema kwa barabara iliyopita, ni kati ya barabara ambazo zinategemea kuanzia kujengwa kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka huu wa fedha. Kabla ya kuanza ujenzi sheria inatuambia tuwalipe kwanza fidia. Kwa hiyo, mara tutakapoanza kutangaza ujenzi huo, basi na wananchi watapatiwa fidia kwanza. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khamis Mbarouk Amour, Mbunge wa Tumbe, aulize swalii lake.

MHE. AMOUR K. MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kwanza jina langu lisomeke Amour Khamis Mbarouk.

SPIKA: Kwa hiyo, Khamis ndio jina la mwisho na Amour jina la kwanza?

MHE. AMOUR K. MBAROUK : Mheshimiwa Spika, Amour jina la mwanzo Khamis jina la pili na Mbarouk ndio la mwisho.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mbarouk, nadhani Makatibu mmeshalipata hilo vizuri.

Na. 155

Ushuru wa Mizigo kwenye Boti Bandari ya Dar es Salaam

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK aliuliza:-

Je, Serikali inakusanya jae ushuru kwenye Boti zinazoondoka saa moja kamili asubuhi katika Bandari ya Dar es Salaam ilhalil watumishi hufika kazini kuanzia saa moja na nusu na zaidi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*), pamoja na wadau wote muhimu ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), hutoa huduma za kibandari kwa saa 24 kwa siku saba za juma katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Utumishi kwa Wafanyakazi wa Bandari za mwaka 2019 zimetoa Mwongozo wa Muda wa Kuwa Kazini, ambapo wafanyakazi wote wa Bandari wanaopangiwa maeneo ya kutoa huduma kwa meli ama boti za mizigo hupaswa kuingia kazini kwa zamu (*shifts*) tatu kama ifuatavyo; saa 1:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri; *shift* ya kwanza; saa 9:00 alasiri hadi saa 5:00 Usiku; *shift* ya pili na saa 5:00 Usiku hadi saa 1:00 asubuhi *shift* ya tatu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, aidha, watumishi wa *TPA* wanaopangiwa zamu katika eneo la boti zinazosafiri kati ya Dar es Salaam na Zanzibar wanapaswa kuwepo kwenye eneo la kazi na kuhakikisha kuwa huduma zote muhimu za kibandari zinatolewa ikiwemo ukusanyaji wa mapato ya Bandari. Nitumie fursa hii kuitaka *TPA* kusimamia kwa karibu utaratibu uliowekwa. Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, swali la nyongeza.

MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri au majibu ya Serikali.

Kimsingi majibu ni mazuri sana, ila uhalisia ulivyo ni kwamba, abiria anaweza kuwa na mzigo akatakiwa kulipa, lakini akiuliza alipie ofisi gani, akakosa hiyo ofisi na akatakiwa kumpa fedha mkononi mchukuzi ambaye ndiye atamlipia itakapofika saa 1.30. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maswali mawili ya nyongeza; kwanza, naomba kujua ni mzigo wenyewe uzito kiasi gani ambao mtu akipita nao hapo bandarini atatakiwa kulipa? (*Makof*)

Pili, je, Serikali haioni umuhimu wa kupunguza au kuondoa kabisa ushuru wa wafanyabiashara wadogo wadogo wanaotoka Zanzibar kuja kuchukua biashara zao hapo Tanzania? Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk kama ifuatavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwanza nipokee shukurani za Mbunge kwa niaba ya Serikali. Pili, naomba kujibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza amezungumzia suala la uzito; anataka kufahamu ni uzito kiasi gani ambao anastahili ama anapaswa kulipa anapopita pale bandarini? leleweke kwamba Mamlaka yetu ya Bandari nchini inaongozwa kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 2004 na miongozo mbalimbali ikiwepo Mwongozo wa Mwaka, 2003 na Aya ya 12(1) na aya ya 71(1). Miongozo hii inatuelekeza kwamba mzigo wa abiria yejote anayetoka Bara ama kwenda Visiwani au Visiwani kuja Bara inatakiwa atozwe ukiwa hauzidi kilogram 21. Hilo la kwanza kupitia Mwongozo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, inaelekeza kwamba inatakiwa ujazo wa huo mzigo kwa maana ya *cubic measurements* usizidi moja, kwa maana ya ujazo wake ama nafasi inayochukua huo mzigo wako ni kiasi gani? Kuhusu wafanyabiashara wadogo kupunguziwa gharama pale bandarini; nataka nimhakikishie Mbunge ya kwamba kama wewe una bidhaa, kwa mfano, una balskeli au TVya matumizi yako binafsi, haitakiwi utozwe ushuru pale bandarini. Ila kama una zaidi ya hivyo, hii sheria itatuhusu sote. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Nadhani tutilie maanani ule wito ulioutoa na Mheshimiwa Naibu Waziri utatusaidia kufuatilia pale bandarini kwa hivyo viwango ulivyoweka. Kwa sababu wananchi wanapata usumbufu hata kwa bidhaa zile ambazo ni kwa ajili ya matumizi yao binafsi. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, swali la nyongeza. (*Makofii*)

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, tunajua bandari yetu ni mionganii mwa chanzo cha mapato, na kumeibuka kuwepo kwa bandari bubu zaidi ya 58 katika Mikoa mbalimbali ambapo Serikali yetu inakosa mapato. Naibu Waziri ulikuwa Mwenyekiti

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Kamati na huu ni mfupa mzito ambapo mapato ya Serikali yanapotea.

Je, ni lini sasa mchakato wa kuangalia hizi bandari zote kama walivyokuwa wameahidi walipokuja kwenye kamati. Ni lini sasa mtazirasimisha rasmi ikiwemo na badari ya Mbweni ili Serikali iweze kukusanya mapato ya kutosha na kupeleka maendeleo kwa Watanzania? Ahsante. (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE): Mheshimiwa Spika, kwanza nitambue Mheshimiwa Ester Bulaya kama ulivyo sema nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma changamoto hizi tuliziona na hivi sasa kati ya bandari zote nchini tuna bandari 693 nchi nzima ya Tanzania ambazo ni bandari bubu. Na tunazo bandari 66 tu ambazo ni rasmi. Bandari ya Mbweni ambayo ni miongoni mwa bandari 24 ambazo tutakwenda kuzirasimisha hivi sasa ninavyosema.

Mheshimiwa Spika, badari hizi zinaingiza fedha kwa mwaka shilingi milioni 200 kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa kurasimisha bandari bubu ambazo zinaingiza fedha Serikalini. Nitoe wito pia kwa kuwa siyo kila sehemu tutaajiri kama TPA kwa maana tutashirikiana na halmashauri husika katika maeneo hayo ili hizo bandari ziewe kurasimishwa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya maji Mheshimiwa Ali Anyihulile Jumbe

Na. 156

Usalama wa Maji yaliyoko Ardhini

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE aliuliza:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba maji yote yaliyopo ardhini yanabaki salama kwa

kuwa tone moja la *oil* (vilainishi) huharibu lita 600 za maji yaliyoko ardhini.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghali, Mbunge wa Kyela kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mWaka 2009 na Sheria ya Mazingira Na. 20 ya Mwaka 2004 kwa pamoja zinasisitiza uhifadhi, utunzaji na usimamizi wa vyanzo vya maji. Maji chini ya ardhi ni rasilimali ambayo inalindwa dhidi ya uchafuzi wa aina zote hii ni pamoja na *oil*. Hii ni kutokana na kuwa maji chini ya ardhi yakishaharibiwa ubora wake ni vigumu na ni gharama kubwa kuyasafisha ili yaweze kutumika kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia Bodi za Maji za Mabonde inaendelea na jukumu la kutambua vyanzo vya maji juu ya ardhi na chini ya ardhi, kuweka mipaka na kutangaza katika Gazeti la Serikali ili yalindwe kisheria. Hivyo, maeneo tengefu ambayo yametangazwa ni Saba (7) ambapo Sita (6) ambayo yalitangazwa mwaka 2016 yapo Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa maeneo ya Chokaa, Kidole, Kiswaga, Matundasi A, Matundasi B na Mkola katika Wilaya ya Chunyu Mkoa wa Mbeya na eneo moja Makutupora Mkoani Dodoma katika Bonde la Wami-Ruvu lilitangazwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, vilevile, maeneo Hamsini na Nne (54) katika Bodi ya Maji Bonde la Rufiji (16), Ziwa Tanganyika (3), Pangani (7), Wami/Ruvu (5) Ruvuma na Pwani ya Kusini (13), Ziwa Nyasa (8) na Ziwa Victoria (1), Bonde la Kati (1) yamewekewa mipaka ili yatangazwe mwaka huu 2022.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utekelezaji wa Mipango ya Uhifadhi wa Vyanzo vya maji, Wizara ya Maji inatekeleza kazi ya kuainisha miamba yenye maji (*Aquifer Mapping*) katika Mabonde manne ambayo ni Bonde la Kati, Pangani, Wami/Ruvu na Rufiji.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kutathmini maeneo yenye maji chini ya ardhi imekamilika na hatua inayofuata ni kuchimba visima ili kupata takwimu za wingi na ubora wa maji katika maeneo hayo. Baada ya hatua hii, itaandaliliwa ramani ili kutangaza maeneo hayo katika Gazeti la Serikali ili yalindwe kisheria na yaweze kutumika kulingana na mahitaji ya shughuli za maendeleo.

SPIKA: Mheshimiwa Ally Jumbe swali la nyongeza.

MHE. ALLY A. J. M. JUMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa Mto Kiwira unapita maene mengi sana ya Wilaya ya Kyela ikiwemo Vijiji vya Lema, Mwalisi, mpaka Bujonde. Na kwa kuwa mto huo umelalamikiwa na wananchi wa maeneo hayo kuwa na uchafuzi mkubwa ambapo inafikia hatua mto unanuka na unakuwa na rangi ya damu.

Je, ni lini Serikali itaunda Tume Maalum kufanya utafiti wa nini kinasababisha maji hayo yawe machafu?

Mheshimiwa Spika, mbili, kwa kuwa wananchi wengi wa eneo hilo baada ya kukosa maji ya Ngana wanatumia kwa ajili ya kunywa na kuoga. Je, ni lini Serikali sasa itaanza ujenzi wa mradi wa Ngana?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Ally amekuwa mfuatiliaji mzuri, amekuwa anakwenda zaidi ya uhitaji wa kupata maji yakiwa bombani lakini pia amekuwa akizingatia suala la usalama.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na bonde hili maji haya yanapochafuka, Mto Kiwira ni Mto ambao tunautumia kwa miradi mingi, naomba kutumia Bunge lako Tukufu kuagiza Bonde husika lifanye kazi kadri ambavyo inatakiwa kisheria. Vilevile Wizara tutaendelea kusimamia. Tayari Mheshimiwa Waziri amekuwa akitoa maagizo kadhaa kwa Mabonde yote kuhakikisha shughuli za maji kuwa salama yafanye usimamizi unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake la pilii la lini ujenzi wa Ngana utaanza, kwa furaha kubwa ninapenda kukuarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu tayari tumeshatangaza na hivi karibuni kabla yam waka huu wa fedha kuisha tutapata Mkandarasi na lazima kasi zije zianze kwa kasi kwa sababu tunafahamu umuhimu wake kulingana na jiografia ya eneo hilo. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Michael Kembaki swalii la nyongeza.

MHE. MICHAEL M. KEMBAKI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Mji wetu wa Tarime tunategemea chanzo kimoja kikuu cha maji ya Bonde la Ndurumo, lakini kumetokea baadhi ya watu kuanzisha *plant* za kuchenjua dhahabu kandokando ya chanzo hiki.

Je, Serikali inatuhakikishiaje watu wa Tarime kwamba maji tunayotumia yapo salama? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, maji yote ambayo yanafika kwa mlaji wa mwisho kwa maana ya mwananchi ni maji salama ambayo tayari Wizara kuititia Idara ya Maabara inakuwa imeshafanya kazi yake, hivyo ninapenda kuwatoa hofu wananchi wote wanaoishi

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kandokando ya wachimbaji kwamba maji yanafanyiwa kazi katika maabara.

SPIKA: Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza!

MHE. BENAYA L. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Mradi wa maji wa Litembo, Mahenge kutokea Mwogelo, mwaka jana niliuliza swali hapa na nikapewa majibu mazuri na Mheshimiwa kwamba tayari fedha imetengwa na mradi unaanza kujengwa. Kwa bahati mbaya mradi huu unatoa maji Litembo tu.

Je, ni lini maji yatatoka Mahenge na Langandondo?
(*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli anachokiongea Mheshimiwa Mbunge lakini Mheshimiwa Mbunge unafahamu kwa namna ambavyo tumekuwa tukiwasiliana tumeweza kufanya kazi sasa Litembo inapata maji. Kwa hiyo, maeneo haya ya Mahenge tayari tunapeleka Mkandarasi ambaye ataanza kazi hivi karibuni na kuona kwamba maeneo yote haya mawili yaliyobaki nayo yanakwenda kunufaika na maji bombani.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kwa pamoja kama ambavyo umekuwa ukifanya. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu sasa aulize swali lake.

Na. 157

Usambazaji wa Maji katika Vijiji vya Wilaya ya Meatu

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, ni lini Serikali itasambaza maji katika Vijiji vya Mwanjoro, Jinamo, Mbushi na Witamihya Wilayani Meatu baada ya ujenzi wa Bwawa la Mwanjoro kukamilika

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI aliuliza: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, vijiji vya Mwanjoro, Jinamo, Mbushi na Witamihya kwa sasa vinapata huduma ya maji kwa wastani wa asilimia 24 kuitia visima vifupi 13.

Mheshimiwa Spika, bwawa la Mwanjolo lilikamilika mwishoni mwa mwaka 2018 likiwa na lengo la kuhudumia vijiji vya Jinamo, Mbushi na Mwanjoro, lakini katika utafiti uliofanyika hivi karibuni bwawa hilo limeonekana kupungua kina kutokana na kujaa kwa mchanga unaosababishwa na kunyweshea mifugo na changamoto ya uharibifu wa mazingira iliyopelekea pia kuathiri ubora wa maji hayo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa Bwawa la Mwanjolo linatumika kusambaza maji vijiji vya Mwanjoro, Jinamo, Mbushi. Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 itatenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Bwawa la Mwanjolo ambapo ukarabati huu utahusisha kuongeza kwa kina cha bwawa, kujenga kingo za bwawa ambazo kwa sasa zimechakaa. Kujenga miundombinu ya kuzuia mchanga kuingia katika Bwawa (*sand trap*) pamoja na upandaji wa miti na nyasi ili kuzuia mmomonyoko wa ukuta. Pia katika bajeti hiyo Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kunyweshea maji mifugo ili wafugaji wasiweze kuingiza mifugo yao kwenye bwawa na mwisho wananchi wa maeneo haya watapewa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu vijiji hivi pia vitawenza kunufaika na mradi mkubwa unaotarajia kujengwa katika Mkoa wa Simiyu kuitia *program* ya mabadiliko ya tabia ya nchi maana vijiji hivi vya Mwanjoro viro umbali wa kilomita 12 toka kwenye eneo la ujenzi wa bomba kuu.

SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya swali la nyongeza.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Rais na Wizara kwa kuidhinisha na kutekeleza mradi wa dharura katika Mji wa Mwaluzi siku si chache wananchi wataanza kunufaika na Mto semu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto zilizoainishwa katika majibu ya Serikali ninamuomba Mheshimiwa Naibu Waziri afike Jimbo la Meatu katika Bwawa hilo ilia one hizo adhan a kuchukua hatua za haraka ili kunusuru bwawa hilo lililogharimu Shilingi Bilioni 1.8 bila kunufaisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mradi huu ulitekelezwa na Wizara, RUASA Wilaya kwa mwaka uliotajwa tayari mipango mingine imewekwa. Je, ukarabati huu utafanywa kwa ngazi ya Mkoa au ngazi ya Wizara? Ninakushukuru. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninapenda kupokea pongezi na kwa hakika tuna kila sababu ya kuendelea kumuombea Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameitendea haki hii Wizara ya Maji. Tumeendelea kupata fedha na ndiyo maana tunaona kila kona miradi ya maji inaendelea kutekelezwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kufika Meatu ni moja ya taratibu zangu za kazi, naomba nikupe taarifa Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote wanaotoka Mkoa wa Simiyu ratiba yangu ni kuanzia tarehe 25 mwezi huu kuwa Simiyu hivyo tutafika maeneo haya yote korofii ili kuona tunafanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ukarabati tutafanya kwa kushirikiana na watendaji wetu amba wapo katika Mkoa ule na Wizara hatuna pa kukwepea ni lazima tuwajibike katika hilo. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Stansalau Nyongo swali la nyongeza.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kabisa kwamba atakuja katika Mkoa wa Simiyu, na kwa kweli katika Mkoa wa Simiyu tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha kwa ajili ya mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria.

Je, katika Wilaya ya Maswa kuna vijiji ambavyo mradi huu unapita mbali na kuna mabwawa ambayo yameachwa siku nyingi kwa mfano bwawa la Mwamanenge, Mwamashindike, Bushitara, Mwantonja, Nyangiganwa, Sola na Lalago. Mheshimiwa Waziri uko tayari kupitia tena katika maeneo haya na kutoa *commitment* ya Serikali kuyafufua mabwawa haya kwa ajili ya kuwapelekea matumizi ya maji wananchi wa Wilaya ya Maswa? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri umeshasema unaenda Simiyu, unalo jambo la nyongeza hapo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Hapani!

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Waziri ameonesha hana ubishi kupitia hayo maeneo kwa sababu anakuja kwenye Mkoa wako na ameshasema hapa. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Spika, Jimbo la Shinyanga Mjini katika Kata za pembedni, Kata ya Chibe, Mwalili, Old Shinyanga, Kizumbi na Mwawaza kuna shida kubwa sana ya maji, watu wanakunywa maji ya kwenye madimbwi.

Ni nini mpango wa Serikali kupeleka mtandao wa maji kwenye Kata hizi kwa sababu hata sasa ukiwfua Mamlaka ya Maji wanassema hawana fedha kwa ajili ya kupeleka maji safi na salama. Nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wanapeleka fedha na kupeleka maji katika Kata hizo za pembezoni.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Makamba, maeneo ya Shinyanga Mjini ni kweli imekuwa ni moja ya maeneo ambayo yamekuwa changamoto ya maji, lakini Wizara hapa tulipo chini ya uongozi thabitii wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan siyo Wizara ya wananchi kunywa maji kwenye madimbwi.

Mheshimiwa Spika, hili tayari tumeendelea kulifanya kazi na maeneo haya yote ambayo bado yana changamoto, Wizara tutaleta fedha, tutasimamia kuhakikisha kwamba Majimbo yote, maji yatapatikana ili kuona wananchi wanapata maji safi bombani na ya kutosha. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Spika, ninataka kujua ni lini Serikali itakamilisha mradi mkubwa wa maji wa Mwanga, Same, Korogwe ili kusaidia usambazaji wa maji kwenye vijiji vyta Kata ya Mtomazi na Mkumbara katika Wilaya ya Korogwe? (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Mahundi majibu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mradi mkubwa ambao umeshachukua muda mrefu lakini Wizara tunaendelea kutekeleza tunaamini ndani ya muda wa usanifu tunakwenda kukamilisha wa *phase* hii ambayo tupo. Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana na hongera kwa kuendelea kufuatalia mradi huu muhimu. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Zuberi Muhammed Kuchauka, Mbunge wa Liwale sasa aulize swali lake.

Na. 158

Udanganyifu kwenye Mikataba ya Ujenzi wa Minara ya Simu Katи ya Makampuni ya Simu na Wenyе Maeneo

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA aliuliza: -

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya udanganyifu mkubwa kwenye mikataba ya Ushuru wa kampuni za Simu na wenyе maeneo pale panapojengwa minara ya simu kiasi cha kusababisha ushuru kwenda kwa watu wasiohusika.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Lukundo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI aliibusi: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swalı la Mheshimiwa Zubeir Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa huduma ya mawasiliano kwa mtumiaji wa mwisho huwezeshwa na minara ambayo kwa kiasi kikubwa hujengwa ardhini, lakini pia husimikwa katika majengo marefu, hususan katika

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maeneo ya miji mikubwa. Ardhi ambayo hutumika katika ujenzi wa minara humiliikiwa na wananchi ama taasisi za umma au taasisi za kijamii ambapo hupangishwa kwa mto huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, katika kubaini eneo linalopaswa kujengwa mnara wa mawasiliano vigezo mbalimbali nya kitaalam hutumika kama vile uimara wa ardhi, eneo linalowezesha mnara husika kuwasilisiana na minara mingine na maeneo yanayoweza kufikiwa na mawasiliano kuitia mnara husika. Vigezo hivi na vingine ndio vinaweza kuamua mahali sahihi ambapo mnara unaweza kujengwa. Kwa utaratibu uliopo sana, eneo likibainika kukidhi vigezo nya kitaalam, mto huduma hufanya mawasiliano na mmiliki wa eneo husika pamoja na Serikali ya eneo hilo ili eneo hilo liweze kujengwa mnara wa mawasiliano. Mto huduma huingia mkataba na mmiliki wa eneo ambapo mmiliki huyo hulipwa fedha ya pango la ardhi kulingana na makubaliano yaliyofikiwa ambayo ndiyo huwekwa katika mkataba.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya minara ya mawasiliano ikiwemo kufuata taratibu katika upangishaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa minara. Vilevile Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umetoa maelekezo katika mikataba wanayoingia na Kampuni za Simu kufuata taratibu zote katika kukodi ardhi ambapo minara hiyo hujengwa kuitia halmashauri husika. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zubeir Kuchauka, swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nitoe shukrani kwa majibu mazuri ya Serikali juu ya swali langu, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, kwani upo udanganyifu uliofanywa katika Kijiji cha Kibutuka na aliyejewa mfanyakazi

wa *tiGO*, alienda pale akadanganya wanakijiji kwamba, anahitaji eneo la kujenga mnara, baadaye wanakijiji walimpa bure wakitumia mukhtasari ule yule sasa hivi anekuwa ndio mnufaika wa kodi ya mnara ule badala ya kuwa wanakijiji waliopo katika kijiji kile.

Je, Serikali ina mkakati gani au ina kauli gani juu ya utapeli wa huyu mtumishi wa *tiGO* ambaye yeche anajifanya kwamba, ndio mmiliki wa lile eneo wakati aliliomba apewe bure?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; pamoja na kwamba, Vijiji vya Ndapata, Ndunyungu, Makata, Mtawatawa, Kipelele, Makinda na Nambinda havina mawasiliano ya kutosha. Nini mkakati wa Serikali wa kutuwashia ile minara ambayo tayari imeshawashwa kwenye baadhi ya vijiji hapa nchini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Kundo; swalii la pili la nyongeza; kuhusu swalii la kwanza ni swalii mahususi kuhusu huyu mtumishi wa *tiGO*, kama unayo majibu unaweza kutoa, la sivyo, Mheshimiwa Mbunge akuletee taarifa mahususi kuhusu huo utapeli na sheria zichukue mkondo wake. Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipengele cha kwanza. Ni kweli kabisa changamoto ya udanganyifu uliojitokeza tunaifahamu, lakini tayari suala hili lilikuwa limeshafika mahakamani na lilikuwa limeshatolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu pia migogoro ya ardhi inapotokea kwa Sheria Na.2 ya Mwaka 2002, tunafahamu kabisa kwamba, hili linahusisha Wizara ya Ardhi moja kwa moja, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa

changamoto hii ambayo imejitokeza tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Ardhi, ili tuweze kujua namna gani tutatatua changamoto hii ambayo imejitokeza katika eneo husika.

Mheshimiwa Spika, vilevile swalii la pili ni kuhusu minara ambayo haijawashwa. Ni kweli kabisa katika maeneo ya Jimbo la Liwale, kwanza kabisa labda tuseme kwamba, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana katika ujenzi wa minara ndani ya nchi yetu, likiwepo Jimbo la Liwale. Ni takribani bilioni 19.56 imewekezwa katika minara 161 ambapo tunatarajia katika kipindi cha miezi miwili mitatu minara hii ambayo tayari imeshasimama itahakikisha kwamba, itakuwa imeshawashwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imefanya uwekezaji mwingine wa minara 127 ambayo iko katika hatua za *civil works*. Katika kipindi cha miezi miwili mitatu, tunaamini kabisa kwamba, minara hii itakapokamilika, naamini maeneo mengi yatakuwa yamepata ufumbuzi wa changamoto hizi za mawasiliano, likiwepo Jimbo la Mheshimiwa Kuchauka ambalo ni Liwale. Nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Condesta Sichalwe, swalii la nyongeza.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo imewapata wananchi wa Liwale, imewapata pia wananchi wa Kata ya Kapele, Kijiji cha Namchinga. Kampuni mbili za Simu ambazo ni tiGO pamoja na Halotell ziliingia mikataba ya udanganyifu kwa kuwarubuni wananchi ambapo ilipaswa mapato yao yawe yanalipwa kwenye Serikali ya Kijiji, lakini mapato haya yanaingia kwenye mifuko ya watu binafsi. Je, ni nini kauli ya Serikali kutusaidia jambo hili kwa sababu, tumeshughulikia kwenye ngazi ya Wilaya tumeshindwa, tunaomba Wizara itusaidie. [Maneno yaliyotajwa hapo juu siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

SPIKA: Sasa ili twende vizuri kikanuni, umesema aliyefanya udanganyifu ni kampuni au ni? Maana umetaja hapo kampuni mbili, nataka kuwa na uhakika, aliyefanya udanganyifu ni nani?

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kama ambavyo alielezea Mheshimiwa Kuchauka hapo awali, watu hawa wakati wanaenda kuingia mikataba na wananchi wanadanganya. Wanatangulia kwa kuwarubuni...

SPIKA: Ngoja, tuelewane vizuri. Waliofanya udanganyifu kuna wananchi au wamefanya udanganyifu makampuni uliyoyataja, ndio swali langu?

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, ni kampuni pamoja na hao wananchi ambaao wao wananaufaika.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, ukiituhumu kampuni humu ndani, nadhani unajua kanuni zetu zinakopelekea jambo kama hilo. Ukiituhumu kampuni humu ndani kwa kuitaja kampuni fulani na fulani imefanya utapeli, uwe na uhakika nalo, ndio maana nilikuwa nakupa nafasi kwa sababu, anaweza kuwa ameenda mtu, kama Mheshimiwa Kuchauka alivyosema, yeye ameeleza wazi ni mtu ameenda kutapeli wanakijiji. Wewe Mheshimiwa unasema ni hizo kampuni ulizozitaja wewe ndio zilizoenda kutapeli, hebu fafanua vizuri, nakupa hiyo nafasi ya mwisho.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Wakati kampuni hizi zinaenda kutafuta maeneo, watumishi wanatangulia kutafuta maeneo kwa kuwarubuni wananchi kwamba, wanapaswa kununua maeneo, ilhali baadhi ya maeneo yalikuwa ni maeneo ambayo yanapaswa kumilikiwa na Serikali ya Kijiji. Kwa hiyo, badala ilipwe Serikali ya Kijiji wanaolipwa sasa hivi ni watu binafsi ambaao walidanganya pamoja na wale watumishi ambaao wanatoka kwenye hizo kampuni za simu.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ni kazi yangu kusimamia utaratibu hapa mbele, ikiwa ni pamoja na kuwalindia heshima wale walio nje ya hapa kama mtu hana ushahidi, kama Mbunge hana ushahidi.

Mheshimiwa Mbunge kwa maelezo uliyotoa mara ya pilii sijapata uhakika wako kwamba, hao walitumwa kwenda kwenye hivyo vijiji walitumwa na hizo kampuni. Ningepata huo uhakika ningempa nafasi Mheshimiwa Waziri na mimi kesi za namna hii kidogo, nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri ukutane na Mheshimiwa Mbunge kwa sababu anasema kesi hiyo wameshafikisha mpaka wizarani, lakini kwa maelezo yake sipati muunganiko katika hawa anaosema watu wametumwa na kampuni, huenda hizo kampuni hazijawatuma. Hebu limalizeni hilo jambo ili wananchi wake waweze kusaidiwa na mimi sitaki kuingia kwenye huo mgogoro wa mambo kama hayo ama kumtia Mheshimiwa Mbunge kwenye mgogoro. Kwa hiyo, hili swali lake alilolitaja kuhusu hizo kampuni linaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka kwa upande wa Serikali. Ninayo matangazo hapa:-

Tutaanza na Tangazo la Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokuwepo Bungeni. Wakati huo amemteua Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa kwamba ndiye atakayekuwa Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni wakati ambao Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa hayupo hapa Bungeni. Kwa hivyo, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa anakaribishwa kwenye kitikile ambacho huwa anakaa Kaimu Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, matangazo mengine na niwakumbushe kwa sababu, kama nilivyosema ni kazi yangu kusimamia kanuni hapa; Wabunge waliosimama wanapaswa kukaa kwa sababu, mimi nimesimama. Wabunge wanaotembea wanapaswa kukaa kwa sababu, mimi nimesimama. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Naona Kaimu Kiongozi bado anatembea, inabidi... (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zinataka anayekuwa anaongoza kikao hapa mbele akisimama Wabunge wote tukae ili awe amesimama mtu mmoja hapa Bungeni na mwingine namwona anatembea na yeye na mwingine na mwingine, tukae Waheshimiwa Wabunge. (*Kicheko/Makofi*)

Wageni waliopo Jukwaa la Spika; kwanza ni wageni wangu wawili kutoka *Omega Churches Dar es Salaam*; na hawa ni Ndugu Nabii Samuel Samson Rolinga na Ndugu Clement Mwabungulu. Karibuni sana Bungeni Watumishi wa Mungu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge; kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Hamad Chande ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na huyu ni Afisa Mahusiano Chuo cha Uhasibu Arusha, Ndugu Elina Benson Mwangomo. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ambaao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai na watumishi *SACCO*Sya Walimu kutoka Hai, Mkoani Kilimanjaro, wakiongozwa na Mheshimiwa Edmund Rutaraka. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Grace Victor Tendega ambaao ni baba yake mzazi na mwanafamilia kutoka Mkoani Iringa; baba yake ni Ndugu Victor Tendega Mpanda. Karibu sana, sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Grace Tendega namwona amefurahi sana hapo ametembelewa na baba Bungeni. Karibu sana baba yetu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Mwitwa Kembaki, ambaao ni Madiwani kutoka Nyamisangura, Tarime Mjini, Mkoani Mara. Waheshimiwa Wabunge hawa ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Madiwani, sijui kama wametokaje sehemu moja, lakini acha niwataje; Mheshimiwa Veronica Francis Mwise Mheshimiwa Diwani. Tunaye pia Diwani mwingine Mheshimiwa Tobas Ghati naye ni Diwani. Tunaye pia Mheshimiwa Chacha Ludovic ambaye ni Mjumbe wa CCM Wilaya ya Tarime. Karibuni sana, huyu wa mwisho hapa, nadhani huyu ni ndugu kwa sababu, kule CCM tunaitana ndugu. (*Makofi*)

Wageni 35 wa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben ambao ni Viongozi wa Serikali ya wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Mkoa wa Morogoro, wakiongozwa na Rais wa Chuo Ndugu George Lubeleje. Karibuni sana. (*Makofi*)

Sasa huyu George Lubeleje ndio yupi? Hivi inaonekana huu ukoo majina ya George ndio yenyewe hayo? Maana hata yule Mbunge tuliye kuwa naye hapa alikuwa anaitwa George Malima Lubeleje na huyu naye anaitwa George Lubeleje, karibu sana. Bila shaka hili jina ni la mtu maarufu sana kwenye ukoo.

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza ni Mheshimiwa Stefania Cheyo, huyu ni Mheshimiwa Diwani kutoka Simiyu. Amekuja kutembelea Bunge, karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Ndugu Elizabeth Timoth na Ndugu Mathias Magove na Ndugu Fabian Chajama, wote hawa wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na wote wanatoka Simiyu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wanafunzi 90 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Shalom ya Njiro, Jijini Arusha. Karibuni sana watoto wetu na Walimu hapo, tunaamini mmejifunza mawili, matatu mlipohudhuria kipindi chetu cha maswali na majibu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo lingine hapa, tangazo muhimu kabisa. Jana Mheshimiwa Naibu Spika alipokuwa hapa aliwatangazia Waheshimiwa Wabunge namna ambavyo siku ya leo ni ya muhimu kwetu kama Bunge, lakini ni ya muhimu kwetu kama *Bunge Sports Club*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Sasa hili tangazo litanichukua muda kidogo, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tulisikilize ili tutiane moyo katika mambo ambayo Wabunge wenzetu huwa wanatuwakilisha. (*Makofii*)

Sasa, jana ilitangazwa kwamba, leo kutakuwa na tafrija mara baada ya shughuli za Bunge, lakini kabla hatujaenda huko kwenye tafrija, lazima tutambue humu ndani ya Bunge kazi nzuri iliyofanywa na *Bunge Sports Club* kwa niaba ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Sasa siku ya leo tunawasilisha makombe katika Bunge tuliyoyapata kutokana na ushiriki wetu katika Michezo ya 11 ya Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo yalifanyika Jijini Arusha kuanzia tarehe 4 hadi 17 Disemba, 2021. Timu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanikiwa kushinda vikombe nane na kuibuka mshindi wa jumla katika michezo hiyo; maana yake nchi zote za Afrika Mashariki Tanzania ndio iliongoza. Tanzania kwa maana ya Bunge hili liliongoza. (*Makofii*)

Michezo ambayo Timu ya Bunge ilipata vikombe na ambayo tutakabidhiwa rasmi na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* kwenye tafrija yetu, niyataje hapa makombe hayo ambayo tutakabidhiwa leo baadaye na yatakuwa yanaonesha humu ndani. Maana yameingia humu ndani ili kuwatia hamasa Wabunge ambao hawahudhurii sana, michezo hii ni ya muhimu sana. (*Makofii*)

Kwanza ni kikombe cha mchezo wa mpira wa miguu. Ahsante sana. Hapa nilikuwa nashawishika sijui niwasimamishe wale waliocheza mpira huu? (*Makofii*)

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Haya, wachezaji wa mpira wa miguu wasimame. Waliotuletea kombe na kombe likiwa limesimama pale. (*Makofii*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge ni dhahiri kwamba, kwa sababu nimeziona sura kadhaa ambazo zimevamia, ni dhahiri wanao utayari wa kuingia kwenye timu yetu ya mpira wa miguu. Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi, tuwakaribishe, tuwaangalie vizuri wote waliosimama. (*Makofi*)

Pia, tunao mchezo wa mpira wa pete. Wachezaji wa *Netball*/wasimame tuwapigie makofi na kombe lao. (*Makofi*)

Haya, sasa hapa Waheshimiwa Wabunge namwona na Mheshimiwa Flatei Massay amesimama. Ahsanteni sana kwa namna ya kipekee kabisa kwa sababu, mchezo huu wa mpira wa pete anacheza Spika wenu, lakini pia anacheza Mheshimiwa Salma Kikwete. Kwa hiyo, kipekee kabisa niwataje hao wawili tutakuwa tumewawakilisha akinadada wote na akinamama. (*Kicheko/Makofi*)

Mchezo wa mpira wa wavu, *Volleyball*, wanaume. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mchezo wa mpira wa wavu, *Volleyball*, wanawake. Haya, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mchezo wa mpira wa wavu, *Volleyball*, wanaume na wanawake hawa huwa wanaitwa *The Dons*. (*Makofi*)

Haya, mchezo wa Mpira wa Kikapu (*Basketball*) Wanaume wasimame, nao walileta kikombe na kombe lao pale lioneshwe. (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, kazi nzuri ilifanyika...

WABUNGE FULANI: Wako watano. (*Kicheko*)

SPIKA: Wako zaidi ya hapo, wengine wameenda canteen kidogo. (*Makofi*)

Mchezo wa Mpira wa Kikapu (*Basketball*) wanawake wameleta kikombe. Ahsanteni sana. Wewe ukiwaona tu,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

unaziona zile nguvu za kusukuma mle ndani, wako vizuri.
(*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao mchezo wa Kuvuta Kamba Wanaume. Ahsanteni sana. Hawa watu wa kuvuta kamba huwa wanaitwa wazee wa simika. Ahsanteni sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Aidha, timu ya Bunge la Tanzania ilishika nafasi ya pili katika michezo ifuatayo; kwanza, ni mchezo wa Kutembea kwa Kasi (Wanawake). Nina uhakika kuna Wabunge hawajaelewa vizuri hapa. Mchezo wa kutembea kwa kasi, aliyeshinda hapa ni mimi. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Ahsanteni sana. Mchezo wa Kutembea kwa Kasi (Wanaume), tulikuwa wa pili pia. Mheshimiwa asimame, yuko kona gani? yuko wapi jamanii! Haya, ahsante sana, tutamwona baadaye. Pia Mchezo wa Kuvuta Kamba (Wanawake), sasa wasimame wapigiwe makofi na wao. ahsanteni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kama nilivyosema, taarifa zaidi za nani alituwakilisha kwenye mchezo gani, zitaendelea baadaye. Riadha nadhani walikusudia utangazwe baadaye, lakini kwa namna ya kipekee, pamoja na kwamba kwa maana ya nchi walishinda wenzetu Uganda, lakini hapa Tanzania tuliwakilishwa vizuri sana kwenye mbio mbalimbali ndefu na fupi Mheshimiwa na Anatropia Rweikiza. (*Makofi/Vigelegele*)

Kwa kuwa tumetambua hawa ambao wanacheza mchezo mtu mmoja mmoja na nafasi ambazo walikuwa amezishika kwa upande wa *Golf* (Wanawake), Tanzania ilishinda kwa maana ya *pointsnyingi*, aliongoza Mheshimiwa Neema Mgaya. Ahsante sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Baadaye tutatoa maelezo zaidi ili Waheshimiwa Wabunge wengi zaidi tujitokeze kwenye mazoezi na michezo ili kuongeza ushiriki wetu kwa maana ya idadi na pia ushindani. Ninalo pia tangazo lingine kutoka kwa Mheshimiwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Fredy Atupele Mwakibete ambaye ni Katibu wa Chama cha Wabunge Vijana, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge Vijana; sasa hapa vijana wametajwa umri jamani, maana huko tusije tukatokeza na wenzangu na mimi. Wale ambao ni Wabunge ambao wana umri wa chini ya miaka 40 kwamba kesho ljumlah saa sita mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa kwa madhumuni ya kufanya uchaguzi wa Uongozi wa Chama cha Wabunge Vijana hapa Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mnaombwa mhudhurie huko, wale ambao umri unawaruhusu ili mkachaguliwe na pia kushiriki kuchagua viongozi wenu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo niliyoyaleta kwenu, sasa tunaendelea na ratiba iliyoko mbele yetu. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Maafa wa Mwaka 2022

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Muswada umesomwa kwa Mara ya Kwanza, unaoitwa Muswada wa Usimamizi wa Maafa wa mwaka 2022. Kwa mamlaka niliyonayo chini ya Kanuni ya 97, ninauelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria ili uweze kufanyiwa kazi.

Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo la ziada na nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa kuwa huu ni Muswada ambao umeletwa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, naamini sasa tutakapokuwa tunaleta, kama kutakuwa na yale mabadiliko, tutafurahi humu ndani kwa sababu Wabunge watakuwa wanaleta sasa hayo mabadiliko kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

lugha ya Kiswahili. Ahsanteni sana Serikali na tuna wapongeza sana. (*Makof*)

Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali PAC kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021 na Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*Public Accounts Committee*) Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

MHE. NAGHENJWA KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Taarifa ya Mwaka ya Kamati kuhusu Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Ulipoishia Tarehe 30 Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia zawadi ya uhai, hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa leo hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, nakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwenyezi Mungu akupe afya njema katika kutekeleza majukumu yako. Pia nampongeza Mheshimiwa Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika, naye tunamwambia Mungu aendelee kumpa afya njema. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 136 kifungu cha 15 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kuhusu shughuli zilizotekelawa katika mwezi Februari, 2021 hadi Februari, 2022 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) liipokea na kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020. Kamati ilijielekeza katika kubainisha thamani ya pesa iliyotumika katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa (*Value for Money*), uzingatiaji wa bajeti, kiasi cha matumizi ikillinganishwa na mahitaji halisi, na Matokeo ya Taarifa za Kaguzi Maalum zilizofanyika zilizofanyika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kutohana na vigezo ambavyo vimefafanuliwa kwa kina katika taarifa hii, naomba sasa kuwasilisha hoja 17 ambazo Kamati inaomba Bunge lako lizijadili kwa kina na kuzizingatia katika kuimariswa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza, ni Matokeo ya Ukaguzi Maalum wa Kiuchunguzi kuhusu Ununuzi na Usimikaji wa Mfumo wa *ERP* katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*). Kamati ingependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba kwa mwaka wa fedha 2019/2020 *CAG* alifanya Ukaguzi Maalum wa Kiuchunguzi ili kubaini dosari za usimikaji wa mifumo mbalimbali katika *TPA*. Ukaguzi huu maalum wa kiuchunguzi uliangalia masuala ya ununuzi, na usimikaji wa mfumo wa *ERP* uliotekelawa na *TPA* katika mwaka 2010 hadi 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, matokeo ya ukaguzi yamebainisha namna ambavyo Serikali kuititia *TPA* ilipata hasara ya takriban shilingi za Kkitanzania bilioni 3.2 na Dola

za Kimarekani milioni 2.3 kutokana na dosari za ununuzi na usimikaji wa mfumo wa *EPR*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Hoja ya pili ni hali ya mtaji katika kampuni ya ndege Tanzania *ATCL* na changamoto za kimkakati kati ya *ATCL* na *TGFA*. Katika *ATCL* Kamati imebainisha hoja kubwa mbili ambazo Serikali inatakiwa kuzifanyia kazi haraka. Kwanza ni uwepo wa madeni makubwa ya siku za nyuma ambayo hayajalipwa. *ATCL* inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 152.2. Deni hili linajumuisha deni linalodaiwa na *TGFA* kiasi cha shilingi bilioni 70.9 yaani 47% ya deni lote.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuna deni la kiasi cha shilingi bilioni 87.2 ambayo ni 59% ya deni lote ambapo ni deni la kampuni ya *Walis Red Income* iliyokuwa imeikodishia *ATCL* ndege mlaaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili katika *ATCL* ni changamoto za kimkataba kati ya *ATCL* na *TGFA* (*Aircraft Lease Contracts*). Kamati imebaini uwepo wa vifungu kadhaa vya kimkataba ambavyo vinasababishia *ATCL* kuongeza deni.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya hesabu za *TRA* kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 2030. Taarifa ya ukaguzi wa makusanyo ya faida kwa upande wa fedha kwa Tanzania Bara imebainisha kiasi halisi kilichokusanya kilikuwa shilingi trillioni 17.6 ukilinganisha na makadirio ya kiasi cha shilingi trillioni 19.1. Kwa msingi huo, kulikuwa na nakisi ya makusanyo ya kiasi cha shilingi trillioni 1.4 ambapo ni sawa na asilimia 7.6 ya makadirio ya makusanyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tanzania Zanzibar, *TRA* ilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 281.8 ukilinganisha na makadirio ya kiasi cha shilingi bilioni 350.1, hivyo kuwepo nakisi ya makusanyo ya kiasi cha shilingi milioni 68.3 sawa na 19.5% ya makadirio.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati katika *TRA* ni uwepo wa mashauri mengi ya kodi yenye thamani ya shilingi triliioni 366.1 ambayo hayajaamuliwa kwa wakati, hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne ni uchambuzi wa hali ya kifedha na mtaji katika Shirika la Umeme (*TANESCO*). Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Umeme (*TANESCO*) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020 umebaini kuwa kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi Shirika lilipata faida ya kiasi cha shilingi bilioni 45.2 ukilinganisha na hasara ya shilingi bilioni 34 iliyoripotiwa kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, hesabu za *TANESCO* zimebainisha uwepo wa changamoto kubwa mbili. Kwanza, ni deni ambalo *TANESCO* inadai kwa watu binafsi na taasisi za umma kiasi cha shilingi bilioni 4,022.3, kwa upande mwingine *TANESCO* nayo inadaiwa ikiwemo deni la Songas kiasi cha shilingi bilioni 493. Hali hii inaathiri mizania ya hesabu ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano ni ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Katika ukaguzi wa mwaka 2019/2020, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua hesabu za mifuko ya hifadhi ya jamii. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Serikali; *PSSSF*, *NSSF* na *NHIF*. Hoja kubwa ambayo imepewa msisitizo na *CAG* katika mifuko ya hifadhi ya jamii ni uwepo wa deni la muda mrefu ambalo mifuko inadai kwa taasisi mbalimbali na hasa Serikali. Madeni hayo yanapunguza ufanisi wa kiutendaji wa mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, kwa *PSSSF* ambapo deni lilihakikiwa, ilikuwa shilingi bilion 731. *CAG* aliifahamisha Kamati kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021, Serikali ilikuwa imetoa kiasi cha shilingi bilioni 500 kupunguza deni husika. Aidha, kwa mwaka huu Serikali imetoa hati fungani maalum isiyo taslimu (*Special Known Cash Bond*) yenye thamani ya shilingi triliioni 2.17 ili kulipa deni la *PSSSF*.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizi madhubuti ilizochukua kwa upande wa *PSSSF*, hali ambayo itasaidia kuimarisha mtiririko wa fedha wa mfuko na malipo ya mafao kwa wastaafuli kwa wakati. Hata hivyo, hoja ya madeni katika mifuko ya *NSSF* na *NHIF* bado inahitaji jitihada za Serikali katika kuimaliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *NSSF* hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 deni la Serikali lilikuwa kiasi cha bilioni 214.2 wakati kwa upande wa *NHIF* deni lilikuwa kiasi cha shilingi trillioni 1.174; na madeni haya pamoja na kupunguza ufanisi wa mifuko husika, lakini pia yanaharibu taarifa za mizania za fedha ya mifuko kinyume na kanuni za Kimataifa za uandaaji wa hesabu (*IFRS*).

Mheshimiwa Spika, hoja ya sita, ni hali ya mtaji na ongezeko la mikopo chechefu katika Benki ya Biashara Tanzania baada ya kuunganishwa na Benki ya *TIB* Biashara. Uamuzi wa kuziunganisha *TIB* Biashara na *TPB* umesababisha ongezeko kubwa la mikopo chechefu (*Known Performing Loans*) hali ambayo inaathiri hesabu za benki mpya ya *TCB*. Ni kwa msingi huo madeni chechefu yaliyorithiwa ya *TCB* yanakula mtaji wa *TCB* ambayo hapo awali ilikuwa ikifanya vyema sokoni. Mikopo chechefu imeongezeka kutoka 5.87% mwaka 2019 hadi 15.1% mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, hoja ya saba ni uchambuzi wa taarifa ya ukaguzi ya ufanisi (*Performance Audit Report*), ya utekelezaji wa mradi wa uzalishaji sukari, Mbigiri. Taarifa ya *CAG* imebainisha masuala kadhaa katika utekelezaji wa mradi wa uzalishaji sukari katika eneo la Mbigiri. Masuala hayo yanatakiwa yafanyiwe kazi kwa haraka ili kuhakikisha malengo ya mradi yanafikiwa. Mapendekezo 12 yametolewa ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nane ni kasi ndogo ya uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa kuititia *NIDA*. Uhakiki uliofanywa na *CAG* katika Kituo cha Uzalishaji cha Kibaha, tarehe 23 Septemba, 2021 ilibaini kuwa mashine tatu kati ya

tano zilizopo kituoni hazitumiki kutokana na kukosa *ribbon* pamoja na matengenezo (*maintenance*). Aidha mashine mbili mpya ambazo zinafanya kazi, kasi yake ya uzalishaji ni kadi 1,000 kwa saa badala ya kasi inayotakiwa ya kadi 4,500 kwa saa.

Mheshimiwa Spika, hali hii imesababisha *NIDA* kutokuwa na ufanisi wa kutosha pamoja na kutumia fedha nydingi za Serikali katika manunuzi ya mitambo mara kwa mara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya tisa ni usimamizi wa mapato ya Serikali katika Tume ya madini. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 Sura 123 na Kanuni ya 5(4) ya sheria ya husika kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 7 ya Mwaka 2017, inatoa maelekezo ya namna bora ya usimamizi wa rasillimali za madini yanapokuwa yakisafirishwa nje ya nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeamua kuileta hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu kutokana na mkanganyiko uliojitokeza kati ya maelezo ya Tume ya Madini na CAG. Pamoja na maelezo ya Tume ya Madini kuwa nyaraka husika zinapatikana *TRA* ili kudhibiti mapato ya Serikali, hata hivyo hadi ukaguzi unakamilika *CAG* alifahamisha Kamati kuwa nyaraka za usafirishaji madini za kiasi cha shilingi bilioni 159.32 zilikuwa hajijawasilishwa kwa uhakiki. Hoja hii inahusu mapato ya Serikali, hivyo inahitaji majibu na maelezo yenye uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi, masuala ya utawala bora na uwajibikaji wa kifedha katika mabonde ya maji hapa nchini; Serikali imeanzisha jumla ya mabonde ya maji tisa kupitia mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 10 ya mwaka 1982.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati katika eneo hili ni kuhusu kutooundwa kwa Bodi za Wakurugenzi katika mabonde ya maji hapa nchini. Aidha, taarifa za ukaguzi zimebainisha kutokamilika kwa miundo ya utumishi katika mabonde ya maji

halii inayoathiri usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na moja; ongezeko la riba ya shilingi bilioni 2.19 kila mwaka kutokana na kutolipwa kwa madai ya mkandarasi katika Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi); taarifa ya CAG imebainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Fungu – 98 (Sekta ya Ujenzi) ilikuwa inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 31.38 sawa na dola za Kimarekani milioni 13.7 kutoka kwa mkandarasi aliyetekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Ilbanda - Uyole. Madai haya ni ya tangu mwaka 1991 (miaka 17 iliyopita).

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati ni kuwa kutolipwa kwa deni hili kunasababisha Serikali kutozwa riba ya shilingi bilioni 2.19 kila mwaka; fedha hizi zingeweza kuelekezwa maeneo mengine yenye tija.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na mbili; uwiano wa utoshelevu wa mtaji (*capital adequacy ratio*) kuwa chini ya kiwango kinachohitajika kisheria katika Benki ya *TIB* Maendeleo; kwa mujibu wa Kanuni namba 19(2) ya Utoshelevu wa Mtaji wa Benki Kuu ya mwaka 2011, Benki ya Maendeleo (*TIB*) inatakiwa kuwa na uwiano wa mtaji wa msingi (*core capital*) na mtaji wa jumla (*total capital*) kwa asilimia 13 na 15 mtawalia.

Mheshimiwa Spika, hadi kufika tarehe 31 Desemba, 2020, Benki ilikuwa na mtaji wa msingi (*core capital*) na jumla ya mtaji (*total capital*) uliofikia kiasi cha shilingi bilioni 38.358 wakati kima cha chini kinachohitajika kwa taasisi ya fedha za maendeleo ni kiasi cha shilingi bilioni 50.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo *TIB* Maendeleo imekiuka Sheria ya Benki Kuu katika suala la utoshelevu wa mtaji na pia haitimizi ipasavyo majukumu ya kugharamia shughuli za maendeleo.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na tatu; madeni ambayo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) linadai kwa *TANESCO, SONGAS*, Ndovu na *PAET*, shilingi bilioni 429; hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*) lilikuwa linadai taasisi mbalimbali ikiwemo *TANESCO, SONGAS*, Ndovu na *PAET* jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 429. Hali hii inaathiri shughuli ya *TPDC* katika kusambaza gesi majumbani na viwandani.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na nne; masuala ya ujumla katika kaguzi za hesabu za Sekretarieti za Mikoa (*Regional Secretariats*); kaguzi za Sekretarieti za Mikoa zimebaini changamoto kadhaa ikiwemo usimamizi duni wa mikataba na dosari katika uandaaji wa taarifa za fedha katika Mfumo wa *IPSAS*. Dosari hizi zimesababisha hesabu za Sekretarieti nyingi za Mikoa kufanyiwa marekebisho (*adjustments*) za mara kwa mara ili kufikia matakwa ya *IPSAS*.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na tano; kusimama kwa mradi wa ujenzi wa vihenge unaoteklezwa na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (*NFRA*) na deni la Serikali la shilingi bilioni 166.4; taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2020 ilibainisha kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipokea mkopo wa dola za Kimarekani milioni 55 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Poland kwa ajili ya ujenzi wa vihenge na maghala ya kuhifadhi nafaka kupitia mkataba uliosainiwa na pande hizo mbili tarehe 28 Septemba, 2015. Hata hivyo, mradi katika eneo la Dodoma umesimama tangu Desemba 01, 2020.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili katika *NFRA* ni uwepo wa deni la kiasi cha shilingi bilioni 166.4 ambayo *NFRA* wanadai Serikali, hivyo kuathiri shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na sita, ukaguzi wa Bohari ya Madawa Tanzania (*MSD*); katika *MSD* Kamati ina hoja nne ambazo ni pamoja na deni ambalo Serikali inadaiwa na *MSD*, kiasi cha shilingi bilioni 281. Hoja ya pili ni changamoto ya utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika uagizaji wa dawa na vifaa tiba ambapo *MSD* inatumia mlolongo mrefu kuagiza dawa.

Mheshimiwa Spika, hoja namba tatu, kodi kwa malighafi zinazotumika kutengeneza dawa na uwepo wa kodi kwa baadhi ya vifaa tiba vinavyohusika kutolea huduma muhimu kama kusafisha damu; na hoja namba nne ni utegemezi wa manunuzi ya dawa.

Mheshimiwa Spika, hoja namba kumi na saba; kutokuwepo na maelezo ya kutosha katika hesabu za Fungu 56 – TAMISEMI kuhusu fedha kiasi cha shilingi bilioni 2.1; Kamati ilibaini kiasi cha shilingi bilioni 2.1 ambacho ni *cash and cash equivalents* ambacho hakikujumlishwa katika *cash flow statement* ya mwaka wa fedha 2018/2019. Suala hili linakwenda kinyume na masharti ya uandaaji hesabu katika Mfumo wa *IPSAS*.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo; kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufanisi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*); Serikali iboreshe shughuli za vyombo vinavyohusika na kushughulikia rufaa za kodi (*TRAT* na *TRAB*) kwa kuvipa rasilimali za kutosha kwa maana ya fedha na watu ili vitekeleze majukumu yake kwa ufanisi na kumaliza mashauri ya kodi kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hasara iliyotokana na manunuzi na usimikaji wa Mfumo wa *ERP* katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*); Serikali ichukue hatua za kisheria kwa kampuni zote ambazo zimehusika kuisababishia *TPA* hasara kama zilivyobainishwa kwa kina katika taarifa ya ukaguzi maalumu wa kiuchunguzi wa mfumo wa *ERP* uliofanywa na *CAG*. Aidha, hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe kwa watumishi wote wa *TPA* waliohusika na hoja

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za mifumo kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi wa ukaguzi maalum wa *CAG*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania; Serikali ikamilishe mchakato wa majadiliano kuhusu madeni ya *ATCL* na mapitio ya kina ya mikataba iliyopo kati ya *ATCL* na *TGFA* ili kuhakikisha dosari zinazosababisha hasara kwa *ATCL* zinaondolewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*); Serikali ichambue kwa kina na kuhakiki madeni yote ambayo *TANESCO* inadaishi ikiwa ni pamoja na deni la *capacity charge* ya *SONGAS* kiasi cha shilingi bilioni 493.5 ili kuangalia uwezekano wa kubadilisha madeni hayo kuwa mtaji (*equity*) hali itakayosaidia kusafisha mizania ya vitabu vya hesabu za *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya mtaji na ongezeko la mikopo chechefu (*NPL*) katika Benki ya Biashara Tanzania (*TCB*) baada ya kuunganishwa na Benki ya *TIB* Biashara; Serikali ikamilishe ahadi yake ya kuongeza mtaji wa *TCB* kuititia utoaji wa hati fungani isiyo taslimu (*non-cash bond*) ya shilingi bilioni 130 kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2022. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu taarifa ya ukaguzi wa ufanisi wa utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari Mbigiri; Serikali itekeleze kwa ukamilifu mapendekezo yote kumi na mbili yaliyotolewa na *CAG* katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi ili kuhakikisha malengo ya mradi yanafikiwa ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mifuko ya Hifadhi za Jamii; Serikali iendelee na hatua za kulipa madeni husika kwa kutumia njia mbalimbali kama ilivyoanza katika Mfuko wa *PSSSF*. Hatua hizi za Serikali ziendelee katika Mifuko ya *NSSF* na *NHIF*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Madini; Serikali kuititia Tume ya Madini iwasilishe nyaraka husika kwa *CAG*

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa uhakiki. Aidha, Serikali iboreshe mfumo wa udhibiti na usimamizi wa shughuli za usafirishaji wa madini ili kuhakikisha mapato stahiki ya Serikali yanakusanywa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*); Serikali ikamilishe majadiliano na mkandarasi na taratibu za manunuvi ili kuwezesha kusainiwa kwa mkataba na upatikanaji wa kadi ghafi zipatazo 13,735,728 kwa kuzingatia idhini iliyotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kuongeza muda wa mkataba na mkandarasi, tarehe 29 Mei, 2021. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mtaji usiotosheleza wa Benki ya *TIB* Maendeleo; Wizara ya Fedha na Mipango ichambue na kuangalia uwezekano wa kuongeza mtaji katika *TIB* Maendeleo ili kuiwezesha benki kulipa amana zillizolva kwa taasisi zillizowekeza na pia kukidhi matakwa ya Kanuni namba 19(2) ya Utoshelevu wa Mtaji wa Benki Kuu ya mwaka 2011. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu riba ya shilingi bilioni mbili kila mwaka kutokana na kutolipwa kwa madeni ya wakandarasi katika Fungu 98 – Sekta ya Ujenzi; Serikali ihakiki na kulipa deni husika ili kuepuka riba inayotozwa kila mwaka ambayo ni hasara kwa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa vihenge katika *NFRA* na deni la Serikali la shilingi bilioni 166.4; Serikali ichukue hatua stahiki ili kukamilisha mradi wa ujenzi wa vihenge uliosimama tangu mwaka 2020 ili thamani halisi ya fedha za umma ipatikane. Aidha, Serikali ifanye tathmini na kuptitia upya masharti ya makubaliano ya mkopo uliochukuliwa kutoka nchini Poland kwa ajili ya ujenzi wa vihenge ili kuondoa masharti hasi yaliyopo katika mkopo huo. Aidha, Serikali itafute utaratibu wa kulipa deni inalodaiwa na *NFRA* la shilingi bilioni 166.4. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwajibikaji katika mabonde ya maji; Bunge linaishauri Serikali kukamilisha muundo wa bodi zote za maji hapa nchini na kuhakikisha

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kunakuwepo watumishi wa kutosha wenye taaluma za uhasibu ili kuhakikisha uwajibikaji katika fedha za umma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni *TPDC* inayodai kwa *TANESCO*, *SONGAS*, *PAET* na Ndovu, shilingi bilioni 429; Serikali ifanye mapitio ya madeni ambayo *TPDC* inadai kwa taasisi mbalimbali ikiwepo *TANESCO*, *SONGAS*, *PAET* na Ndovu ili kuangalia utaratibu bora wa kuondoa madeni hayo. Aidha, *TPDC* iongezewe uwezo wa kirasilimali ili kutekeleza miradi ya gesi ambayo ni muhimu kwa uchumi na mazingira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya ujumla katika kaguzi za hesabu za Sekretarieti za Mikoa; Sekretarieti za mikoa ziwezeshwe kuwa na watumishi wa kutosha na wenye sifa katika maeneo ya manunuzi, uhasibu na sheria. Hii itasaidia kuongeza hali ya uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria katika masuala ya fedha, manunuzi na mikataba katika sekretarieti za mikoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bohari ya Madawa Tanzania (*MSD*); Serikali ikamilishe ulipaji wa deni ambalo inadaiwa na *MSD* na kuhakikisha inatoa fedha kwa Bohari kwa kuzingatia bajeti iliyopitishwa na Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu – 56, Ofisi ya Rais – *TAMISEMI*; Bunge linaazimia kwamba *CAG*afanye uhakiki wa kina wa hesabu za Fungu 56 – *TAMISEMI* ili kubaini hali halisi ya hoja husika na kuliarifu Bunge ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, shukrani; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini wa Bunge letu. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabitii kwa Kamati. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wangu, Mheshimiwa Japhet Hasunga, kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Naomba majina yote ya Wanakamati yaingie kwenye *Hansard*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi, kwa ushauri wake kwa Kamati. Natoa shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kuititia kwa Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto; Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Mswige Dickson Bisile; Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Sostenes Maseke na Ndugu Amina Salum Namtema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho japo sio kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (*NAOT*) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) Ndugu Charles Kichere. (*Makof*)

Aidha, naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kuititia kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, Msajili wa Hazina, Kamishina wa Bajeti na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliota katika kuratibu shughuli za Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja; nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja sasa kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kukubali mapendekezo ya Kamati ya *PAC* yaliyopo katika taarifa hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**TAARIFA YA MWAKA YA KAMATI KUHUSU TAARIFA ZA
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA
HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SERIKALI KUU NA MASHIRIKA YA
UMMA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI,
2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za
Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020)*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

1.1 Utangulizi

Mheshimiwa Spika, Awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujalia zawadi ya uhai hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa leo hii. Aidha, ninakupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mwenyezi Mungu akupe afya njema katika kutekeleza majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu shughuli zilizotekelawa kwa mwaka 2021 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kujadili inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka 2021, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) liipokea na kujadili Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Taarifa husika za ukaguzi ziliwasilishwa hapa Bungeni tarehe 08 Aprili, 2021. Kwa msingi huo, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika Taarifa hizo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

1.2 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Majukumu hayo ni: -

- a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
- b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na
- c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa wizara za Serikali na mashirika ya umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

1.3 Miongozo Iliyotumika na Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu yake

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya rejea ya kina katika nyaraka zifuatazo: -

- a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;
- b) Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2019/20);
- c) Taarifa za kaguzi mahsus (*Individual audit report*) za mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma;

- d) Barua za mapungufu ya ukaguzi (*Management letter*) za mafungu mahususi;
- e) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008;
- f) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, 2001;
- g) Sheria ya Bajeti namba 11 ya Mwaka 2015;
- h) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370;
- i) Sheria ya Manunuzi ya Umma Sura 410;
- j) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286;
- k) Sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura 296; na
- l) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia mbinu zifuatazo: -

- a) Kupokea, kuchambua na kujadili maelezo mafupi “briefs” za CAG kuhusu hoja za ukaguzi za mafungu husika;
- b) Mahojiano na Maafisa Masuuli kuhusu hoja za ukaguzi;
- c) Uchambuzi wa kina wa taarifa za ukaguzi za mafungu mahususi;
- d) Ziara za ukaguzi wa ufanisi katika miradi ya maendeleo;
- e) Semina kuhusu Majukumu ya Kamati;
- f) Kupokea maoni ya wadau hasa wakati wa uchambuzi wa Muswada; na
- g) Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma.

1.4 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati


Mheshimiwa Spika, Shughuli za Kamati kwa mwaka 2021, zililenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya CAG kwa Mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2020. Aidha, shughuli hizo zilikusudia kufuatilia utekelezaji wa maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa nyakati tofauti kwa kipindi chote cha mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2020 CAG alifanya ukaguzi wa jumla ya Taasisi¹ mia mbili sitini na tatu (263) za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara na Idara zinazojitegemea sitini na sita (66), Wakala thelathini na nne (34), Mifuko maalum kumi na nne (14), Sekretarieti za Mikoa ishirini na sita (26), Taasisi nydingine hamsini na tatu (53), Vyama vya Siasa kumi na tisa (19) na Bodi za Mabonde ya Maji kumi na tano (15).

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi ulihuisha pia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa (*Consolidated accounts*), ukaguzi wa malipo tarajali ya pensheni, hospitali za rufaa thelathini na mbili (32) na kaguzi maalumu kumi na nne (14). Kaguzi za Balozi hazikufanyika katika mwaka unaotolewa taarifa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa uviko 19.

Mheshimiwa Spika, Mchanganuo wa Taasisi za Serikali kuu zilizokaguliwa na CAG na kujumuishwa katika taarifa ya mwaka 2020 ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 1.1 hapa chini: -

Chati Na. 1.1 Mchanganuo wa Taasisi za Serikali Kuu zilizokaguliwa mwaka 2020.



Chanzo: *Taarifa ya CAG kwa ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.*

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Mashirika ya Umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikaguwa na kutoa Taarifa ya jumla ya Mashirika ya Umma mia moja sitini na tano (165) ikilinganishwa na Mashirika ya Umma mia moja ishirini na mbili (122) yaliyokaguliwa kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mafungu ya Serikali Kuu na ya Mashirika ya Umma kwa kuzingatia vipaumbele iliyojiweke. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo ikiwamo ya umeme vijiji (REA) inayotekelawa katika Mikoa ya Singida, Iringa na Manyara. Miradi mingine iliyojtembelewa ni ya maji katika Mkoa wa Morogoro na barabara katika Mkoa wa Morogoro chini ya Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA).

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya pekee na kwa maelekezo yako, mapema mwezi Agosti, 2021, Kamati ilishughulikia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286 (*The Accountants and Auditors Registration, Amendments Act, 2021*), ambao ulikamilika katika hatua zake zote². Shughuli hii ilikuwa muhimu kwa Kamati kwani ilitoa fursa adhimu kwa Waheshimiwa Wajumbe kuongeza uzoefu katika eneo la uchambuzi wa Miswada ya Sheria ukizingatia majukumu yao ya kila mara ambayo hulenga zaidi uchambuzi wa taarifa za hesabu katika ngazi ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na shughuli hizo, Kamati ilitekeleza jukumu lingine ulilotuagiza ambapo ilizhoji Bodi na Menejimenti za Taasisi kumi na moja za umma (11) ambazo zilikuwa hazijakamilisha kufunga hesabu zake kwa wakati kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Taasisi hizo hazikuwa zimekamilisha hesabu zake hadi muda ambao CAG alikuwa anakamilisha ukaguzi wa mwaka 2019/2020 na kuwasilisha taarifa yake jumuifu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mwisho, Kamati ilichambua Taarifa moja (1) ya Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance audit report*) inayohusu uzalishaji na uendeshaji wa shamba la miwa na Kiwanda cha Sukari Mbigiri, Dakawa Morogoro yaani (*The performance audit report on the implementation of Mbigiri sugar production project*).

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kina wa hoja zilizofanyiwa kazi na Kamati unapatikana katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

SEHEMU YA PILI

- 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI**
- 2.1 Maeleo ya Jumla Kuhusu Uchambuzi**

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijielekeza katika kubainisha thamani ya pesa iliyotumika katika matumizi yaliyoripotiwa

na kukaguliwa (*Value for money criteria*), uzingatiaji wa bajeti, kiasi cha matumizi ikilinganishwa na mahitaji halisi na matokeo ya taarifa za kaguzi maalum zilizofanya hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na vigezo hivyo, Kamati ilijielekeza kwa kuangalia hali ya kujirudia rudia kwa hoja za ukaguzi katika taasisi husika, uzingatiaji wa mamlaka halali za kuidhinisha matumizi ya fedha, uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma na kuwepo kwa kumbukumbu na nyaraka zinazopaswa kutunzwa kwa ushahidi wa matumizi kama zilivyohitajiwa na CAG.

2.2 Uchambuzi

Mheshimiwa Spika, Kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ullibainisha mambo yafuatayo: -

2.2.1 Matokeo ya Ukaguzi Maalumu wa Kiuchunguzi Kuhusu Ununuzi na Usimikaji wa Mfumo wa ERP Katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi kirefu katika taarifa zake za ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), CAG amekuwa akibainisha namna mapungufu ya mifumo ya uendeshaji na usimamizi (*Operational systems³*) wa shughuli za TPA yanavyochangia upotevu wa mapato ya Serikali. Mifumo ya kielektroniki ni mojawapo ya nyenzo muhimu ya kurahisisha utekelezaji wa shughuli za TPA kama vile utunzaji wa taarifa sahihi na kwa wakati za hesabu, watumishi na mali.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na taarifa za CAG kubainisha dosari hizo za kimfumo katika TPA, Bunge lako Tukufu kwa nyakati tofauti kwa takribani miaka mitano (5) kati ya mwaka 2016 hadi 2020 limekuwa likibainisha umuhimu wa TPA kurekebisha dosari za mifumo ili kuongeza mapato ya Serikali. Hali kadhalika, TPA imekuwa ikitumia fedha nyingi kuwalipa wakandarasi wa mifumo bila ya kupata thamani halisi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua jitihada ambazo Serikali na TPA imeanza kuchukua kwa sasa katika kurekebisha dosari za mifumo na kuchukua hatua kwa watumishi kumi na tano (15) waliohusika kwa nyakati tofauti na changamoto za kimfumo. CAG aliifahamisha Kamati kuwa Kamati huru imeundwa na TPA kushughulikia masuala ya kinidhamu kwa wahusika ikiwa na wajumbe kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, TEMESA, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Viwanda na Biashara, Tume ya Utumishi wa Waalimu, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na PPRA ambapo Kamati hii ilianza kazi rasmi mnamo tarehe 20 Januari 2022⁴.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, pamoja na hatua hizo za TPA ambazo zinategemea kukamilika ifikapo tarehe 01 Machi, 2022, Kamati ingependa kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, CAG alfanya ukaguzi maalumu wa kiuchunguzi ili kubaini dosari za usimikaji wa mifumo mbalimbali katika TPA. CAG aliwasilisha kwa Katibu wa Bunge matokeo ya ukaguzi huo mnamo tarehe 17 Agosti, 2021 kuititia barua yenyewe Kumb. Na. CEB.35/238/01B/55.

Mheshimiwa Spika, Katika kuchambua matokeo ya ukaguzi maalumu wa kiuchunguzi, Kamati ilibaini kuwa hoja hii ilianza katika ukaguzi wa hesabu za TPA kwa mwaka 2009/2010 na imeendelea hadi katika ukaguzi huu maalumu wa kiuchunguzi wa mwaka 2019/2020. Hivyo basi ni muhimu Bunge lako Tukufu likafahamu kwa kina matokeo ya ukaguzi huu maalumu wa kiuchunguzi uliohusisha kipindi cha miaka kumi (10), yaani kati ya mwaka 2009/2010 hadi 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya ukaguzi huu maalumu wa kiuchunguzi ni muhimu kwa sababu TPA hadi sasa inakabiliwa na changamoto za ununuzi na usimikaji wa mifumo wakati fedha nyingi za Serikali zimetumika katika eneo hilo. Aidha, taarifa hii inatoa fursa muhimu na adhimu kwa Serikali kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na CAG na maazimio yatakayotolewa na Bunge lako Tukufu ili kuboresha mifumo husika na hatua za kiuwajibikaji zinazotakiwa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa matokeo ya ukaguzi maalumu wa kiuchunguzi katika mchakato mzima wa ununuzi na usimikaji wa mfumo ujulikanao kwa jina *Enterprises Resource Planning* (ERP). Mfumo wa ERP ulitakiwa kutekelezwa katika awamu nne (4).

Mheshimiwa Spika, Kwa awamu ya kwanza, taarifa ya CAG imebainisha kuwa mnamo tarehe 14 Julai, 2010, TPA waliipa zabuni kampuni ya *Soft Tech Consultant Limited* (STCL) ili kutekeleza mkataba wa usimikaji mfumo jumuishi (*Intergreated system*). Malengo ya usimikaji wa mfumo ilikuwa kusaidia katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Shirika kama masuala ya usimamizi wa bajeti, usimamizi wa taarifa za uagizaji na uondoshaji wa shehena za mizigo na usimamizi wa kanzi data na masuala ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Katika awamu ya kwanza, mfumo huo uliana kutumika rasmi mwezi Julai 2011. Hata hivyo, kuitia taarifa ya CAG Kamati imebaini kwamba mfumo uliana kutumika bila ya kufanyiwa majoribio ya mfumo mzima (*Full operational acceptance test*) ili kubaini ukamilifu na uhimilivu wa mfumo huo. Jambo hili lilikuwa kinyume na matakwa ya kipengele Na. 27 cha masharti ya jumla ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na dosari hiyo, baada ya kuanza kutumika kwa mfumo mapungufu mbalimbali yalijitokeza ikiwa ni pamoja na mfumo kukosa udhibiti wa bajeti (*Missing capital budget*), kutowezesha utunzaji sahihi wa taarifa za huduma za uagizaji na utoaji wa shehena za mizigo (*Clearing and forwarding*), kutohifadhi ipasavyo kwa taarifa za kihasibu (*Cost accounting*) na mengineyo yalibainika. Dosari hizi zinathhibitisha hoja ya ukaguzi kuwa TPA walitoa zabuni kwa mzabuni ambaye hakuwa na sifa.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 18 Juni, 2014 TPA na STCL walikubaliana kuvunja mkataba husika kutokana na dosari za kiutekelezaji zilizofafanuliwa hapo awali. Hata hivyo, hapakufanyika makubaliano yejote ya mwisho ya kufunga mkataba huo. Aidha, tathmini ya kazi iliyotekelze wa haikufanyika ukilinganisha na madai na malipo kwa mzabuni.

Hadi mkataba unavunjwa tarehe 18 Juni, 2014 TPA ilikuwa imeishailipa STCL **Sh. 600,433,960** sawa na **asilimia 87** ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya pili (2) ya utekelezaji wa mfumo wa ERP ilikuwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo ilitengwa kiasi cha **Sh. 6,600,000,000** kwa ajili ya ununuzi, mafunzo na usimikaji wa mfumo. Hata hivyo, mkataba wa usimikaji wa mfumo haukusainiwa baada ya zabuni husika kufutwa.

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa ununuzi wa zabuni hii ulifutwa kwa sababu kampuni ya KPMG iliyoshinda zabuni ilikuwa na mgongano wa kimaslahi kwa sababu ilishiriki kuandaa nyaraka za zabuni na kisha ikashiriki katika mchakato wa zabuni husika.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya tatu (3) ya utekelezaji wa mradi wa ERP ilikuwa mwaka 2015/2016. TPA ilitenga tena kiasi cha **Sh.6, 100,100,000** kwaajili ya ununuzi, usanifu, mafunzo, upimaji na kukabidhi mfumo wa TEHAMA uitwao SAP – ERP.

Mheshimiwa Spika, Katika awamu hii kampuni ijulikanayo kwa jina la *Twenty Third Century Systems PVT limited* (TTCS) ya Kenilworth Garden, 1 Kenilworth Road, Newlands, CY 1938, Causeway, Harare Zimbabwe ilipewa tozo ya zabuni kwa mkataba Na. AE/016/2014-15/CTB/G/39 wa thamani ya **Dola za Kimarekani 6,635,387.16** sawa na **Sh. 14,161,575,046** kiasi ambacho kinajumusisha **15%** ya kodi ya zuio.

Mheshimiwa Spika, Mkataba huu ulisainiwa tarehe 30 Oktoba, 2015 na ulipaswa kukamilika katika kipindi cha miezi tisa (9) kuanzia tarehe 22 Disemba, 2015 hadi tarehe 22 Septemba, 2016 ukifuaatiwa na kipindi cha miaka mitatu (3) cha muda wa uangalizi.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya TTCS haikuweza kukamilisha kazi kwa wakati na kwa mujibu wa mkataba. Kutohana na mapungufu ya kiutekelezaji, mnamo tarehe 21 Machi, 2019 TPA ilivunja mkataba na TTCS. Wakati mkataba unavunjwa

TPA ilikuwa imekwishailipa kampuni ya TTCS kiasi cha **Dola za Kimarekani 4,632,099.01 (Sh. 9,983,541,692.91)** sawa na **asilimia 70** ya thamani ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, Awamu ya nne (4) ya utekelezaji wa mradi wa ERP ilianza mnamo tarehe 20 Septemba, 2019 ambapo TPA waliingia mkataba wa thamani ya **Dola za Kimarekani 433,011** na kampuni ya SAP East Africa Limited. Kampuni hii ilikuwa ni mwakilishi wa kampuni ya SAP SE ya Ujerumani, kampuni inayotengeneza mfumo wa ERP. Lengo la mkataba huu ilikuwa ni kuwezesha kuititia na kuhakiki ubora wa kazi iliyotekelze wa na TTCS. Uhakiki wa kazi ulibaini kuwa TTCS ilijenga **module 7** tu kati ya **module 26** ilizotakiwa kutengeneza kwa mujibu wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo ya kina yenye kufafanua mtiririko wa matukio ya utekelezaji wa mradi wa ERP, ukaguzi wa kiuchunguzi umebainisha dosari mahsusizi zifuatazo katika mchakato mzima hali iliyosababisha hasara kwa Serikali: -

- a) TPA haikufuata mwongozo wa kuishirikisha Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) katika maandalizi ya utekelezaji wa mifumo. Jambo hili ni kinyume na matakwa ya Kifungu 4.2.1 cha mwongozo wa matumizi bora, sahihi na salama wa vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano Serikalini (TEHAMA), Toleo la Julai, 2012;
- b) Hali kadhalika, ukaguzi ulibaini TPA ilikuwa imesimika mifumo zaidi ya kumi (10) ambayo haikuwa inasomana (*Intergrated*) hivyo kutokuwa na tija na ufanisi kwa Shirika;
- c) TPA ilitoa tuzo ya mkataba wa kusimika mfumo wa ERP kwa awamu ya kwanza kwa Kampuni ya *Soft Tech Consultant Ltd* (STCL) kwa gharama ya **Sh. 694,142,960** ambayo haikuwa na sifa na uwezo stahili. STCL ililipwa kiasi cha **Sh. 600,433,963** sawa na **asilimia 87** ya mkataba pamoja na mkataba husika kusitishwa hivyo TPA ilipata hasara ya **Sh. 600,433,963**;

- d) TPA iliingia mkataba wa nyongeza na STCL wa **Dola za Kimarekani 31,860** kwa ajili ya mafunzo ya watumishi 165 licha ya mkataba wa awali kuhusisha mafunzo ya aina ileile;
- e) Kiasi cha **Sh. 12,177,480** kililipwa zaidi isivyostahili kutokana na kubadilishwa sifa za vifaa vilivyopangwa kufungwa kwenye mradi;
- f)Ukaguzi ulibaini pia, Kampuni ya *Twenty Third Century Systems* (TTCS) ilipewa tuzo ya mkataba Na. AE/016/2014-15/ CTB/G/39 wa **Dola za Kimarekani 6,635,387.16** kwa upendeleo kwa kuwa haikuwa na sifa stahiki. Mkataba huu pia ulivunjwa wakati TPA akiwa amelipa kiasi cha **Dola za Kimarekani 4,632,099** sawa na asilimia 70 ya thamani ya mkataba wakati utekelezaji ukiwa kwa asilimia 42;
- g) Kiasi cha **Dola za Kimarekani 410,817.37** cha kodi ya zulo hakikuwasilishwa TRA kwa mujibu wa sheria wakati wa utekelezaji wa mkataba wa TPA na TTCS;
- h) TPA ilitozwa Ada ya Mwaka ya Leseni kiasi cha **Dola za Kimarekani 404,029.03** katika mkataba wake na TTCS. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kuwa Ada halisi iliyopaswa kulipwa ni **Dola za Kimarekani 190,643.70**;
- i) TPA ilipata hasara ya kiasi cha **Dola za Kimarekani 433,011** kwa kuingia mkataba wa ziada na Kampuni ya SAP – East Africa Ltd ili kuhakiki kazi zilizotekerezwa kwenye mkataba uliovunjwa wa Kampuni ya TTCS. Fedha hizo zingeokolewa endapo mkataba wa TTCS ungetekerezwa ipasavyo;
- j) Ukaguzi ulibaini udanganyifu katika upukuzi wa mikataba hali iliyosababisha masharti mapya kujumuishwa kwenye mikataba wakati hayakuwa sehemu ya nyaraka ya zabuni; na
- k) Mwisho ukaguzi ulibaini kuwa mikataba miwili (2) kati ya TPA na SAP – East Africa Ltd yenye thamani ya **Dola za Kimarekani 433,011** na **Dola za Kimarekani 997,647** mtawalia, haikuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya upekuzi. Suala hili ni kinyume masharti ya Kanuni ya 59(2)(1)(b) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, Ufanuzi wa ziada na mchanganuo wa kiasi cha hasara ambayo TPA imepata kutokana na dosari za utekelezaji wa mkataba wa ERP umefafanuliwa kwa kina katika jedwali Na. 2.1 hapa chini.

Jedwali Na. 2.1: Hasara iliyopatikana kutokana na mradi wa ERP

Mzabuni	Kiasi cha Mkataba	Maelezo ya Hasara	Kiasi cha Hasara	
			Dola za Kimarekani	TZS
STCL	Sh. 694,142,960	Mfumo ulisiomikwa haukukamilishwa na hautumiki	-	600,433,960
STCL	Dola za Kimarekani 31,860	Nyongeza ya mkataba wa mafunzo ambayo yalipaswa kulipiwa kwenye mkataba mama	-	55,149,660
Ndg. Ramadhani Mwikalo	0	Malipo yaliyofanywa zaidi ya yale yaliyostahili	15,920.00	-
TTCS	Dola za Kimarekani 6,635,378.16	Kodi ya zuij ambayo haikuakutwa (USD 398,123.23) na (USD 12,694.14) ili katwa lakini haikuwasilishwa (Jumla USD 410,817.37)		877,229,116.93
		Ada ya Mwaka ya Leseni kubwa Kuliko Thamani Haikuakutwa (USD 1,000,000.00) na mzabuni alllipwa zaidi ya alichostahili.		862,298,957.26
	Chanzo mkataba wa ERP	Tarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa kiuchunguzi wa na mzabuni alllipwa zaidi ya alichostahili.	2027/08.40	79
SAP Africa Limited	East	Dola za Kimarekani 433,011.4	Gharama ya kuhakiki ubora wa mradi kutokana na TTCS kushindwa kutekeleza	433,011.4 841,802,190.38

Mheshimiwa Spika, Kama jedwali Na. 2.1 linavyofafanua hapo juu, mapungufu katika utekelezaji wa mkataba wa ERP katika awamu zote nne (4) umesababisha hasara ya moja kwa moja kwa Serikali kwa takribani kiasi cha **Sh. 3,236,913,884.57** na **Dola za Kimarekani 2,306,839.8.**

Mheshimiwa Spika, Hivyo basi ukijumlisha na ghamama zote za mkataba husika, TPA ilitumia jumla ya **Sh. 17,825,043,623,000** katika kununua na kusimika mfumo wa ERP ambao haukukamilika na haukutoa thamani halisi ya fedha (*Value for money*) katika matumizi ya fedha za umma.

2.2.2 Hali ya Mtaji Katika Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na Changamoto za Kimkataba katи ya ATCL na TGFA

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2020 ulibaini kuwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ilikuwa na mtaji hasi (*Negative working capital*)⁵ kiasi cha **Sh. 246,665,705,000**. Pamoja na changamoto za mtaji, ATCL imekuwa na ongezeko la deni (*Liabilities with related parties*) kiasi cha **Sh.152, 165,868,000** ambapo deni hilo linahusisha kiasi cha **Sh. 70,940,850,905** (asilimia 47 ya deni lote), deni ambalo ATCL wanadaiwa na TGFA.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina katika hesabu zilizokaguliwa za ATCL na kubaini kuwa ATCL ilipata hasara ya kiasi cha **Sh. 60,246,925,000** kwa mwaka wa fedha 2019 /2020 hivyo kufanya hasara jumuifu tangu mwaka 2015/2016 (*Accumulated losses*) kufikia kiasi cha **Sh. 152,960,200,731**.

Mheshimiwa Spika, Uwepo wa madeni ya muda mrefu ni kihatarishi cha uendelevu wa kampuni kwa siku zijazo. Kwa msingi huo, kihatarishi hicho kimesisitizwa kwa kina katika hati ya ukaguzi iliyotolewa na CAG katika hesabu za ATCL kwa mwaka wa fedha 2019/2020. CAG alitoa hati safi ya ukaguzi yenye masuala ya msisitizo (*Unqualified audit opinion with emphasis of matter*). Suala la msisitizo katika hati hiyo ya ukaguzi ni hoja ya mtaji na madeni ya ATCL hali ambayo

inaweza kusababisha kampuni kushindwa kuijendesha kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya CAG katika msisitizo wa hati ya ukaguzi ni kama yanavyonukuliwa hapa chini: -

Nukuu:

...These conditions indicate the existence of material uncertainty that may cast significant doubt on the company's ability to continue as a going concern⁶...

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, Kutohana na changamoto za mtaji na madeni na kwa kuzingatia uchambuzi wa kina wa taarifa ya CAG na mahojiano na uongozi wa ATCL na TGFA yaliyofanyika Bungeni Dodoma mnamo tarehe 16 Februari, 2022, Kamati ilibainisha hoja nyingine ambazo zinachangia ATCL kutokuwa na ufanisi wa kutosha kifedha hadi sasa;

a) Uwepo wa madeni makubwa ya siku za nyuma ambayo hayajalipwa. ATCL inadaiwa kiasi cha **Sh. 152,960,200,731**. Deni hili linajumuisha deni inalodaiwa na TGFA kiasi cha **Sh. 70,940,850,905** (Asilimia 47 ya deni lote). Aidha, kuna deni la kiasi cha **Sh. 87,253,607,184** (Asilimia 59 ya deni lote) ambalo ni deni la Kampuni ya Wallis Trading Inc. iliyokuwa imeikodishia ATCL Ndege miaka ya nyuma;

b) Kutofikiwa kwa malengo ya kifedha ya kampuni kwa kiwango cha **asilimia 76**. Kwa mwaka 2019/2020, ATCL ilipanga kupata mapato kiasi cha **Sh. 661,647,900,000**. Hata hivyo, walifanikiwa kupata mapato kiasi cha **Sh. 157,602,265,776** hivyo kuathiri ufanisi wa kampuni;

c) Changamoto za kimkataba kati ya ATCL na TGFA (*Aircraft lease contracts*). Kamati imebaini uwepo wa vifungu kadhaa vyta Kimkataba ambavyo vinasababisha ATCL kuongeza deni. Mathalani, uchambuzi wa Kamati ulibaini mapungufu mahsusni katika mikataba ya ATCL na TGFA kama ifuatavyo: -

i. ATCL iliingia gharama za ukodishaji wa ndege kiasi cha **Sh. 15,464,914,743** kutohana na mkataba kati yake na TGFA

kutokuwa na kipengele cha “Force Majeure”⁷ (Vihatarishi visivyotabirika). Gharama hii ilitokana na ukodishaji wa ndege ambazo hazikufanya kazi wakati wa kipindi cha janga la uviko - 19 kati ya tarehe 15 Machi na tarehe 30 Juni, 2020. Endapo kipengele hicho kingekuwepo kwenye mkataba, ATCL wasingetozwa gharama hizo; na

ii. ATCL iliingia gharama mara mbili (2) kiasi cha Sh. **16,977,343,704** kama gharama za matengenezo ya ndege kutokana na dosari za kimkataba katи yake na TGFA.

Mheshimiwa Spika, Masuala hayo matatu (3) kwa kiasi kikubwa ndio yaliyochangia kutofikiwa malengo na ufanisi wa ATCL kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kamati imefahamishwa kuwa Serikali inaendelea na mchakato wa kuchukua hatua ya kushughulikia masuala hayo. Hii inatokana na maelezo yaliyowasilishwa mbele ya Kamati, hivyo ni muhimu mchakato huo ukakamilika mapema ndani ya mwaka huu wa fedha ili ATCL iweze kuijendesha kibiashara na kwa ufanisi.⁸


2.2.3 Tathmini ya Ufanisi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Katika Kufikia Malengo ya Ukusanyaji wa Kodi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2020. Taarifa ya ukaguzi wa makusanyo ya fedha kwa upande wa Tanzania Bara imebainisha kiasi halisi kilichokusanywa kilikuwa Sh.17,649,024,427,539 ukilinganisha na makadirio ya kiasi cha Sh. 19,100,933,314,570. Kwa msingi huo, kulikuwa na nakisi ya makusanyo ya kiasi cha (**Sh.1,451,908,887,031**) ambayo ni sawa **asilimia 7.6%** ya makadirio ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Tanzania Zanzibar makusanyo halisi yaliyofanywa na TRA yalikuwa kiasi cha Sh. **281,852,372,440** ukilinganisha na makadirio ya kiasi cha Sh. **350,191,592,000**, hivyo kuwepo na nakisi ya makusanyo ya kiasi cha (**Sh. 68,339,219,560**) sawa na **(19.5%)** ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa makusanyo ya kodi katika TRA kwa kipindi cha mwaka 2017 hadi mwaka 2020 kwa upande wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar mtawalia umefafanuliwa katika chati Na. 2.1 na 2.2 hapa chini: -


Chati Na. 2.1: Mwenendo wa makusanyo ya kodi kwa Tanzania Bara 2017/2018 hadi 2019/2020.



Chanzo: *Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa TRA kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.*'

Mheshimiwa Spika, Kama ufanuzi wa kwenye chati Na. 2.1 hapo juu unavyobainisha, kwa takribani kipindi cha miaka mitatu (3) ya fedha mtawalia, yaani kati ya 2017/2018 hadi 2019/ 2020, TRA kwa Tanzania Bara wamekuwa wakiongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo taswira ya mwenendo wa makusanyo inabainisha kuwa makadirio ya juu yanayowekwa yanakuwa hayafikiwi kila mwaka.

Chati Na. 2.2: Mwenendo wa makusanyo ya Kodi kwa Tanzania – Zanzibar kati ya mwaka 2017/2018 – 2019/2020.



Chanzo: *Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa TRA kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020.*

Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa makusanyo kwa Tanzania Zanzibar, kwa miaka mitatu (3) ya fedha mtawalia pia umekuwa chini kidogo ukilinganisha na makadirio kama inavyoonekana katika chati Na. 2.2 hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua kwa kina hoja mbalimbali za ukaguzi ambazo zimechangia kutofikiwa malengo ya ukusanyaji wa mapato katika TRA hususan kwa mwaka 2019/2020. Hoja hizo mahsus ni kama zifuatavyo: -

a) Ongezeko la mashauri ya kodi katika vyombo vya rufaa za kodi yanayosubiri uamuzi. Kwa mwaka 2018/2019 kulikuwa na mashauri 770 yenye thamani ya **Sh. Milioni 366,036,394.67** ambayo hayajaamuliwa. Kwa mwaka 2019/2020 kumekuwepo na jumla ya mashauri 1097 yenye thamani ya **Sh. Milioni 360,496,241.98** ambayo hayajaamuliwa hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki kwa wakati⁹;

b) Ushuru wa forodha ambao haukukusanywa katika bidhaa za mafuta yanayopita nchini kwenda nje ya nchi yenye thamani ya **Sh. 136,376,033,167.** (CAG alibaini nyaraka za mizigo (*Bills of lading*) hamsini na tatu (53) za litu za mafuta

197,766,765 zenyе makadirio ya kodi ya kiasi cha **Sh. 136,376,033,167** kutoka kwa kampuni 12 ambazo hazikukadirwa kodi kwa matumizi ya ndani na hazikutolewa taarifa ya kusafirishwa nje ya nchi. Hatua hii ilienda kinyume na matakwa ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki (¹⁰EACCMA, 2004) na taratibu nyingine za forodha;

- c) Jumla ya makasha ya mizigo **281** yaliondolewa kwa ruhusa ya muda (*Provisional release*) kupitia fomu Na. 12 (Form C.12) na makampuni manne (4) bila ya kuzingatia taratibu za kodi (*Lodging assessments and payment of taxes*) kwa mujibu wa kanuni ya 49(2) ya EACCMR 2010¹¹;
- d) Uchambuzi wa Kamati ulibaini taarifa ya jumla ya magari **936** kutoka mfumo wa TANCIS¹² katika mipaka ya Namanga, Holili, Tarakea, Mtambaswala na Sirari ambayo yalikuwa yamepitilliza muda wake wa kukaa kwa miezi mitatu (3). Aidha, hapakuwepo uthibitisho wa maombi ya nyongeza ya muda wa kukaa kwa magari hayo kinyume na kanuni ya 136 (3) ya EACCMR, 2010;
- e) Dosari katika mfumo wa kushughulikia mashauri ya kodi (CIMIS)¹³. Ukaguzi umebaini uwepo wa dosari katika utunzaji wa taarifa wa kushughulikia mashauri ya kodi. Mathalani, katika kila Kanda ya kikodi, Meneja wa Kanda anaweza kuingia kwenye mfumo wa CIMIS kuangalia mashauri yanayoshughulikiwa na Meneja wa Kanda nyingine. Suala hili linaweza kuwa na athari katika maamuzi ya mashauri husika kwani Afisa asiye muadilifu anaweza kubadili nyaraka za ushahidi; na
- f) Mwisho, uchambuzi wa Kamati umebaini dosari kadhaa katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato kutoka kwa mauzo ya mwaka ya watu binafsi kupitia mfumo wa ITAX¹⁴.

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi wa hoja mahsusisita (6) katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamati imezingatia kwa kina mapendekezo ya CAG na hivyo kuboresha maoni na mapendekezo yake. Mapendekezo husika kuhusu kuongeza ufanisi wa TRA ili iweze kufikia

malengo ya ukusanyaji wa kodi stahiki yamefafanuliwa kwa kina katika sehemu ya tatu (3) ya taarifa hii.

2.2.4 Uchambuzi wa Hali halisi ya Kifedha na Mtaji Katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020 umebaini kuwa kwa mara ya kwanza baada ya miaka mingi Shirika lilipata faida ya kiasi cha **Sh. 45,246,000,000¹⁵** ukilinganisha na hasara ya **Sh. 34,228,000,000** iliyoripotiwa kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, Faida hii kwa TANESCO kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na kupungua kwa gharama za uendeshaji katika maeneo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kwa kipindi husika mapato ya Shirika yalipanda kwa **asilimia 2 (Sh. 1,564,353,000,000)** kutoka (**Sh. 1,535,040,000,000**) kwa mwaka 2019. Kwa muktadha huo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa gharama za mauzo ya umeme zilishuka kwa kiwango cha **asilimia 2** hivyo kuchangia kushuka kwa gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana katika Shirika, Kamati imebaini kuwa hali ya kifedha ya TANESCO bado ni changamoto hivyo inaweza kuathiri ufanisi wa Shirika hilo muhimu na la kimkakati hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa hesabu za TANESCO umebainisha kuwa Shirika lina changamoto ya mtaji hivyo kuhatarisha uwezo wa kutekeleza majukumu yake yanayoweza kujitokeza kwa muda mfupi na muda mrefu (*Current and future financial obligations*).

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi ufuatao katika jedwali Na. 2.2 unatoa kwa muhtasari hali halisi ya kifedha ya Shirika kwa sasa.

Jedwali Na. 2.2: Uchambuzi wa vigezo mbalimbali vyatathmini ya hali ya kifedha ya TANESCO

	Aina ya uwiano	Uchambuzi	Kiasi (Sh. Milioni)	Kiasi halisi cha uwiano	Tuliwa za 2020.
1.	Uwiano wa mali na Madeni ya muda mfupi madeni ya muda mfupi (Inventory ratio)	Uchambuzi ukuwa unatakiwa katika jedwali Na 2.2 hapo juu, uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi ya TANESCO upo katika Wastani wa 0.53 . Wastani unaopendekezo wa katika eneo hilo unatakiwa kuwa angalau 2.1 . Tafsiri zaidi ya uwiano huo ni kwamba, TANESCO ina changamoto ya kutimiza majukumu ya muda mfupi ya kimtaji kwa sababu kuna wastani wa Sh. 0.53 katika mali za muda mfupi inazotakiwa kugaramia dani la muda mfupi la kiasi	1,465,420.02	0.53	
2.	Uwiano wa ukwasi (Mali za muda mfupi) (Liquidity ratio)	Uchambuzi ukuwa unatakiwa katika jedwali Na 2.2 hapo juu, uwiano wa mali na madeni ya muda mfupi madeni ya muda mfupi (Inventory ratio)	1,456,388.12	0.53	
3.	Mtaji cha Sh. 1. (Working capital ratio)	Mheshimiwa Spika (2,761,812.68)	Madeni ya muda mfupi (1,465,420.02)	Madeni ya muda mfupi (1,465,420.02)	
		Mheshimiwa Spika (2,761,812.68)	Madeni ya muda mfupi (1,465,420.02)	Madeni ya muda mfupi (1,465,420.02)	Mheshimiwa Spika. Kwa upande wa uwiano wa ukwasi (Liquidity ratio), uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa katika eneo hilo uwiano upo katika wastani wa 0.53 wakati wastani unaotakiwa katika eneo hilo ni 1.1 . Tafsiri ya uwiano huo ni kwamba, TANESCO ina changamoto ya mtaji hivyo kuwepo uwezekano wa kuathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia taarifa ya ukaguzi, changamoto nyingine inayopunguza ufanisi wa kifedha wa TANESCO ni uwepo wa deni kubwa ambalo TANESCO inadai kutoka kwa Taasisi za Serikali na watu binafsi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020, TANESCO ilikuwa inadai kiasi cha **Sh. 422,372,936,233.61**. Uchambuzi wa kina wa deni hilo ulibaini kuwa kiasi cha **Sh. 56,045,155,042.73** (13%) ilikuwa ni deni lilitengenezwa ndani ya kipindi cha miezi minne (4). Aidha, kiasi cha **Sh. 366,327,781,190.88** (87%) ilikuwa ni deni la zaidi ya kipindi cha miezi minne (4).

Mheshimiwa Spika, Kutokana na uchambuzi wa muda wa uwepo wa deni (*Receivables aging analysis*) ambalo TANESCO inadai, ni dhahiri kuwa sehemu kubwa ya deni ni la muda mrefu ambalo halijakusanya hadi sasa. Katika hatua nyingine, CAG alifahamisha Kamati kuwa, jitihada kadhaa zimefanyika ambapo hadi kufikia Januari 2021 kiasi cha **Sh. Bilioni 14.4** kilikuwa kimekusanya. Kiasi hicho kinahusisha **Sh. Bilioni 7.8** kutoka Taasisi za Serikali na kiasi cha **Sh. Bilioni 6.1** kutoka kwa watu binafsi. Hata hivyo, hii ni sehemu ndogo tu ya deni ambalo Kamati imelibainisha hapo awali ambalo linatakiwa kukusanya ili kuongeza uwezo wa kifedha wa TANESCO kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Eneo lingine ambalo Kamati ilibaini kuwa linaathiri mizania ya hesabu za TANESCO ni uwepo wa deni la kiasi cha **Sh. Bilioni 493 (Dola za Kimarekani Milioni 200)**. Fedha hizi zilichukuliwa kama Mkopo na Serikali kwenda TANESCO wakati wa ujenzi wa mitambo ya gesi ya SONGAS. Kamati imezingatia ushauri na mapendekezo ya CAG katika eneo hili na yamewasilishwa katika sehemu ya tatu ya taarifa hii kama mapendekezo ya Kamati.

2.2.5 Matokeo ya Ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mheshimiwa Spika, Katika ukaguzi wa mwaka 2019/2020, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua hesabu za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Serikali (PSSF), Shirika la Taifa la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Mheshimiwa Spika, Hoja kubwa ambayo imepewa msisitizo na CAG katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni uwepo wa deni la muda mrefu ambalo mifuko inadai kwa Taasisi mbalimbali na hasa Serikali. Madeni hayo yanapunguza ufanisi wa kiutendaji wa mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, Kwa PSSSF ambapo deni liliohakikiwa ilikuwa **Sh. Bilioni 731**, CAG aliifahamisha Kamati kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Serikali ilikuwa imetoa kiasi cha **Sh. Bilioni 500** kupunguza deni husika. Aidha, kwa mwaka huu Serikali imetoa hati fungani maalum isiyo taslim (*Special non cash bond*) yenye thamani ya **Sh. Trilioni 2,176,740,000,000** ili kulipa deni la PSSSF.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hizi madhubuti zilizochukuliwa kwa upande wa PSSSF hali ambayo itasaidia kuimarisha mtiririko wa fedha wa Mfuko na malipo ya mafao kwa Wastaafu kwa wakati. Hata hivyo hoja ya madeni katika Mifuko ya NSSF na NHIF bado inahitaji jitihada za Serikali katika kuimaliza.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa NSSF, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2020 deni la Serikali ilikuwa kiasi cha **Sh. Trilioni 1.174** deni ambalo ni la kati ya mwaka 2007 hadi 2021¹⁶. Kwa upande wa NHIF deni la Serikali ni kiasi cha **Sh. Bilioni 209.70**. Madeni haya pamoja na kupunguza ufanisi wa Mifuko husika lakini pia yanaharibu taarifa za mizania ya fedha ya Mifuko kinyume na Kanuni za Kimataifa za Uandaaji wa Hesabu (IFRS).

2.2.6 Hali ya Mtaji na Ongezeko la Mikopo Chechefu (NPL) Katika Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Baada ya Kuunganishwa na Benki ya TIB Biashara

Mheshimiwa Spika, Iliyokuwa Benki ya Posta Tanzania (TPB) kwa nyakati tofauti iliunganishwa na iliyokuwa Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) na Benki ya Twiga. Mnamo tarehe

01 Juni, 2020, Serikali ilifanya uamuzi wa kuziunganisha iliyokuwa Benki ya Posta Tanzania na iliyokuwa Benki ya TIB Biashara. Lengo la Serikali kufikia maamuzi hayo lilikuwa kuungeza uwezo wa kifedha wa Benki za Serikali katika kuhudumia wateja wake.

Mheshimiwa Spika, Uamuzi wa kuziunganisha TIB Biashara na TPB umesababisha ongezeko kubwa la mikopo chechefu (*Non performing loans*) hali ambayo inaathiri hesabu za Benki mpya ya TCB. Ni kwa msingi huo, madeni chechefu yaliyorithiwa na TCB yanakula mtaji wa TCB ambayo hapo awali ilikuwa ikifanya vema sokoni.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati katika hesabu zilizokaguliwa za Benki mpya iliyounganishwa ya TCB umebaini masuala ya msingi katika Benki ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka. Hoja hizo ni kama ifuatavyo: -

- a) Mikopo chechefu imeongezeka kutoka **asilimia 5.87** mwaka 2019 hadi **asilimia 15.1** mwaka 2020;
- b) Faida ya Benki imeshuka kutoka **Sh.15,891,302,000** mwaka 2019 hadi **Sh. 5,865, 991,000** kutokana na kurithi mali za TIB Biashara ambazo hazizalishi faida; na
- c) Mikopo iliongezeka kutoka **Sh. 420,593,683,000** mwaka 2019 hadi **Sh. 617,813,683,000** ongezeko kubwa ikiwa ni mikopo iliyorithiwa kutoka TIB Biashara.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na kuunganishwa huko kwa TCB, mzigo wa madeni yaliyotoka TIB Biashara umesababisha kupungua kwa mtaji wa Benki. Kwa msingi huo na kwa kuzingatia Kanuni za Kimataifa za Uandaaji wa Hesabu (IFRS)¹⁷, mikopo husika ilitakiwa kutengewa tengo (*Impairment*)¹⁸ hali ambayo ingesababisha hesabu za Benki kupata hati yenye shaka kwa kutokuwa na mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na hoja ya mtaji kuathirika baada ya uunganishaji wa Benki husika, Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ambaye ni msimamizi wa sekta ya fedha alitoa

kibali maalumu (*Waiver*) kwa TCB ambacho kinaisha tarehe 28 Februari, 2022 kwa madhumuni kwamba Serikali ishughulikie suala la mtaji na ukusanyaji wa mikopo chechefu katika TCB.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 11 Februari, 2022 Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina (TRO) aliifahamisha Kamati kuwa wamepanga kutoa hati fungani isiyo taslim (*Non cash bond*) ya kiasi cha **Sh. Bilioni 130** ili kuongeza mtaji wa Benki. Hata hivyo hadi tunawasilisha taarifa hii, bado mchakato wa utoaji wa hati fungani hiyo ulikuwa haujakamilika.

2.2.7 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance audit report*) ya Utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari Mbigiri

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa fedha ulloishia Juni 30, 2020 CAG alifanya kagazi kadhaa za ufanisi katika nyanja mbalimbali. Moja wapo ya kagazi zilizofanyika ni ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji wa mradi wa uzalishaji sukari katika eneo la Mbigiri, Dakawa Morogoro.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Kamati umebainisha kuwa, kampuni hodhi ya Mkulazi ni kampuni iliyoundwa kwa ushirikiano baina ya Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSF) mnamo tarehe 6 Septemba 2016.

Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la kampuni ni kuzalisha na sukari nchini. Kwa sasa, Kampuni Hodhi ya Mkulazi inamilikiwa kwa pamoja na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSF) na Jeshi la Magereza. Muundo wa hisa za ubia ni asilimia 96 inayomilikiwa na NSSF na asilimia nne (4) inayomilikiwa na Magereza.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kuzalisha sukari yenyе ubora, Kampuni ilitarajiwa pia kuzalisha bidhaa zinazotokana na miwa. Ili kufikia lengo hili kampuni ilipanga kutekeleza miradi miwili ya sukari ambayo ililenga kuzalisha **tani 250,000** za sukari kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mojawapo ya miradi hiyo ni Mradi wa Uzalishaji Sukari wa Mbigiri ambao unatekelezwa katika shamba namba 217 lilitopo Mkulazi, Wilaya ya Morogoro Vijiji. Aidha, lengo la uzalishaji kwa shamba la Mkulazi ni kuzalisha **tani 200,000** za sukari kwa mwaka. Mradi mwingine upo katika eneo la Mbigiri lilitopo katika Wilaya ya Kilosa katika Mkoa wa Morogoro. Mradi huu unalenga kuzalisha **tani 50,000** za sukari kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha masuala kadhaa katika utekelezaji wa mradi wa uzalishaji sukari katika eneo la Mbigiri. Masuala hayo yanatakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuhakikisha malengo ya mradi yanafikiwa. Uchambuzi wa Kamati katika taarifa hiyo ulibainisha masuala muhimu yafuatayo: -

- a) Mapungufu katika usimamizi wa shughuli za shamba. Mathalani kulikuwa na visima vyenye thamani ya **Sh. Milioni 81.5** vilichimbwa lakini vilichelewa kuanza kutumika. Aidha, kulikuwa na matumizi ya mbolea na viuatilifu bila kuwa na maelezo ya matumizi yake;
- b) Ucheleweshaji wa ujenzi wa kiwanda cha sukari na usimikaji wa mitambo;
- c) Changamoto kwenye usimamizi wa shughuli za manunuzi na mikataba; na
- d) Kampuni ya Mkulazi haijasajiliwa ili kutoza kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Hoja nyininge ambayo ukaguzi wa ufanisi umeibua ni kuhusu mgawanyo wa hisa uliowasilishwa katika taarifa za fedha za Kampuni ya Mkulazi ambapo ni **asilimia 96** kwa NSSF na **asilimia nne** (4) kwa Jeshi la Magereza. Hata hivyo, mapitio ya nyaraka za makubaliano ya ubia ya tarehe 17 Oktoba, 2020 katika Bodii ya Wadhamini ya NSSF na Jeshi la Magereza yalibainisha kuwa taasisi hizi zilikubaliana kuhusu thamani ya mali zilizochangiwa na Jeshi la Magereza kuwa ni **Sh. 19,380,164,500**.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi zaidi katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi ulibainisha kuwa thamani ya mali hizo ambazo zilichangwa na Jeshi la Magereza zilikuwa ni zaidi ya **asilimia 4** ya kiasi cha mtaji wa ubia kilichoidhinishwa cha **Sh. Bilioni 250**. Hata hivyo ukokotozi halisi wa kiwango cha mtaji uliochangiwa ni **asilimia 7.6** ya mtaji wa ubia uliodhinishwa. Kwa muktadha huo, Kamati imebaini hoja ya mgawanyo sahihi wa hisa kwa kuzingatia kiasi halisi cha mali kilichochangiwa na wanahisa inahitaji kufanyiwa kazi na wanahisa kabla ya mradi kufikia hatua kubwa ya utekelezaji.

2.2.8 Kasi Ndogo ya Uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa Kupitia Mamlaka ya Vitambulisho Vya Taifa (NIDA)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa, NIDA ilinunua mashine mpya ikiwa ni mkakati wa kuongeza uwezo na kasi ya uzalishaji Vitambulisho vya Taifa. Mashine mpya za uzalishaji vitambulisho zilisimikwa na kuanza kutumika tarehe 14 Januari, 2021. Matumizi ya mashine mpya na kadi za uzao wa kwanza zimevezesha uzalishaji wa vitambulisho 3,007,509 kwa kipindi cha miezi minane (8) kuanzia tarehe 14 Januari, 2021 hadi 5 Oktoba, 2021 kwa kasi ya uzalishaji vitambulisho 1,000 kwa saa na kufanya jumla ya vitambulisho vilivyozaalishwa kufikia 9,879,184.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa mpango kazi wa uzalishaji wa vitambulisho kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ilitarajiwu ifikapo mwezi Juni, 2021 vitambulisho 13,735,728 vingezaalishwa. Hata hivyo, CAG amebainisha kuwa lengo hilo halikufikiwa kutokana na Mamlaka kuwa na changamoto ya kupata kadi mpya za uzao wa pili zinazoendana na mashine mpya ambazo kasi yake kwa saa ni vitambulisho 4,500 kwa saa kwa Mashine moja.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa kadi mpya haukuweza kufanyika kwa wakati kutokana na changamoto za kimkataba na mkandarasi ambazo ni makato ya kodi yasiyo sahihi, madeni ambayo hayajalipwa kutokana na huduma ambazo zilitolewa na mkandarasi na mashine tatu (3) za zamani kutofanyiwa matengenezo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Uhakiki uliofanywa na CAG katika Kituo cha uzalishaji cha Kibaha, tarehe 23 Septemba 2021 ulibaini kuwa mashine tatu (3) kati ya tano (5) zilizopo kituoni hazitumiki kutokana na kukosa riboni pamoja na matengenezo (*Maintenance*). Aidha, mashine mbili (2) mpya ambazo zinafanya kazi, kasi yake ya uzalishaji ni kadi 1,000 kwa saa badala ya kasi inayotakiwa ya kadi 4,500 kwa saa. Hali hii imesababisha NIDA kutokuwa na ufanisi wa kutosha pamoja na kutumia fedha nyingi za Serikali katika manunuzi ya mitambo mara kwa mara.

2.2.9 Usimamizi wa Mapato ya Serikali Katika Tume ya Madini

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya mwaka 2010 Sura 123 na Kanuni 5(4) ya sheria husika kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 7 ya mwaka 2017 inatoa maelekezo ya namna bora ya usimamizi wa rasilimali za madini yanapokuwa yakisafisirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Lengo la masharti ya vifungu husika ilikuwa ni kudhibiti mapato ya Serikali. Nukuu ya kifungu husika cha sheria ni kama ifuatavyo: -

Nukuu.

"Every permit to export minerals or samples of minerals shall, at the time of export, be surrendered by the licensed dealer to the postmaster or customs official through whom the export is effected and the postmaster or customs official, as the case may be, shall forthwith forward such permit to the authorized officer by whom it was issued".

Mwisho wa Nukuu.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa taarifa ya CAG katika ukaguzi wa Tume ya Madini kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2020 ulibaini uwepo wa vibali vyatya kusafirisha madini ya dhahabu na shaba (*Silver*) yenye thamani ya **Sh. 159,323,911,396** ambayo yalisafrishwa bila ya kuwa na kibali (*Mineral transportation document*) na ruhusa ya kibali cha Mamlaka ya Mapato Tanzania (*Customs verification remarks*).

Mheshimiwa Spika, Kamati imeamua kuileta hoja hii mbele ya Bunge lako Tukufu kutokana na mkanganyiko uliojitokeza kati ya maelezo ya Tume ya Madini. Pamoja na maelezo ya Tume ya Madini kuwa nyaraka husika zinapatikana TRA ili kudhibiti mapato ya Serikali, hata hivyo hadi ukaguzi unakamilika CAG aliifahamisha Kamati kuwa nyaraka za usafirishaji madini za kiasi cha Sh. **159,323,911,396** zilikuwa hazijawasilishwa kwa uhakiki. Hoja hii inahusu mapato ya Serikali inahitaji majibu na maelezo yenye uhakika.

2.2.10 Masuala ya Utawala Bora na Uwajibikaji wa Kifedha Katika Mabonde ya Maji Hapa Nchini

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanzisha jumla ya Mabonde ya Maji tisa (9) kupitia mabadiliko ya Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na 10 ya Mwaka 1982. Majukumu ya Mabonde haya yamefafanuliwa katika sheria husika ikiwa ni pamoja na kuandaa mipango kazi na utekelezaji wake katika sekta ya maji, kuunganisha mipango kazi ya maji ya Wilaya katika mipango ya maji ya kitaifa, kutoa miongozo kuhusu ujenzi wa miundombinu ya maji na utunzaji wa kanzi data za rasilimali za maji.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 06 Februari, 2022, Kamati ilikutana ili kupitia na kuchambua taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Maji ya Bonde Wami – Ruvu kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2020. Uchambuzi wa Taarifa ya CAG ulibainisha kuwa Bonde la Wami – Ruvu lillianzishwa mwezi Julai 2002¹⁹. Majukumu ya Bonde la Wami – Ruvu yamefafanuliwa katika Kifungu cha 23 cha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na kazi za msingi za Mabonde ya Maji, Taarifa ya CAG imebainisha changamoto za masuala ya utawala bora na uwajibikaji katika Mabonde ya Maji hapa Nchini. Changamoto hizo ni pamoja na Bodi za Mabonde ya Maji kumaliza muda wake na bodi mpya bado hazijateuliwa. Hali kadhalika, taasisi hizo zinakabiliwa na changamoto za kimuundo na kiutumishi kwa kuwa na upungufu wa wataalamu wa uhasibu na hesabu. Dosari hizo

zinasababisha kutokuwepo na uwajibikaji wa kutosha wa fedha za umma zinazotolewa katika Mabonde ya Maji hapa nchini.

2.2.11 Ongezeko la Riba ya Shilingi 2,196,680,467 Kila Mwaka Kutokana na Kutolipwa kwa Madai ya Mkandarasi Katika Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Fungu – 98 (Sekta ya ujenzi) ilikuwa inadaiwa kiasi cha **Sh. 31,381,149,525** sawa na (**Dola za Kimarekani 13,777,500**), kutoka kwa Mkandarasi aliyetekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Ibanda - Uyole. Madai haya ni ya tangu mwaka 1991 (miaka kumi na saba iliyopita).

Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka huu tunaoutolea taarifa deni hilo lilitozwa riba ya kiasi cha **Sh. 2,196,680,467** sawa na (**Dola za Kimarekani 964,425**) kutokana na kuchelewa kulipa madai husika.

Mheshimiwa Spika, Kupitia taarifa ya ukaguzi ya Wizara (Ujenzi), Kamati iliona mawasiliano ya Wizara kuomba fedha hizo kutoka Hazina kupitia barua zenyé Kumb. Na.CAB 198/215/10/56 ya tarehe 27/05/2021, CDA. 296/414/01/3 ya tarehe 14 Novemba, 2018 na AB.186/215/02/3 ya tarehe 5 Novemba, 2019.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo, hadi sasa bado malipo hayo hayajafanyika na hivyo kutozwa riba ya **Sh. 2,196,680,467** kila mwaka. Ni dhahiri kuwa malimbikizo ya deni husika na riba **ya Sh. 2,196,680,467** inayotozwa kila mwaka ni mzigo kwa Serikali kwani fedha hizo zingeweza kuelekezwa maeneo mengine yenye tija.

2.2.12 Uwiano wa Utoshelevu wa Mtaji (*Capital Adequacy ratio*) Kuwa Chini ya Kiwango Kinachohitajika Kisheria Katika Benki ya TIB Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni namba 19(2) ya Utoshelevu wa Mtaji wa Benki Kuu ya mwaka 2011 Benki ya

Maendeleo ya TIB inatakiwa kuwa na uwiano wa mtaji wa msingi (*Core Capital*) na mtaji wa jumla (*Total Capital*) kwa asilimia 13% na 15% mtawalia.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya ukaguzi ya TIB imebainisha kuwa katika Benki ya TIB Maendeleo, uwiano wa mtaji wa msingi na mtaji wa jumla kwa jumla ya mali zinazoambatana na vihatarishi (*Risk Weighted Assets*) ni asilimia 6.9 kwa mwaka wa fedha 2020. Aidha, changamoto hii ya kuwa na uwiano chini ya kiwango cha chini cha mahitaji ya mtaji ya kisheria ipo kwa miaka mitano (5) mfululizo.

Mheshimiwa Spika, Hadi kufika tarehe 31 Disemba 2020 Benki ilikuwa na Mtaji wa msingi (*Core capital*) na jumla ya mtaji (*Total capital*) uliofikia kiasi cha shilingi **bilion 38.358** wakati kima cha chini kinachohitajika kwa taasisi ya fedha za maendeleo ni kiasi cha shillingi **billion 50**.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya ukaguzi ya TIB ilifafanua kuwa, tarehe 11 Januari 2022 Benki ya Maendeleo TIB iliwasilisha mapendekezo kwa Wizara ya Fedha na Mipango ya kuongezewa mtaji. Mapendekezo ya TIB yaliomba mtaji wa **shilingi billion 373.78**. Kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali, Benki imeomba hati fungani maalumu (*Non-cash bond*) za **shilingi billion 373.78** na kibali cha kutoa hati fungani za Benki yenyeza za **shilingi billion 300**.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na changamoto katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba 2020 Benki ilishindwa kulipa amana zilizoiva (FDR) zenye jumla ya **Sh. 119,272,296,808.73** na **Dola za Marekani 28,758,949.78** kwa wadai wake. Kwa mujibu wa Kifungu 2.3 cha "**Fund mobilization manual**" na kanuni ya 60 ya Utoshelevu wa Mtaji wa Benki Kuu ya mwaka 2011, (DFI) inalojukumu la kuhakikisha inakuwa na ukwasi (*maintain liquid asset*) ambazo itawezesha DFI kulipa amana zote kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi tunachowasilisha taarifa hii, wateja wenye amana za jumla ya **Sh. 35,493,520,896** na **Dola za Marekani 11,281,712** sawa na asilimia 30% na 39% mtawalia

walikubaliana na ombi la Benki la kuendelea kushikilia amana zao pamoja na riba na kuacha amana zenyé jumla ya thamani ya **Sh. 83,778,775,912** na **Dola za Marekani 17,477,237** sawa na asilimia 70 and 61 mtawalia bila kutolewa maamuzi.

2.2.13 Madeni Ambayo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Linadai kwa TANESCO, SONGAS, Ndovu na PAET Sh. Bilioni 429

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) lilikuwa linadai Taasisi mbalimbali ikiwamo TANESCO, SONGAS, Ndovu na PAET jumla ya kiasi cha **Sh. Bilioni 429**.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kina wa umri wa deni hili ulibaini kuwa kiasi cha **Sh. Bilioni.209.7** killikuwa kinadaiwa kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita (6).

Mheshimiwa Spika, Uwepo wa deni hili ambalo halijalipwa kwa wakati unaathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa miradi ya TPDC. Mathalani, CAG amebainisha kuwa TPDC inakabiliwa na changamoto ya kasi ndogo ya utekelezaji wa miradi ya usambazaji gesi katika eneo la Mkuranga, mradi wa "*compressed natural gas project*", usambazaji gesi eneo la Tegeta - Bagamoyo na usambazaji gesi majumbani katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG imefafanua kuwa Serikali kupitia TANESCO waliingia makubaliano na TPDC ya kulipa kiasi cha **Sh. Bilioni 9** kila wiki ili kupunguza deni hilo. Hata hivyo hadi mwaka wa fedha 2020 unakamilika na hesabu zinafungwa na kukaguliwa deni hilo lilibaki **Sh. Bilioni 429**.

2.2.14 Masuala ya Ujumla katika Kaguzi za Hesabu za Sekretarieti za Mikoa (*Regional Secretariats*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya kaguzi mbili (2) za Sekretarieti za Mikoa. Sekretarieti za Mikoa zilizowasilishwa hesabu zake kwa Kamati ni Sekretarieti ya

Mkoa wa Geita Fungu – 63 na Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro Fungu – 79.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla kaguzi za hesabu za Sekretarieti za Mikoa umebaini masuala kadhaa ambayo Serikali inatakiwa kuyafanyia kazi ili kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Hoja hizo ni kama ifuatavyo: -

- a) Changamoto za usimamizi wa mikataba. Mfano katika Fungu – 63 Sekretarieti ya Mkoa wa Geita ilibainika dosari katika utekelezaji wa mkataba Na. RAS/GTA/203/2014/W/08 wenyе thamani ya **Sh. 113,566,034** ambaо ulifanyiwa nyонgeza ya **Sh. 89,190,654** (*Revised to TZS.202, 756,688*) ambaо ulichelewa kutekelezwa kwa miezi kumi na mbili (2) bila ya kumkata mkandarasi tozo ya uchelewaji;
- b) Dosari katika usimamizi wa malipo. Katika eneo hili ukaguzi wa Fungu – 63, RAS Geita ulibainisha malipo yaliyofanyika bila ya kuwa na nyaraka ya jumla ya **Sh.52, 380,442**;
- c) Dosari katika usimamizi wa mafuta ya magari na watumishi kukaimu kwa muda mrefu katika Fungu – 79; na
- d) Dosari katika uandaaji wa taarifa za fedha hali inayosababisha vitabu vya hesabu kufanyiwa marekebisho ya mara kwa mara.

2.2.15 Kusimama kwa Mradi wa Ujenzi wa Vihenge Unaotekelawa na Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) na Deni la Serikali la Sh.166, 447,544,945.82

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2020 ilibainisha kuwa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipokea mkopo wa **Dola za kimarekani Milioni 55** kutoka Serikali ya Jamhuri ya Poland kwa ajili ya Ujenzi wa vihenge na maghala ya kuhifadhia nafaka kupitia mkataba uliosainiwa na pande hizo mbili tarehe 28 Septemba, 2015.

Mheshimiwa Spika, Msimamizi wa ujenzi huu kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA). Baadhi ya masharti ya Mkopo huo ni kama ifuatavyo: -

- a) Muda wa kulipa mkopo ni miaka thelathini (30);
- b) Riba ya mkopo ni asilimia 0.3;
- c) Muda wa kutolipa mkopo (*Grace Period*) ni miaka tano (5); na
- d) Adhabu ya kuchelewa kulipa mkopo ni asilimia tatu (3).

Mheshimiwa Spika, NFRA inatekeleza mradi huu kupitia wakandarasi wawili kutoka nchini Poland ambao ni Unia SP Z.o.o na Ferum S.A. mkandarasi Ferum S.A anatekeleza mradi huo katika maeneo ya Dodoma, Shinyanga, Makambako, Songea na Mbozi kwa jumla ya thamani ya **Dola za Marekani Milioni 33.14** na mkandarasi Unia SP Z.o.o anatekeleza katika maeneo ya Babati, Sumbawanga na Mpanda kwa jumla ya **Dola za Marekani milioni 20.85**.

Mheshimiwa Spika, Hadi tarehe 31.12.2021 mradi eneo la Babati umekamilika, Mpanda umefikia 95% na Sumbawanga umefikia 90%. Aidha taratibu za kupokea mradi eneo la Babati zinaendelea. Kwa maeneo ya Mpanda na Sumbawanga, mkandarasi atakamilisha ujenzi na kukabidhi maeneo ifikapo tarehe 31 Machi 2022.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa mkandarasi Ferum SA kwa ujumla mradi umefikia asilimia 73 ya utekelezaji. Hata hivyo mkandarasi huyu amesimama utekelezaji wa mradi toka Desemba 1, 2020. Hii ilitokana na kukataliwa ombi alilowasilisha mwezi Septemba, 2020 la kutaka kuongezewa fedha kiasi cha **Dola za Marekani milioni 12.1**, kupewa fedha za zuio (*retention money*), kuongezewa muda wa utekelezaji kwa miezi 12, na kulipwa asilimia 50 ya fedha za nyongeza kabla ya kuendelea na utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Baada ya NFRA kutokulaliana na madai ya mkandarasi kwa kuwa yanakiuka mkataba, mkandarasi aliamua kuandika barua ya kuvunja mkataba tarehe 1 Desemba 2020. Wakala ulimjibu kupitia Meneja wa Mradi (TBA) kuwa jambo hilo halikubaliki kwa kuwa limefanywa kinyume na taratibu za mkataba, na hivyo kumtaka mkandarasi aendelee na utekelezaji wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, Kutokulaliana huko kwa pande mbili ndio kulikosababisha kuwepo kwa mgogoro uliopo sasa. Ni muhimu suala hili likafanyiwa kazi ili Serikali ipate thamani halisi ya fedha za umma zilizotumika katika mradi husika.

Mheshimiwa Spika, Hoja ya pili katika NFRA inahusu deni la Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu ambalo linatokana na mgao wa mahindi ya njaa kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi tarehe 30 Juni, 2015. Deni hilo limefikia kiasi cha **Sh. 166,447,544,945.82** kutokulipwa kwa deni hili kunaharibu mizania ya hesabu za NFRA na pia kunapunguza ufanisi wa Wakala katika kutekeleza majukumu yake.

2.2.16 Ukaguzi wa Bohari ya Madawa Tanzania (MSD)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya CAG katika ukaguzi wa Bohari ya Madawa Tanzania (MSD) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020 umebainisha kuwa hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya umeendelea kuimarika kutokana na mapokezi ya fedha ya manunuvi ya bidhaa za afya iliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Hata hivyo CAG amefafanua uwepo wa changamoto mbalimbali ambazo zinachangia kupunguza ufanisi wa MSD. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

- a) Deni ambalo Serikali inadaiwa na MSD kiasi cha **Sh. Bilioni 281**;
- b) Changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Manunuvi ya Umma katika uagizaji wa dawa na vifaa tiba ambapo MSD inatumia mlolongo mrefu kuagiza dawa;

- c) Kodi kwa malighafi zinazotumika kutengeneza dawa;
- d) Kodi kwa baadhi ya vifaa tiba vinavyohusika kutolea huduma muhimu kama kusafisha damu; na
- e) Utetemezi wa manunuzi ya dawa nje ya nchi kwa zaidi ya asilimia tisini (90).

Mheshimiwa Spika, Hoja hizo ni muhimu zikafanyiwa kazi ili kuboresha matumizi ya fedha za umma yanayoelekezwa katika MSD.

2.2.17 Kutokuwepo na Maeleo ya Kutosha Katika Hesabu za Fungu 56 – TAMISEMI Kuhusu Fedha Kiasi cha Sh. 2,066,018,559.95

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi wa hesabu zilizokaguliwa za Fungu – 56 Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020, Kamati ilibaini kiasi cha **Sh. 2,066,018,559.95** ambacho ni *“cash and cash equivalents”* ambacho hakikujumlishwa katika *“cash flow statement”* ya mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 10 Februari, 2022, Kamati ilimuagiza Afisa Masuuli – TAMISEMI kuwasilisha maeleo ya kina ya tofauti iliyoonekana katika vitabu vyta Wizara. Kupitia barua ya Katibu Mkuu – TAMISEMI ya tarehe 10 Februari, 2020 kwenda kwa Katibu wa Bunge yenye Kumb. Na. CE.69/239/01/12, Afisa Masuuli aliwasilisha maeleo kuhusu tofauti hiyo.

Mheshimiwa Spika, Maeleo ya Afisa Masuuli yalifafanua kuwa kiasi cha **Sh. 2,066,018,559.95** kutoonekana katika *“cash flow statement”* kilitokana na ukokotozi wa fomula kutovuta kiasi kilichopaswa kwa usahihi. Maeleo yake yaliendelea kufafanua kuwa badala ya fomula kuvuta kiasi sahihi cha **Sh. 44,963,929,249.94** fomula ilivuta kiasi cha **Sh. 42,897,910,689.99** na kusababisha tofauti ya **Sh. 2,066,018,559.95**.

Mheshimiwa Spika, Maelezo ya Afisa Masuuli yaliendelea kufafanua kuwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kiasi cha Sh. 2,066,018,559.95 kilihamishwa kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali (*Cash surrendered to PMG*) kwa kuwa ni fedha ambazo hazikutumika hadi tarehe 30 Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na maelezo ya ufanuzi wa Wizara, Kamati ilikuwa na hoja kadhaa ambazo bado zinahitaji majibu ya Wizara. Hoja hizo ni pamoja na hesabu za Fungu – 56 kufungwa na kuonekana zimekuwa sawa wakati tofauti hiyo haikuwa imefanyiwa marekebisho (*Adjustments*). Aidha, maelezo yaliyowasilishwa na Afisa Masuuli hayakuwa yamefanyiwa uhakiki na CAG kama Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 kinavyoelekeza.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maelezo ya Jumla

Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2020, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

3.2 Maoni

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati yanazingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusni cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni ya jumla kuwa bado kuna changamoto kwa baadhi ya taasisi za umma katika kuzingatia ipasavyo sheria zinazosimamia matumizi ya fedha umma. Kutokana na suala hilo, Kamati inasitisiza umuhimu wa Serikali kufanya kazi kwa wakati mapendekezo na

ushauri katika hoja za ukaguzi zinazokua zimeibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na maazimio yanayotolewa na Bunge katika kuongeza uwajibikaji katika rasilimali za umma.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na hilo, Kamati ina maoni kwamba ni vema Serikali iwe inachukua hatua za kisheria na kinidhamu kwa wakati kwa wahusika wanaokuwa wamethhibitika kuhusika kwa namna moja au nyingine katika ubadhirifu wa fedha za umma. Mwisho ni vema watumishi wa umma wakaendelea kujengewa uwezo katika utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa sheria na miongozo inayosimamia matumizi ya fedha za umma.

3.3 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika. Mapendekezo ya Kamati ni yale yanayolenga hoja zenye athari ya juu na hivyo kuhitaji utekelezaji wa haraka ili kuondoa matumizi yasifaa ya fedha za umma katika Taasisi za Serikali.

3.3.1 Kuhusu Ufanisi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

KWA KUWA, Kamati imefafanua kuhusu changamoto mbalimbali katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikiwa ni pamoja na uwepo wa rufaa nyingi za kodi ambazo hazijaamuliwa, dosari katika usimamizi wa ushuru wa forodha na mapungufu kadhaa ya mifumo ya ukusanyaji kodi;

NA KWA KUWA, Changamoto hizo zimesababisha kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya kodi kwa mwaka 2019/2020 kama yalivyofafanuliwa katika mwenendo wa ukusanyaji wa kodi katika chati Na. 2.1 na 2.2 zilizopo sehemu ya pili ya taarifa hii;

KWA HIYO BASI, Ili kuongeza ufanisi wa makusanyo ya kodi, Bunge linapendekeza kwamba: -

- a) Serikali iboreshe shughuli za vyombo vinavyohusika na kushughulikia rufaa za kodi (TRAT²⁰ na TRAB²¹) kwa kuvipa rasilimali za kutosha kwa maana ya fedha na watu ili vitekeleze majukumu yake kwa ufanisi na kumaliza mashauri ya kodi kwa wakati;
- b) TRA iimarishe mfumo wa ukadiriaji kodi kwenye mafuta yanayoingizwa hapa nchini kwa kuhakikisha nyaraka zote za mizigo zinapitiwa kwa kina na kodi stahiki zinalipwa. Aidha, TRA wahakikishe kodi ya kiasi cha **Sh. 136,376,033,167** inakusanywa pamoja na adhabu na riba inayotokana na kuchelewa kulipa kodi husika kwenye bidhaa za mafuta;
- c) TRA ihakikishe Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2009 na Kanuni zake za Mwaka 2010 zinazingatiwa ipasavyo na waagizaji wote wa mizigo; na
- d) TRA iboreshe mifumo yake ya CIMIS na ITAX kwa kuhakikisha mapungufu yaliyoibuliwa na CAG yanafanyiwa kazi ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi.

3.3.2 Hasara iliyotokana na Manunuvi na Usimikaji wa Mifumo wa ERP Katika Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA)

KWA KUWA, Kamati imebainisha changamoto ya kutokamilika kwa wakati mchakato wa usimikaji mifumo muhimu ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za TPA;

NA KWA KUWA, Kutokamilika mwa mifumo hiyo, hususan mifumo wa ERP kumeisababishia Serikali hasara ya takribani **Sh. 3,236,913,884.57** na **Dola za Kimarekani 2,306,839.8** zilizochambuliwa katika jedwali Na. 2.1 katika sehemu ya pili ya taarifa hii;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba: -

- a) Serikali ichukue hatua za kisheria kwa Kampuni zote ambazo zimehusika kuisababishia TPA hasara kama

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zilivyobainishwa kwa kina katika taarifa ya ukaguzi maalumu wa kiuchunguzi wa mfumo wa ERP uliofanywa na CAG;

b) Watumishi wote wa TPA waliotajwa kushiriki mchakato wa manunuzi na usimikaji wa mfumo wa ERP wachukuliwe hatua kwa kuzingatia matokeo ya kiuchunguzi na uhusika wa kila mmoja katika mchakato huo; na

c) Serikali itumie taasisi ya umma ya Wakala wa Serikali Mtandao (*E - Government*) kusimamia na kuratibu shughuli zinazoendelea za uwekaji mifumo ya TPA. Jambo hili litasaidia kuungeza uwajibikaji na kupunguza gharama ambazo Serikali imekwishaingia hadi sasa.

3.3.3 Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha changamoto za mtaji, madeni na dosari za kimkataba kati ya ATCL na TGFA;

NA KWA KUWA, Changamoto hizo zimesababisha ATCL kuendelea kupata hasara, kuwa na mtaji hasi na kutofikia malengo yake kwa mujibu wa mpango mkakati wa kampuni;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba; Serikali ikamilishe mchakato wa majadiliano kuhusu madeni ya ATCL na mapitio ya kina ya mikataba iliyopo kati ya ATCL na TGFA ili kuhakikisha dosari zinazosababisha hasara kwa ATCL zinaondolewa. Suala hili likamilike ndani ya mwaka huu wa fedha kama Serikali ilivyoitaarifu Kamati.

3.3.4 Kuhusu Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

KWA KUWA, Uchambuzi wa Kamati umebainisha changamoto ya mtaji katika Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), hasa kutokana na changamoto kama uwepo wa madeni makubwa ambayo Shirika linadai, changamoto za kimkataba kama ule wa ujenzi wa bomba la Songas na uchakavu wa njia za usafirishaji na usambazaji wa umeme;

NA KWA KUWA, Kutokuwepo kwa mtaji wa kutosha kumesababisha changamoto ya kiufanisi kwa TANESCO

katika kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme hapa nchini hali inayosababisha kutofikiwa ipasavyo kwa malengo mapana ya Taifa kiuchumi;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba: -

a) Serikali ichambue kwa kina na kuhakiki madeni yote ambayo TANESCO inadaiwa ikiwa ni pamoja na deni la "*capacity charge*" ya SONGAS kiasi cha **Sh. Bilioni 493.5** ili kuangalia uwezekano wa kubadilisha madeni hayo kuwa mtaji (*Equity*) hali itakayosaidia kusafisha mizania ya vitabu vya hesabu za TANESCO;

b) Shirika lihakikishe shughuli za manunuzi na usimamizi wa mikataba zinafanyika kwa kuzingatia sheria ili kuепusha ongezeko la gharama za uendeshaji; na

c) Mifumo ya udhibiti wa mapato iimarishwe sambamba na mifumo ya ICT pamoja na maboresho ya kina katika miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kupunguza upotevu wa mapato ya Shirika.

3.3.5 Hali ya Mtaji na Ongezeko la Mikopo Chechefu (NPL) Katika Benki ya Biashara Tanzania (TCB) Baada ya Kuunganishwa na Benki ya TIB Biashara

KWA KUWA, Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa Benki ya TCB umebaini changamoto za mtaji na limbikizo la madeni zinazotokana na kuunganishwa kwa TCB na iliyokuwa TIB Biashara;

NA KWA KUWA, Changamoto hizo zinaathiri ufanisi wa Benki kufikia malengo yake na malengo mapana ya Serikali katika kukuza uchumi;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza yafuatayo: -

a) Serikali ikamilishe ahadi yake ya kuongeza mtaji wa TCB kuititia utoaji wa hati fungani isiyo taslim (*Non cash bond*) ya **Sh. Bilioni 130** kabla ya kukamilika kwa mwaka wa fedha 2022;

- b) Serikali kupitia kwa vyombo vyake ihakikishe madeni ya TCB na yaliyorithiwa kutoka TIB Biashara yanakusanywa; na
- c) Serikali ikamilishe mchakato wa uunganishaji wa TCB ili Watumishi watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia sheria. Aidha, Serikali iangalie uwezekano wa kuwapangia majukumu watumishi katika ngazi ya Menejimenti waliotoka TIB Biashara.

3.3.6 Kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari Mbigiri

KWA KUWA, Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi wa mradi wa uzalishaji sukari katika shamba la Mbigiri umebainisha dosari kadhaa ikiwamo usimamizi mbaya wa shamba na kutosimikwa kwa kiwanda kwa wakati mwafaka;

NA KWA KUWA, Dosari hizo zimesababisha hasara kwa Wabia wa mradi (NSSF na Jeshi la Magereza) na wakulima wadogo wa miwa wa maeneo ya Dakawa;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba, Serikali itekeleze kwa ukamilifu mapendekezo yote kumi na mbili (12) yaliyotolewa na CAG katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi ili kuhakikisha malengo ya mradi yanafikiwa ipasavyo.

3.3.7 Kuhusu Mifuko ya Hifadhi za Jamii

KWA KUWA, Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG umebaini uwepo wa madeni ambayo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inadai kutoka Serikalini na kwa Taasisi mbalimbali;

NA KWA KUWA, Madeni hayo yanababisha Mifuko husika kutoweza kutimiza majukumu yake ya kisheria kwa ufanisi na kwa wakati;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba Serikali iendelee na hatua za kulipa madeni husika kwa kutumia njia mbalimbali kama ilivyoanza katika mfuko wa PSSSF. Hatua hizi za Serikali ziendelee katika mifuko ya NSSF na NHIF.

3.3.8 Kuhusu Tume Ya Madini

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha kwamba kuna nyaraka za usafirishaji madini za kiasi cha **Sh. 159,323,911,396** ambazo hazikuwa zimewasilishwa kwa wakaguzi kwa uhakiki ili kujiridhisha iwapo mapato stahiki ya Serikali yanakusanya;

NA KWA KUWA, Kutowasilishwa kwa nyaraka hizo ni kiashiria kuwa kuna uwezekano wa mapato ya Serikali kupotea katika utaratibu wa usafirishaji madini. Aidha, maelezo ya Tume ya Madini kwa Kamati na kwa CAG yaliibua mkanganyiko wa iwapo kuna ufanisi wa kutosha katika utaratibu wa usimamizi na udhibiti wa mapato ya Serikali katika usafirishaji wa madini;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba, Serikali kuitia Tume ya Madini iwasilishe nyaraka husika kwa CAG kwa uhakiki. Aidha, Serikali iboreshe mfumo wa udhibiti na usimamizi wa shughuli za usafirishaji wa madini ili kuhakikisha mapato stahiki ya Serikali yanakusanya.

3.3.9 Kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha kwamba Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa imeshindwa kufikia malengo ya utoaji wa Vitambulisho vya Taifa kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo za kimkataba na usimamizi;

NA KWA KUWA, Kutofikiwa kwa malengo ya utoaji wa Vitambulisho vya Taifa kunaathiri malengo mapana ya Serikali ya utoaji wa Vitambulisho husika na pia ni matumizi yasiyofaa ya fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba: -

- Serikali ikamilishe majadiliano na mkandarasi na taratibu za manunuvi ili kuwezesha kusainiwa kwa mkataba na upatikanaji wa kadi ghafi zipatazo 13,735,728 kwa kuzingatia idhini iliyotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kuongeza muda wa mkataba na mkandarasi, tarehe 29.05.2021, na

b) Serikali ipitie upya muundo wa Menejimenti na Bodi ya Ushauri ya NIDA ili kuweka mfumo thabiti utakaosaidia usimamizi wa utendaji wa NIDA kuwa na tija.

3.3.10 Mtaji Usiotosheleza wa Benki ya TIB Maendeleo

KWA KUWA, Kamati imebainisha hali halisi ya mtaji katika Benki ya TIB Maendeleo;

NA KWA KUWA, Kutokuwepo kwa mtaji wa kutosha kumekiuka sheria ya Benki Kuu inayosimamia taasisi za fedha na pia madhumuni ya kuanzishwa kwa Benki hayafikiwi;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba: -

a) Wizara ya Fedha na Mipango ichambue na kuangalia uwezekano wa kuongeza mtaji katika TIB Maendeleo ili kuiwezesha Benki Kulipa amana zilizoiva kwa taasisi zilizowekeza na pia kukidhi matakwa ya Kanuni namba 19(2) ya Utoshelevu wa Mtaji wa Benki Kuu ya mwaka 2011; na

b) Serikali iangalie uwezekano wa kutoa dhamana kwa TIB ili kuhakikisha inapata mikopo ya muda mrefu itakayoiwezesha Benki kufadhili miradi zaidi ya maendeleo. Kwa kutekeleza hilo Benki itapunguza hasara inayolipa kama tozo (*Commitment fees*) ya kushikilia mkopo kwenye Benki ya BADEA. (

3.3.11 Riba ya Shilingi Bilioni Mbili (2) Kila Mwaka Kutokana na Kutolipwa kwa Madeni ya Wakandarasi Katika Fungu 98 Sekta ya Ujenzi

KWA KUWA, Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG ulibaini kuwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi – Fungu 98) inadaiwa kiasi cha **Sh. 31,381,149,525** na riba ya **Sh. Bilioni 2** kila mwaka kutokana na kuchelewesha malipo ya mkandarasi;

NA KWA KUWA, Kutolipwa kwa deni hilo na riba inayotozwa kunaipa mzigo Serikali wa kutumia fedha **Sh. Bilioni 2** kila mwaka ambazo zingetumika katika maeneo mengine;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakiki na kulipa deni husika ili kuepuka riba inayotozwa kila mwaka ambayo ni hasara kwa Serikali.

3.3.12 Kuhusu Ujenzi wa Vihenge Katika NFRA na Deni la Serikali la Sh.166,447,544,945.82

KWA KUWA, Taarifa ya CAG imebainisha kuwa tangu tarehe 01 Disemba, 2020 mkandarasi Feerum SA amesimama ujenzi wa vihenge katika maeneo ya Dodoma, Shinyanga, Makambako, Songea na Mbozi na pia NFRA inaidai Serikali kiasi cha Sh. 166,447,544,945.82 kilichotolewa kwa mgao wa mahindi wakati wa njaa;

NA KWA KUWA, Kusimama kwa mradi ambao umefikia asilimia 73 ya utekelezaji kutaongeza ghamra kwa Serikali na kutofikiwa thamani ya fedha ambayo Serikali ilichukua mkopo. Aidha, kutokulipwa kwa deni ambalo NFRA wanaidai Serikali kunapunguza ufanisi wa NFRA;

KWAHIYO BASI, Bunge linapendekeza kwa Serikali kutekeleza yafuatayo:-

a) Serikali ichukue hatua stahiki ili kukamilisha mradi wa ujenzi wa vihenge uliosimama tangu mwaka 2020 ili thamani halisi ya fedha za umma ipatikane. Aidha, Serikali ifanye tathmini na kuititia upya masharti ya makubaliano ya mkopo uliochukuliwa kutoka nchini Poland kwa ajili ya ujenzi wa vihenge ili kuondoa masharti hasi yaliyopo katika mkopo huo; na

b) Serikali kuititia Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, walipe deni la NFRA ili wakala uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

3.3.13 Uwajibikaji Katika Mabonde ya Maji

KWA KUWA, Kumekuwepo na changamoto za kutokamilika muundo na kutooundwa kwa Bodi katika Mabonde ya Maji ikiwamo Bonde la Wami Ruvu;

NA KWA KUWA, Changamoto hizo zinaathiri masuala ya uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kukamilisha muundo wa Bodi zote za maji hapa nchini na kuhakikisha kunakuwepo watumishi wa kutosha wenyewe taaluma za uhasibu ili kuhakikisha uwajibikaji katika fedha za umma.

3.3.14 Madeni Ambayo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Linadai kwa TANESCO, SONGAS, Ndovu na PAET Sh. Bilioni 429

KWA KUWA, Kupitia taarifa ya ukaguzi ya CAG, Kamati imebainisha uwepo wa deni la takribani **Sh. Bilioni 429** ambalo TPDC inadai kutoka kwa TANESCO, SONGAS, PAET na Ndovu;

NA KWA KUWA, Kutokulipwa kwa deni hilo kunaathiri ufanisi wa TPDC katika kutimiza majukumu yake;

KWA HIYO BASI, Bunge linapendekeza kwamba, Serikali ifanye mapitio ya madeni ambayo TPDC inadai kwa Taasisi mbalimbali ikiwamo TANESCO, SONGAS, PAET na Ndovu ili kuangalia utaratibu bora wa kuondoa madeni hayo. Aidha, TPDC iongezewe uwezo wa kirasilimali ili kutekeleza miradi ya gesi ambayo ni muhimu kwa uchumi na mazingira.

3.3.15 Masuala ya Ujumla katika Kaguzi za Hesabu za Sekretarieti za Mikoa (*Regional Secretariats*)

KWA KUWA, Kupitia taarifa ya ukaguzi ya CAG, Kamati imebainisha changamoto kadhaa katika Sekretarieti za Mikoa;

NA KWA KUWA, Changamoto hizo zinaweza kuwa na athari katika uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba; Sekretarieti za Mikoa ziwezeshwe kuwa na watumishi wa kutosha na wenyewe sifa katika maeneo ya manunuzi, uhasibu na sheria. Hii itasaidia kuongeza hali ya uwajibikaji na uzingatiaji wa sheria

katika masuala ya fedha, manunuzi na mikataba katika Sekretarieti za Mikoa.

3.3.16 Kuhusu Bohari ya Madawa Tanzania (MSD)

KWA KUWA, Taarifa ya ukaguzi ya CAG, imefafanua kwa kina changamoto zilizopo katika Bohari ya Madawa Tanzania (MSD) ikiwa ni pamoja na deni ambalo Serikali inadaiwa, changamoto za utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, kukosekana kwa viwanda vya kuzalisha dawa hapa nchini na uwepo wa kodi katika dawa na vifaa tiba;

NA KWA KUWA, Changamoto hizo kwa ujumla wake zinaongeza gharama kwa Serikali kuititia MSD katika kutoa huduma kwa wananchi;

KWA HIYO BASI, Bunge inapendekeza yafuatayo: -

- a) Serikali ikamilishe ulipaji wa deni ambalo inadaiwa na MSD na kuhakikisha inatoa fedha kwa Bohari kwa kuzingatia bajeti iliyopitishwa na Bunge;
- b) Serikali iangalie uwezekano wa kufanya mapitio ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ili kutoa fursa kwa MSD kuagiza na kununua dawa kwa haraka kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika
- c) Serikali ipitie upya Sheria za kodi katika eneo la dawa na vifaa tiba ili kupunguza mzigoto wa gharama kwa Serikali na MSD unaotokana na kodi husika;
- d) Serikali iweke jitihada katika uwekezaji wa ujenzi wa viwanda vya dawa hapa nchini ili kupunguza fedha za umma zinazoenda nje ya nchi kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

3.3.17 Kuhusu Fungu – 56 OR TAMISEMI

KWA KUWA, Kupitia taarifa ya ukaguzi ya CAG, Kamati imebainisha dosari katika hesabu za Fungu – 56 TAMISEMI ambapo kiasi cha Sh. **2,066,018,559.95** cha “cash and cash equivalents’ hakikuonekana kwenye taarifa ya mtiririko wa fedha (*Cash flow statement*);

NA KWA KUWA, Kutoonekana kwa taarifa hizo kunaenda kinyume na matakwa ya Kanuni za Kimataifa za Uandaaji wa Taarifa za Hesabu katika Sekta ya Umma (IPSAS)²²;

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba CAG afanye uhakiki wa kina wa hesabu za Fungu 56 - TAMISEMI ili kubaini hali halisi ya hoja husika na kuliarifu Bunge ipasavyo.

SEHEMU YA NNE

- 4.0 **HITIMISHO**
- 4.1 **Shukurani**

Mheshimiwa Spika, Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini na kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge letu. Uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. **Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

- 1) Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb-**Mwenyekiti**
- 2) Mhe. Japheti Ngailonga Hasunga, Mb – **M/ Mwenyekiti**
- 3) Mhe. Dr. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb
- 4) Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
- 5) Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
- 6) Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
- 7) Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
- 8) Mhe. Juma Othman Hija, Mb
- 9) Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
- 10) Mhe. Deus Clement Sangu, Mb
- 11) Mhe. Francis Kumba Ndulane, Mb
- 12) Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb
- 13) Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
- 14) Mhe. Aysharose Ndogoli Matembe, Mb
- 15) Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb

- 16) Mhe. Maimuna Ahmad Pathan, Mb
- 17) Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
- 18) Mhe. Jakcline Kainja Andrea, Mb
- 19) Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
- 20) Mhe. Zubeida Khamis Shaibu, Mb
- 21) Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb
- 22) Mhe. Bakar Mohamed Bakar, Mb
- 23) Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb
- 24) Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mb

Mheshimiwa Spika, Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa ushauri wake kwa Kamati. Natoa shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kuititia kwa Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athuman Hussein, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Mswige Dickson Bisile, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Sostenes Maseke na Ndugu Amina Salum Namtema.

Mheshimiwa Spika, Mwisho japo sio kwa umuhimu, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa iliuopata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukarusi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere. Aidha naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kuititia kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen), Msajili wa Hazina (TR), Kamishina wa Bajeti (CB) na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotha katika kuratibu shughuli za Kamati.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
HESABU ZA SERIKALI (PAC)

17 Februari, 2022

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

KIAMBATISHO NA. 1

Mwaka	Kes	MhakamaRiari		TAT		TAXPAYER AS BOARD (TAB)		TOTAL	
		TSh	USD	TSh	USD	TSh	USD	TSh	USD
2015	5	-	-	-	-	10,728,742,411	-	10,728,742,411	-
2016	18	-	-	-	-	13,582,461,801	-	13,582,461,801	-
2017	77	-	-	-	-	30,030,914,301,164	2,486,022	30,030,914,301,164	2,486
2018	197	118,996,637,329	41,230,465	1,183,39,32,160	-	62,297,927,431	-	199,663,916,920	41,231
2019	474	11,152,775,395	-	1,352,89,25,125	1,469,920	457,32,985,079	5,355,122	5961,40195,599	6,606
2020	36	46,682,806,111	10,888,6384	14,007,382,224	22,000,818	55,627,051,852	-	74,033,240,187	13,08
TOTAL	1077	176,822,1885	150,137,310	2,681,308,09,510	2,945,738	357,223,517,42,771	7,941,204	36,081,657,601,115	81,4

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. (*Makofi*)

Mwenyekiti, naamini umebeba kitakasa mkono. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*Local Authorities Accounts Committee*), Mheshimiwa Grace Tendega. (*Makofi*)

MHE. GRACE V. TENDEGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kumshukuru Mwenyezezi Mungu kwa nafasi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya mwaka kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza; tarehe 8 Aprili, 2021 Serikali iliwasilisha Bungeni taarifa mbalimbali za hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguza Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020. Miiongoni mwa taarifa hizo ni taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, chini ya Kanuni ya 136(15) Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) ili iweze kujadiliwa na kuafikiwa na Bunge lako tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha taarifa hii, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwako kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sifa zako kitaaluma, uzoefu na ufanisi katika uongozi zimetukuka sana. (*Makofii*)

Aidha, nina mpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Matumaini ya Wabunge, Serikali, watumishi wa Bunge na umma kwa ujumla juu ya uongozi wenu ni makubwa sana; Mwenyezi Mungu aweze kuwajalia afya njema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo, aidha, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Nape Mosses Nnauye (*Mbunge*), aliyekuwa Mjumbe wa Kamati hii kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kamati inamtakia kila lenye heri katika utekelezaji wa majukumu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tatu; sehemu ya kwanza inayoelezea shughuli zilizotekeliza na Kamati kwa mwaka wa fedha 2021, mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati, wadau walioshirikishwa na nyaraka zilizotumika.

Sehemu ya pili inabainisha matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya *CAG* ya mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwa ni

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

pamoja na taarifa ya kaguzi maalum na mahojiano na Maafisa Masuuli vikaoni na ziarani; sehemu ya tatu inaelezea maoni na mapendekozo ya Kamati katika hoja mahsusizi zinazohusu maeneo yenye mwenendo usioridhisha wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, nakala za taarifa hii zimewekwa kwenye vishkwambi, ninaomba taarifa yote inukuliwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama nilivyowasilisha Mezani kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili; uchambuzi wa taarifa ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na matokeo ya ziara na majadiliano; katika mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya Halmashauri 185 zilikaguliwa na CAG katika Halmashauri hizo, 124 sawa na 67% zilipata hati safi za ukaguzi, Halmashauri 53 sawa na 29 % zilipata hati zenye mashaka na Halmashauri nane sawa na 4% zilipata hati mbaya. Kwa ajili ya taarifa hii, LAAC imeweza kuhoji jumla ya Halmashauri 40 sawa na 21.6% ya Halmashauri zote zilizokaguliwa.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa aina za hati za ukaguzi tangu mwaka 2015/2016 - 2019/2020 unaashiria kuna kuimariika kwa nidhamu na matumizi kiasi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, idadi ya hati safi za ukaguzi ni zaidi ya asilimia 50. Takwimu hizi zinaashiria kuimariika kwa taasisi za usimamizi wa fedha zikiwemo Bunge, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, TAKUKURU, Mabaraza ya Madiwani, Asasi za Kiraia, vyombo vyaa habari na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, aidha, msukumo unaowekwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassani kuhusu nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni dira tosha kwamba kila senti ya Serikali lazima ilete tija katika maendeleo ya jamii.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, maeneo yenye mwenendo mbaya wa Matumizi ya Fedha za Umma katika Halmashauri; Kamati imebaini maeneo yafuatayo kuwa na mwenendo usiofaa katika mapato au matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa:-

Mheshimiwa Spika, moja, fedha za ruzuku ya maendeleo hazitolewi ipasavyo na Serikali kuu kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Fedha hizi hutolewa chini ya masharti ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982. Zipo Halmashauri zinazopata ruzuku zaidi ya maombi yao, zingine chini ya maombi yao na zingine hupata lakini kwa kuchelewesewa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 890.3 ikiwa ni ruzuku ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi taarifa za Hesabu zilipofungwa, kiasi cha shilingi bilioni 479. 9 tu cha fedha zilizoidhinishwa kilitolewa. Hii ni pungufu ya 46% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Halmashauri zinazopata fedha zaidi ya kiasi zilichohitaji hujenga tabia ya ubadhirifu kwa kufanya manunuzi nje ya mipango ya manunuzi kwa mwaka. Halmashuri zinazopata fedha kidogo hazikamilishi miradi kwa wakati sawasawa na zile zinazochelewesewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba fedha za ruzuku ya maendeleo zisipotolewa ipasavyo, huchochea matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Kwa namna iliyofafanuliwa zaidi katika Kipengele 2.1.1 cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mbili, kuna Matumizi ya "fedha mbichi" kwa lengo la kukwepa kubainika katika mifumo ya kielektroniki. Katika Halmashauri Serikali kuu imeweka mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuwezesha ukusanyaji wa mapato (*LGRCIS*) na Mfumo wa kunukuu matumizi ya mapato yanayokuwa yamekusanywa (zamani *EPICOR* na sasa *MUSE*). Mifumo hii miwili hulishana taarifa zinazoisaidia Mamlaka

husika kujua mwenendo wa mapato na matumizi yao kwa mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, ili mfumo wa kunukuu matumizi (*MUSE*) upate taarifa ni sharti mapato yaliyokusanywa yapelekwe kwanza katika benki kabla ya kutumika. Mapato yanayotumika kabla ya kupelekwa benki ndiyo tunayoyaита "fedha mbichi".

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, jumla ya shilingi bilioni 18.7 zilikusanywa na kutumika kabla ya kupelekwa benki katika halmashauri mbalimbali nchini. Hii ina maana kwamba kiasi hicho cha fedha hakikusomeka kwenye mfumo wa matumizi mwishoni mwa mwaka husika wa fedha. Kamati ina maoni kwamba matumizi ya fedha mbichi yana nia moja tu ya kukwepa kuonesha mapato halisi yaliyokusanywa na halmashauri husika hivyo wahusika kujipatia manufaa binafsi ya fedha kuijanja ujanja. Maelezo zaidi yapo katika Kipengele 2.1.2 cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuna tatizo la Kufutwa kwa miamala ya mapato katika mfumo wa kielektroniki bila ya kuwepo kwa uthibitisho kwamba miamala hiyo inastahili kufutwa. Kamati imebaini kwamba kuna ujanja unatumia na baadhi ya watendaji katika halmashauri zetu ili wawewe kujipatia manufaa binafsi ya kifedha. Ujanja huu unatendeka kwa kufuta ama kurekebisha baadhi ya miamala ya fedha inayoingia kwenye mfumo wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yote yamebainika kuwa ni ya kupunguza kiasi cha fedha zilizokusanywa wala siyo kuongeza. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya shilingi bilioni 4.5 zilifutwa kwenye mfumo kwa njia ya ujanja huu. Suala hili limeeleza kwa upana zaidi kwa maana ya madhara yake katika kipengere Na. 2.1.3 cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, nne, kiasi cha mishahara ya Watumishi kinachotumwa na Hazina (*Exchequer Release*) katika baadhi ya halmashauri kina tofautiana na mahitaji

halisi ya mishahara katika halmashauri hizo katika Mfumo wa *Lawson*. Hoja hii ina viashiria vya kuibuka tena kwa mishahara hewa katika Utumishi wa Umma nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya Halmashauri Mkoani Tabora, kiasi cha mishahara kinachopelekwa na Serikali (Hazina) ni kikubwa kuliko kiasi halisi kinachotakiwa katika Halmashauri husika katika Mfumo wa Mishahara (*Lawson*). Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo mahitaji ya *Lawson* ilikuwa ni bilioni 13.0 lakini Hazina ilitoa shilingi bilioni 13.3 hivyo kusababisha ziada ya shilingi milioni 145.7. Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua Mahitaji ya *Lawson* yalikuwa ni shilingi bilioni 17.6, lakini Hazina ilipeleka shilingi bilioni 17.8, hivyo kuwa na ziada ya shilingi milioni 209.9. Halmashauri ya Wilaya ya Uyui mahitaji ya *Lawson* yalikuwa shilingi bilioni 17.0, lakini Hazina ilipeleka shilingi bilioni 17.3, hivyo kuwa na ziada ya shillingi milioni 309.3.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikupata majibu kuhusiana na sababu za kuwepo kwa hali hiyo. Maoni yake ni kwamba, huu ni uhalifu katika matumizi ya fedha za umma nchini. Maelezo zaidi yapo katika kipengele 2.1.4 cha Taarifa ya Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tano, kuna udhaifu katika kukusanya mapato ya ndani ya Halmashauri kutokana na sababu mbalimbali kama vile:

(a) Tathimini isiyo sahihi ya fursa za kiuchumi katika baadhi ya Halmashauri;

(b) Uandaaji na usimamizi mbovu wa mikataba mbalimbali ya manunuzi ya huduma au utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(c) Tathimini isiyo sahihi ya uhimilivu wa baadhi ya vyanzo vya mapato kutozwa kodi ya viwango vya juu;

(d) Hujuma katika mashine za kukusanya mapato (*Pos*);

(e) Kutofungwa mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato (*GoTHOMIS*) kwenye hospitali na vituo vyta kutolea huduma za afya;

(f) Udmaifu katika kusimamia marejesho ya *NHIF*;

(g) Udmaifu katika utendaji wa Vitengo vyta Udhibiti wa Ndani; na

(h) Kulegalega kwa motisha wa Serikali kwa Watendaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba endapo Serikali itatekeleza kikamilifu ushauri wa Kamati katika masuala yaliyo orodheswa hapo juu, uwezo wa Halmashauri kujitegemea kimapato utapanda zaidi ya hali ilivyo sasa. Maelezo ya kina yapo katika Kipengele 2.1.5 cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, sita, kutopeleka kikamilifu asilimia 40 ya michango katika miradi ya maendeleo. Kuna utaratibu wa Serikali kwamba halmashauri ziwe zinatenga kiasi fulani (40% au 60%) cha mapato yao ya ndani kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya jamii. Utaratibu huu unakusudia kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kama vile elimu, afya, mawasiliano na maji katika maeneo mbalimbali ya halmashauri. Kamati imebaini kwamba utaratibu huu hautekelezwi ipasavyo, hivyo kuathiri nia iliyokusudiwa. Maelezo zaidi yapo katika Kipengele 2.1.6.

Mheshimiwa Spika, kutopeleka kikamilifu asilimia 10 ya Makundi Maalum; utaratibu wa Serikali kwamba Halmashauri ziwe zinatenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuyawezesha Makundi Maalum kwa maana ya Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu ulitokana na Ushauri wa Bunge lako Tukufu. Madhumuni ya utaratibu huu ni kuharakisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuyasaidia Makundi Maalum yajikwamue kiuchumi. Hivyo, utaratibu huu ni takwa la kisheria chini ya Kifungu cha 37A cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290; na

unasisitizwa katika Mwongozo wa Maandalizi ya Bajeti ya Serikali kila mwaka. Kamati imebaini kwamba utekelezaji umekuwa ni wa kusucasua. Huu ni ukiukwaji wa Sheria ambao madhara yake ni kuzorota kwa maendeleo ya vikundi lengwa. Ufanuzi zaidi upo katika kipengele 2.1.7 cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, nane, madeni makubwa ya baadhi ya Halmshauri kutokana na Mikopo ya Mabenki na Madai ya Watumishi; kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982, mikopo ni mionganoni mwa vyanzo vyatuhusu ya halmashauri. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya halmashauri kama vile Halmashauri ya Jiji la Mbeya inadaiwa na Benki ya *CRDB* takribani Shilingi bilioni 29 ikiwa ni mkopo, riba na adhabu. Jiji la Mbeya liliropa fedha hizi kwa ajili ya kujenga Soko Kuu la Mwanjelwa kwa dhamana ya Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, ambayo pia ina madeni makubwa ya aina hii. Mikopo hii sasa imegeuka kuwa mzigo mzito usioweza kuvutwa tena na halmashauri hizo. Aidha, zipo dalili za Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutumbukia katika mikopo ya aina hii endapo tahadhari hazitachukuliwa katika kukamilisha Jengo la Kitega Uchumi chake katika Mji wa Mtumba. Ukamilishaji wa Kitega Uchumi hicho unakadirisha kutumia shillingi bilioni 59 ikiwa ni mapato ya ndani. Mpaka sasa kiasi kilicholipwa ni shillingi bilioni 18. Sehemu kubwa ya mapato ya ndani yanayotegemewa yanatokana na mauzo ya viwanja. Hoja hii imeelezewa zaidi katika Kipengele 2.1.8 cha Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Malipo ya Kazi na Huduma mbalimbali kutolewa kabla ya Kuhakiki Ubora wa Kazi au Huduma Kifungu cha 243(2)na (3) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013, kinataka malipo ya kazi na huduma yafanyike baada ya taasisi nunuzi kujiridhisha na kiwango au ukubwa wa kazi au huduma iliyotolewa. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba utaratibu huu mara nyingi hauzingatiwi, hivyo kuathiri ubora wa kazi na huduma. Kwa mfano, katika

ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilimlipa Mkandarasi kiasi cha shilingi milioni 72 bila ya kuwepo kwa uhakiki wa kazi iliyofanyika. Halmashauri hii imetumiwa kama mfano kuthibitisha kwamba tatizo lipo na Serikali ichukue hatua. Maelezo mengine yako Kipengele 2.1.9 cha Taarifa.

Mheshimiwa Spika, kumi, Zabuni za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutangazwa kabla ya kupata idhini ya Bodi za Zabuni. Madhumuni ya Serikali kuweka utaratibu wa kuwa na Bodi za Zabuni ni kuimarisha uwazi, tija na uwajibikaji katika manunuzi ya umma. Hivyo, inapotokea kwamba zabuni zinatangazwa bila idhini ya Bodi inakuwa ni ukiukwaji wa makusudi wa Kanuni ya 185(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013. Aidha, hali hii ni kiashiria cha kukosekana kwa uwazi, tija na uwajibikaji unaotakiwa kuwepo. Ufafanuzi upo Kipengele 2.1.10.

Mheshimiwa Spika, kumi na moja, kuwepo kwa mali nyingi chakavu (magari) katika Halmashauri zetu; Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba katika Halmashauri mbalimbali nchini kuna mrundikano mkubwa wa magari yaliyochakaa. Uchakavu wa gari hizo umeendelea kuwa hasara kwa Serikali kutokana na kwamba haziondolewi kwa wakati zinapokuwa zimechokaa. Hoja hi inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutolewaka vema kwa utaratibu wa kuza mali hizo zinapokuwa zimechakaa.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyotajwa hapo juu ndio mianya mikubwa ya ubadhirifu wa fedha za umma katika Serikali za mitaa. Kamati inaomba Bunge Iako Tukufu liyajadili kwa kina maeneo hayo ikiwa ni pamoja na ushauri uliotolewa ili kuongeza mapato na kuleta matumizi yenye tija ya fedha zinazokusanywa.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati; kwanza, kuhusu Ruzuku ya fedha za maendeleo katika kutopelekwa ipasavyo:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa kuwa Kamati imetoa ushahidi usio na shaka kwamba ruzuku ya fedha za maendeleo haipolekwi ipasavyo katika Halmashauri. Zipo Halmashauri zinazopelekewa fedha nygingi kuliko kiasi kilichoombwa, zingine zinapelekewa fedha pungufu na kwa kuchelewa au fedha hutumwa na kurejeshwa Hazina bila maelezo;

Na kwa kuwa vitendo vilivyoelezwa hapo juu vinaathiri utekelezaji wa mipango ya Mamlaka husika katika kuboresha huduma za jamii;

Kwahiyo basi Bunge linaishauri Serikali iwe na uhalisia katika kuandaa bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa na ipeleke fedha za maendeleo katika Mamlaka hizo kwa kuzingatia Sheria ya Matumizi inayotungwa na Bunge kila mwaka ili Mamlaka hizo ziweze kutekeleza ipasavyo miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu unakusudia kuihimiza Serikali kuongeza juhudni katika kubuni vyanzo thabiti nya mapato, kuimarishe mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kupeleka ipasavyo fedha zinazokusanywa ili zikaboreshe maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu matumizi ya “fedha mbichi”:-

Kwa kuwa mifumo ya kielektroniki ya mapato na matumizi ya fedha za umma imewekwa na Serikali kwa ajili ya kuimarishe nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma nchini;

Na kwa kuwa, imebainika sasa kwamba matumizi ya fedha mbichi ni ujanja wa kuzifanya fedha hizo zisionekane katika mfumo wa kielektroniki wa matumizi pindi hesabu zitakapofungwa mwishoni mwa mwaka;

Kwa hiyo basi Bunge linaielekeza Serikali kwamba ni marufuku kutumia fedha mbichi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Watendaji wote watakaobainika kutokutii agizo hili

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wachukuliwe hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi. Pendelekezo hili lina kusudia kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika kukusanya na kutumia fedha za umma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu kufutwa kwa Miamala ya Mapato katika Mifumo ya Kielektroniki bila ya Uthibitisho:-

Kwa kuwa Mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato iliwekwa kwa ajili ya kusaidia ufanisi katika kukusanya na kutunza kumbukumbu za mapato;

Na kwa kuwa imebainika kwamba mifumo hiyo ina mianya ya watendaji wasio waaminifu kuweza kupenya na kuiibia Serikali kimtandao kwa kufuta au kurekebisha miamala ya makusanayo ya fedha;

Kwa hiyo basi Bunge linaitaka Serikali:

(a) Ihakikishe kuwa mamlaka ya kurekebisha ama kufuta miamala kwenye mfumo wa mapato inabaki kwa Afisa Masuuli tu baada ya kujiridhisha na nyaraka halisi za mapendekezo ya kufanya hivyo;

(b) Kuimarisha ubora wa risiti za kielektroniki zinazotolewa na mashine za kukusanya mapato nchini ili ziwe na maandishi yanayosomeka vema na yasiyofutika kirahisi kwa lengo la kutunza kumbukumbu za miamala; na

(c) Kuimarisha usalama na udhibiti wa miamala katika mfumo wa mapato (*LGRC/S*) kwani kuna dalili za mianya mingi inayoruhusu ubadhirifu kwa njia za mtandao katika mashine za kukusanya mapato (*POS*).

Mheshimiwa Spika, pendelekezo hili linakusudia kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kudhibiti ulaghai wa kimtandao katika mapato hayo.

Mheshimiwa Spika, nne, kuhusu Tofauti za Mahitaji ya Mishahara katи ya Halmashauri na Hazina:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ndiyo zenyenye Kanzidata ya idadi halisi ya Watumishi waliopo katika maeneo yao;

Na kwa kuwa imebainika sasa kwamba kiasi cha mishahara kinachotolewa na Hazina katika baadhi ya Halmashauri ni kikubwa kuliko mahitaji halisi ya Halmashauri zenyewe;

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba Serikali ihuishe Mfumo wa Mishahara unaotumiwa na Hazina ili uwe na mawasiliano na Mfumo wa Mishahara unaotumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Lengo kubwa ni kupata kiasi sahihi cha mishahara inayopaswa kulipwa.

Aidha, Serikali ifanye uchunguzi wa sababu zillizopelekea tofauti hiyo ya mishahara katika Halmashauri mbalimbali ikiwemo zile za Mkoa wa Tabora kisha ichukue hatua kwa mujibu wa sheria. Pendekezo hili linakusudia kudhibiti kuibuka upya kwa hoja ya mishahara hewa.

Mheshimiwa Spika, tano, udhaifu katika Makusanyo ya Mapato ya Ndani:-

Kwa kuwa mapato ya ndani ya Halmashauri ni muhimu kwa ajili ya kutoa huduma na miradi mbalimbali;

Na kwa kuwa udhaifu katika ukusanyaji wa mapato hayo huathiri huduma na miradi hiyo;

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba Serikali itumie utaaliam wake kutathmini upya vyanzo mbalimbali vyatika Halmashauri nchini na namna vinyavoweza kutozwa kodi iliyo endelevu huku ikidhibiti upotevu wa mapato hayo kwa njia ya mifumo ya kisasa ya ukusanyaji na utumiaji wa mapato. Pendekezo hili linakusudia kuimarisha uwemo wa Halmashauri kifedha katika kutoa huduma ipasavyo kwa wananchi.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, sita, kuhusu 40% ya Miradi ya Maendeleo na 10% Uwezeshaji wa Makundi Maalum ya Kijamii:-

Kwa kuwa utaratibu wa kutenga fedha ya mapato ya ndani kwa kiasi cha 40% kwenda kwenye miradi ya maendeleo na 10% kwenda kwenye makundi maalum unakusudia kuboresha huduma za jamii na kuinua vipato vya makundi hayo;

Na kwa kuwa inapotokea kwamba utaratibu huo hautekelezwi, nia hiyo njema ya Serikali inakuwa hajatekelezwa;

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba Serikali iweke utaratibu madhubuti kuanzia katika ngazi ya Wizara; Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Sekretarieti za Mikoa na Mabaraza ya Madiwani kwa ajili ya kuhakikisha kuwa ruzuku hii inatolewa na kutumika ipasavyo kwa kila Halmashauri. Aidha, Vikundi vinavyokopeshwa vipewe fedha baada ya kubainisha ama kusaidiwa mawazo ya kibiashara yanayotekelzeza na kuleta faida badala ya kuzitoa fedha hizo ili mradi zimetolewa.

Mheshimiwa Spika, saba, kuhusu Zabuni za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutangazwa kabla ya kupata idhini ya Bodi za Zabuni:-

Kwa kuwa taratatibu za utangazaji wa zabuni mbalimbali katika taasisi za umma zipo kwa mujibu wa sheria za nchi kwa lengo la kuchochaea uwazi, tija na uwajibikaji kwa upande wa Watoa Zabuni na Wazabuni;

Na kwa kuwa imedhihirika kwamba katika baadhi ya halmashauri kumekuwepo na ukiukwaji wa taratibu hizo kiasi cha kuchochaea rushwa, ubadhirifu na ushindani usio na tija;

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba matangazo ya zabuni zote za Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaanchnini yazingatie matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya Umma. Kwa maana kwamba ni shurti yatolewe baada ya kupata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

idhini ya Bodi husika za Zabuni. Pendekezo hili linadhamiria kuchochea matumizi bora ya fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nane, kuhusu Utendaji wa Vitengo vya Udhhibitii wa Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa:-

Kwa kuwa utekelezaji wa dhana ya udhibiti wa ndani kwa njia za TEHAMA, Ugaguzi wa Ndani, Usimamizi wa Vihatarishi na Mifumo ya Kielektroniki ya kihasibu ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha utawala bora.

Na kwa kuwa imebainika kwamba dhana ya udhibiti wa Ndani haitekelezwi ipasavyo katika baadhi ya Mamlaka kiasi cha kuathiri utawala bora na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma,

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba Serikali isimike na kutumia ipasavyo mifumo ya udhibiti wa ndani hususani mifumo ya TEHAMA katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini. Usimikaji na matumizi ya mifumo hii viende sanjari na kutoa mafunzo kwa Watendaji husika kwa ajili ya kuimarisha uongozi huo.

Mheshimiwa Spika, tisa, kuhusu Upungufu wa Watumishi: Niende moja kwa moja mapendekezo, Serikali imeazimia vema kushughulikia masuala hayo;

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba kazi iendelee kwa Serikali kutumiza wajibu wake katika ajira na Stahiki za Watumishi.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili linakusudia kuisaidia Serikali iwe na idadi stahiki ya watumishi wenye ari ya kulitumikia Taifa kwa uzalendo, ufanisi na tija zaidi ya ilivyo sasa. Pendekezo hili litekelezwe sanjari na kuangalia muda ambao watumishi wanakaa katika kituo kimoja cha kazi ili kuwaondolea tabia ya kufanya kazi kwa mazoea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni, Bunge linaishauri:-

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(a) Serikali kuona uwezekano wa kushughulikia madeni hayo kwa kuingia katika mazungumzo na mabenki, ambapo Halmashauri za Jiji la Mbeya na Manispaa ya Temeke zilipata mikopo ambayo sasa imekuwa ni mzigo mzito katika uendeshaji wa Halmashauri. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, pasiwe na mamlaka ya Serikali ya Mitaa inayokwenda kukopa fedha bila ya Serikali Kuu kujiridhisha na andiko la mradi unaokusudiwa kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mali chakavu: -

Kwa kuwa, ni dhahiri kwamba katika Halmashauri nyingi nchini kuna mlundikano wa magari chakavu yanayotakiwa kuuzwa au kutengenezwa ili yaweze kutumika;

Na kwa kuwa, kuendelea kuwepo kwa magari hayo ni hasara zaidi kwa Serikali na ni uharibifu wa mazingira;

Kwa hiyo basi, Bunge linaishauri Serikali kuweka wazi Mwongozo wa Uondoaji wa Mali chakavu katika Taasisi za Umma na kuendesha zoezi kabambe la kuondoa wa gari chakavu katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, nakushukuru sana kwa uongozi wako uliotuwezesha kukamilisha vyema taarifa ya mwaka ya Kamati. Tunatumai utatuongoza vyema zaidi katika kukamilisha uchambuzi wa Taarifa ya CAGya Mwaka 2020/2021 mara itakapowasilishwa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, tunaipongeza sana Sekretarieti ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi, ndc, kwa uratibu makini wa shughuli za Kamati. Sekretarieti ya Bunge imetusaidia sana katika utafiti, mawasiliano na ushauri katika masuala mbalimbali ya Kamati. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Bw. Athumani Hussein, *ndc*, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi katika Sehemu ya Fedha na Uchumi Ndugu Dickson M. Bisile ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya *LAAC* akisaidiana na Ndugu Wilfred Magova na Ndugu Paul Chima. Wametekeleza wajibu wao ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Watendaji wa Serikali, hususan Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (*CAG*), Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao, kila wakati tulipohitaji ufanuzi wa hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa dharti kabisa, naomba kumshukuru Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Zedi na Wajumbe wote 24 wa Kamati ya *LAAC* kwa uvumilivu, ushirikiano na uchapakazi. Mwenyezi Mungu awabariki sana. Majina yao yako kwenye taarifa kuu, naomba yarekodiwe vyema kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mwisho, msingi wa maoni na mapendekozo yaliyotolewa katika taarifa hii ni hoja za ukaguzi wa *CAG* kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na majibu ya baadhi ya Maafisa Masuuli waliohusika katika mahojiano na Kamati. Mapendekozo haya yanakusudia kuimarisha nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inafarijika kuona kuwa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa panakuwepo na nidhamu katika mapato na matumizi ya fedha za umma Serikalini. Hatua alizochukua hivi karibuni za kutengua teuzi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Jiji la Mbeya, Manispaa ya Iringa, Manispaa ya Singida na Wilaya ya Buchosa ni kiashiria cha kuchukia ubadhirifu wa fedha za umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuiafiki Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30, Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi/Vigelegele*)

**TAARIFA YA MWAKA KUHUSU TAARIFA YA MDHIBITI NA
MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA HESABU
ZILIZOKAGULIWA ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA
MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2020 –
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni
za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]*

SEHEMU YA KWANZA

1.0 MAELEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, tarehe 08 Aprili, 2021 Serikali iliwasilisha Bungeni Taarifa mbalimbali za Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2020. Taarifa hizo zinapaswa kujadiliwa na Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia matumizi ya fedha za umma ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

Hivyo, chini ya Kanuni ya 136 (15), Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya LAAC kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini za mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2020.

Kabla ya kuwasilisha Taarifa hii, naomba nitoe pongozi zangu kwako kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania. Sifa zako kitaaluma, uzoefu na ufanisi katika uongozi zimetukuka sana. Aidha, nina mpongeza Mhe. Azzan Mussa Zungu kwa kuchaguliwa kuwa

Naibu Spika wa Bunge. Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema na uongozi bora.

Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Nape Mosses Nnauye (Mb) aliyekuwa Mjumbe wa Kamati hii kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kamati inamtakia kila lenye heri katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu.

Sehemu ya Kwanza inayoelezea shughuli zilizotekelawa na Kamati kwa mwaka 2021, mbinu zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati, wadau walioshirikishwa na nyaraka zilizotumika. **Sehemu ya Pili** inabainisha matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya CAG (2019/2020) na Mahojiano na Afisa Masuuli vikaoni na ziarani. **Sehemu ya Tatu** inaelezea Maoni na Mapendekezo ya Kamati katika Hoja Mahsusizi zinazohusu maeneo yenye mwenendo usioridhisha wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

1.1 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI KATIKA MWAKA 2021/22

(a) Mahojiano na Maafisa Masuuli wa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu Hoja za Ukaguzi zilizo katika Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) Ziara za Ukaguzi wa Ufanisi katika Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri za Wilaya ya Kilolo, Chemba, Mpwapwa, Chamwino, Mvomero, Manispaa za Singida, Ubungo na Kinondoni; Manispaa ya Kigamboni na Jiji la Dodoma;

(c) Semina na Warsha Mbalimbali chini ya Ofisi ya Bunge kuititia Mradi wa Kuliwezesha Bunge (*Legislative Support Project II*) na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(d) Majadiliano na tathmini mionganini mwa Wajumbe wa Kamati kuhusiana na shughuli zilizotekelezwa.

1.2 MBINU ZILIZOTUMIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YA KAMATI

- (a) Mahojiano na Maafisa Masuuli kuhusu Hoja za Ukaguzi;
- (b) Ziara za Ukaguzi wa Ufanisi katika miradi ya Maendeleo;
- (c) Warsha na Semina kuhusu Majukumu ya Kamati;
- (d) Kupokea Maoni ya Wadau;
- (e) Uenezi wa Shughuli za Kamati kuititia Program za Elimu kwa Umma; na
- (f) Tafiti mbalimbali kuhusu Uendeshaji wa Serikali za Mitaa Duniani.

1.3 WADAU WALIOSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KAMATI

- (a) Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi;
- (b) Baadhi ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
- (c) Ofisi ya Rais- TAMISEMI;
- (d) Wizara ya Fedha;
- (e) Mabaraza ya Madiwani;
- (f) Asasi za Kiraia;
- (g) Vyombo vya Habari; na
- (h) Wananchi kwa Ujumla.

1.4 NYARAKA ZINAZOTUMIKA

- (a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- (b) Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2019/20);
- (c) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008;
- (d) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290;
- (e) Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2011;
- (f) Sheria ya Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura 296;
- (g) Sheria ya Bajeti, Sura 439;
- (h) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;
- (i) Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu; na
- (j) Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa, 2019.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI NA MATOKEO YA ZIARA NA MAJADILIANO

Katika mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya Halmashauri 185 zilikaguliwa na CAG. Kati ya Halmashauri hizo, 124 sawa na 67% zilipata Hati Safi za Ukaguzi, Halmashauri 53 sawa na 29 % zilipata Hati zenye Mashaka, na Halmashauri 8 sawa na 4% zilipata Hati Mbaya. Kwa ajili ya Taarifa hii, LAAC imeweza kuhoji jumla ya Halmashauri 40 sawa na 21.6% ya Halmashauri zote zilizokaguliwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Jedwali Na.1 Mwenendo wa aina za Hati za Ukaguzi 2015/16- 2019/2020

Mwaka wa Fedha	Hati Inayoridisha	Hati zenyeye Shaka	Hati Mbaya	Bila Hati
2019/20	124	53	8	0
2018/19	176	9	0	0
2017/18	176	7	1	1
2016/17	166	16	3	0
2015/16	138	32	1	0

Chanzo: *Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 2019/2020*

Takwimu hizi zina ashiria uthabiti katika nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Idadi ya Hati Safi za Ukaguzi ni zaidi ya 50%. Aidha, takwimu hizi zinaweza kutafsiriwa kwamba kuwa kuna uimara katika utendaji wa tasisi za usimamizi wa fedha za umma kama vile Bunge, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, TAKUKURU, Mabaraza ya Madiwani, Asasi za Kiraia, Vyombo vya Habari na Wananchi kwa ujumla.

Kuendelea kuwepo kwa idadi ya hati zenyeye mashaka na hati mbaya kunaashiria kuwa, bado yapo maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kutookana na sababu mbalimbali. Mionganoni mwa sababu hizo ni udhaifu katika usimamizi wa rasilimali watu na fedha ndani ya Halmshauri zenyewe, uelewa na uzoefu mdogo katika kuandaa taarifa za hesabu na tabia za kibadhirifu kwa ujumla mionganoni mwa watumishi.

2.1 UCHAMBUZI WA MAENEKO YENYE CHANGAMOTO KATIKA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA KATIKA HALMASHAURI

Mheshimiwa Spika, pamoja na maoni ya jumla ya Kamati kwamba Mwenendo wa sasa wa mapato na matumizi ya fedha za umma unazidi kuimarika, bado yapo maeneo yenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

changamoto. Taarifa hii imebainisha maeneo hayo na namna yanavyoathiri mapato na matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Kwamfano; Kamati imebaini kwamba:

2.1.1 Ruzuku ya Maendeleo Haipelekwi ipasavyo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 12 na 13 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 na Sheria ya Fedha katika kila Bajeti ya Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zinapaswa kupewa fedha za ruzuku ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka katika Serikali Kuu.

Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Majibu ya Mamlaka za Serikali za Serikali za Mitaa unaonesha kuwa ruzuku hiyo haipelekwi ipasavyo. Baadhi ya Halmashauri hupelekewa kiasi kidogo zaidi cha fedha za miradi ya maendeleo ikilinganishwa na kiasi halisi kilichoidhinishwa na Bunge wakati Halmashauri zingine hupelekewa fedha zaidi. Aidha, baadhi ya miradi hupelekewa fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha hivyo kuzifanya zishindwe kutekeleza miradi hiyo katika mwaka husika.

Jedwali Na. 2 Mwenendo wa Upatikanaji wa Ruzuku ya Maendeleo

Mwaka	Bajeti Idhinishwa na Bunge	Kiasi halisi klichotolewa na Serikali	Pungufu	%	Idadi ya Halmashauri zilizoathirika
2019/20	890.3 Bil	479. 9 Bil	410. 4 Bil	46	152
2018/19	1.2 tril	628. 6 Bil	556. 8 Bil	47	157
2017/18	977.2 Bil	497. 3 Bil	480.01 Bil	49	156
2016/17	1.03 tril	501. 9 Bil	532. 2 Bil	51	167
2015/16	1.01 tril	390. 5 Bil	620. 1 Bil	61	151

Chanzo: Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 2019/20

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyoelezwa hapo juu ina chochea matumizi mabaya ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Kwa mfano, fedha pungufu zinazotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi huingizwa katika utekelezaji wa miradi kwa hatua za awali tu kisha kuacha miradi hiyo ikae kwa muda mrefu bila kukamilishwa. Katika maeneo mengine miradi husika hutelekezwa kabisa kwa kukosa fedha za kuikamilisha. Mfano mzuri ni Ujenzi wa Ukumbi wa Hamashauri ya Wilaya ya Mpwapwa Mkoani Dodoma ulioanza mwaka mwaka 2012/13 kwa kutumia fedha za *Local Government Capital Development Grant* (LGCDG) wakati huo. Mpaka sasa mradi huo upo kama gofu tu kwa sababu ya kukosa fedha za kukamilisha.

2.1.2 Kuna Matumizi ya “fedha mbichi” kwa namna yenye kukwepa kubainika katika mifumo ya kielektroniki ya mapato (LGRCIS) na matumizi (EPICOR/ MUSE).

Mheshimiwa Spika, hapa tunazungumzia mapato yaliyokusanywa lakini hayakupelekwa benki. Utaratibu ni kwamba Serikali kuu imeweka mifumo ya LGRCIS na EPICOR/ MUSE kwa ajili ya kurekodi na kudhibiti mapato na matumizi. Aidha, taarifa zinazotokana na mifumo hii husaidia katika kuandaa hesabu jumuifu za Halmashauri husika mwishoni mwa mwaka wa fedha. Fedha zinapotumika kabla ya kupelekwa benki (fedha mbichi) zinakuwa hazijarekodiwa kama zilikusanywa na kutumika mwishoni mwa mwaka husika wa fedha.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, jumla ya Shilingi bilioni 18.769 zilizokusanywa katika Halmashauri mbalimbali zilitumika kabla ya kupelekwa benki katika mwaka wa fedha 2019/20. Baadhi ya Halmashauri zilizobainika katika hoja hii na kiasi chake cha fedha kwenye mabano ni: Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua (Tsh. 183.2 milioni), Uyui (383.4 milioni), Manispaa ya Temeke (344 milioni), Siha (112.5 milioni), Itilima (54.9 milioni), na Chalinze (25.2 milioni). Hii ni mifano michache tu iliyotolewa

kwa lengo la kuthibitisha kwamba tatizo hili lipo na linahitaji ufumbuzi.

2.1.3 Baadhi ya Halmashauri hufuta Miamala ya Mapato bila ya kuwepo kwa Uthibitisho kwamba Miamala hiyo haikuwa sahihi

Mheshimiwa Spika, utaratibu ni kwamba Mfumo wa Kielektroniki wa LGRCIS ndiyo unaopokea miamala kutoka kwa wakusanyaji mbalimbali. Ofisi ya Rais TAMISEMI ndiyo Wahifadhi Wakuu wa Mfumo huu. Hata hivyo, Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amebaini na Kamati imethibitisha kuwa katika baadhi ya Halmashauri, miamala ya makusanyo hufutwa au hurekebishwa bila ya kuwapo kwa uthibitisho kwamba miamala hiyo kweli ilikosewa. Katika Mwaka wa Fedha 2019/20, jumla ya Shilingi bilioni 4.5 zilifutwa kwenye mfumo kwa utaratibu huu ambao Kamati haikubali.

Baadhi ya Halmashauri zinazohusika katika hoja hii na kiasi cha fedha kilichofutwa bila uthibitisho ni: Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru (bilioni 1.2), Halmashauri ya Wilaya ya Siha (milioni 624.2), Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu (Milioni 497.9), Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi (milioni 320) na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale (milioni 258.7). Hapa tunataja mifano michache tu kuthibitisha kwamba tatizo lipo na Serikali ichukue hatua za udhibiti katika Mfumo na Maadili.

2.1.4 Kiasi cha mishahara kutoka HAZINA (Exchequer Release) kutofautiana na mahitaji halisi ya mishahara katika Mfumo wa LAWSON.

Mheshimiwa Spika, hoja hii ina viashiria vya kuibuka tena kwa mishahara hewa Serikalini. Kuna ushahidi kwamba kiasi cha mishahara kinachotolewa na HAZINA huwa ni kikubwa kuliko kile kinachotakiwa katika Halmashauri. Kwa mfano:

- (a) Halmashauri ya Wilaya ya Urambo mahitaji ya LAWSON ilikuwa ni Tsh. 13, 162, 727, 251 lakini HAZINA ilitoa Tsh. 13, 308, 458, 790 hivyo kusababisha ziada ya Tsh. 145, 731, 539.

(b) Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua Mahitaji ya LAWSON yalikuwa ni Tsh. 17, 679, 189, 899 lakini HAZINA ilipeleka Tsh. 17, 889, 094, 180 hivyo kuwa na ziada ya Tsh. 209, 902, 281.

(c) Halmashauri ya Wilaya ya Uyui mahitaji ya LAWSON yalikuwa Tsh. 17, 061, 985, 326 lakini HAZINA ilipeleka Tsh. 17, 371, 325, 530 hivyo kuwa na ziada ya Tsh. 309, 340, 200.

Mheshimiwa Spika, hoja hii inaashiria kwamba Serikalini kuna usimamizi hafifu wa mfumo wa mishahara. Udhaifu huu usipodhibitiwa utaibua upya mishahara hewa Serikalini.

2.1.5 Udhaifu katika kukusanya mapato ya ndani.

Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zina udhaifu mkubwa sana katika kukusanya mapato ya ndani. Hali hii imezifanya Mamlaka hizo kuwa na utegemezi mkubwa katika ruzuku ya Serikali kuu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi. Miongoni mwa sababu zinachongia udhaifu huu ni:-

(a) Tathimini duni fursa za kiuchumi katika maeneo ya Halmashauri.

Halmashauri nyingi nchini bado hazijafanya tathimini ya kina ya fursa za kiuchumi zilizopo katika maeneo yao kwa ajili ya kujipatia kipato. Baadhi ya fursa hizo ni upimaji na umilikishaji wa ardhi kwa wananchi, usambazaji wa huduma muhimu za kijamii kama vile maji na umeme kwa ajili ya kuvutia umiliki na ukazi katika maeneo hayo, utengenezaji wa maeneo ya mapumziko na biashara, matangazo ya vivutio asilia, nk.

(b) Uandaaji na usimamizi mbovu wa mikataba mbalimbali.

Kwa makusudi au kwa kukosa utaalami wa masuala ya kisheria, Halmashauri nyingi nchini zinapoteza mapato kutoka na udhaifu wa masharti katika mikataba yao na Wadau mbalimbali. Kwa mfano katika Mwaka 2019/2020: Halmashauri ya Korogwe imekosa takribani shilingi 187.3 milioni kutokana na ushuru wa zao la chai na shilingi 382.8

milioni za ushuru wa zao la katani kutokana na udhaifu katika masharti ya makubaliano na mikataba kati yake na Makampuni yallyokuwa yakifanya biashara ya mazao hayo. Aidha, Halmashauri mbalimbali nchini zimekuwa zikikosa Ushuru wa Huduma (Service levy) kutoka kwenye Makampuni mbalimbali yanaendesha shughuli katika maeneo yao kwa sababu tu Ofisi za Makampuni hayo ziko nje ya Halmashauri hizo. Hali hii imekuwa kikwazo katika mapato ya ndani ya Halmashauri za Wilaya za Mkuranga, Chalinze na Rufiji.

(c) Tathmini isiyosahihi ya uhimilivu wa baadhi ya vyanzo vya mapato kutozwa kodi ya viwango vya juu.

Halmashauri mbalimbali zimeanzisha ama zipo kwenye maeneo ya uwekezaji kama vile misitu na vibanda vya biashara kwenye maeneo ya masoko. LAAC imebaini kwamba kutokuwepo kwa tathmini ya kina ya unyumbuwa wa kiuchumi (economic elasticity) wa vyanzo hivyo kwa ajili ya tozo na ushuru unaostahili. Kwa mfano; Manispaa ya Songea ilikusanya ushuru wa huduma (service levy) kiasi cha 363.7 milioni bila hata kuja kiasi cha faida ambacho Makampuni yaliyohudumiwa yalipata kwa mwaka (turnover) kama ilivyokusanya halmashauri ya Wilaya ya Itilima kiasi cha shilingi 76.3 milion kutoka kwa TAWA.

Aidha, baadhi ya Halmashauri zilizowekeza kwenye vibanda vilivyoko kwenye masoko ya kawaida na masoko ya kimkakati, zimekuwa zikipangisha vibanda hivyo kwa bei kubwa kiasi cha kuwatisha wafanya biashara wadogo wadogo kufanya biashara katika vibanda hivyo kwa maana kuwa faida watakayopata haiendani na gharama za upangaji. Kutokana na mazingira kama hayo, miradi mingi ya namna hii hukaa muda mrefu bila kuwa na wapangaji hivyo kuzinyima halmashauri husika mapato.

(d) Hujuma katika mashine za kukusanya mapato (Pos).

Mashine hizi hutumika katika miamala ya biashara mbalimbali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Vipo viashiria kwamba POS hizi zinahujumiwa na watendaji ama mawakala wasio

waaminifu hivyo kuikosesha Serikali mapato stahiki. Kwa mfano:

i. Katika baadhi ya halmashauri, miamala ya biashara zilizofanyika imekuwa ikirekebishwa kiufundi kwenye Mfumo Mama wa Mapato wa LGRCIS bila kuwepo kwa vielelezo vyta marekebisheso yanayo fanyika kutoka kwenye POS iliyokusanya mapato hayo. Katika mwaka 2019/2020, jumla ya Halmashauri 35 (**Kielelezo Na.2**) zilifanya marekebisheso ya aina hii yenye jumla ya Shilingi **bilioni 4.8**.

Kufuta miamala hii bila ya kuwepo kwa vielelezo muhimu vyta kuthibitisha ufutaji huo ni kinyume cha matakwa ya Agizo Na. 37 (6) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 2019. Agizo hili linalekeza kuwa risiti ya mapato iliyofutwa kutokana na makosa katika PoS kutokana na makosa mbalimbali inapaswa kutunzwa kwa ajili ya kuthibitisha marekebisheso kwenye Mfumo Mama.

ii. Katika baadhi ya Halmashauri mashine za POS huzimwa kwa muda mrefu hivyo kutokuwa na mawasiliano na Mfumo wa LGRCIS. Katika mwaka wa fedha 2019/20, POS 613 katika halmashauri 19 (**Kielelezo Na.3**) zilikuwa hazitumiki na zingine zilikuwa hazisomeki kwenye Mtandao.

iii. Katika Halmashauri zingine, tarehe za miamala katika PoS hurekebishwa kwa ufundi ili kudanganya wakati halisi ambao makusanyo yalifanyika. Kwa mfano, katika Manispaa ya Sumbawanga, risiti zilizotolewa na PoS zilionesha kwamba kiasi cha shilingi 9,974,650 kilikusanywa tarehe 01 Julai, 2009 wakati mfumo wa matumizi ya PoS ulianza mwaka 2015/2016.

iv. Katika baadhi ya Halmashauri Miamala ya Mapato kutoka kwa Wakusanya mapato haiwasilishwi kwa Waweka HAZINA wa Halmashauri. Kwa mujibu wa utafiti wa Taasisi ya WAJIBU, kiasi cha Tsh. 35.9 bilioni kilichokuwa kimekusanywa na mawakala katika Halmashauri 67 hakikurejeshwa katika HAZINA za Halmashauri.

(e) Udhaifu katika kusimamia marejesho ya NHIF

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za afya nchini, upo utaratibu kwamba wanufaika wa bima ya afya chini ya NHIF hupata matibabu katika hospitali, zahanati na vituo vya afya viivyo chini ya Halmashauri. Baada ya matibabu, Halmashauri zinapaswa kudai gharama kwa NHIF.

Mara nydingi NHIF hugoma kufanya marejesho ya gharama hizo kwa madai kwamba wanufaika hawakujaza form ipasavyo. Halmashauri ndizo zinazopata hasara ya kutorejeshewa gharama hizo. Hoja hii inazidi kukua kwa sababu kila Halmashauri iliyofika mbele ya Kamati inakabiliwa na hasara hii mnufaika akiwa ni NHIF.

Mifano ya Halmashauri hizo kwa mujibu wa Taarifa ya CAG ni Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto (25.3 mil), Halmashauri ya Wilaya ya Magu (90.0 Mil), Halmashauri ya Mji wa Mwanga (95.7 mil), Halmashuari ya Mji wa Korogwe (68.0 mil), Halmashauri ya Mji wa Mafinga (68.0 mil), Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru (84.8 mil), Halmashauri ya Manispaa ya Temeke (75.6 mil) na Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo (701m).

(f) Udhaifu katika utendaji wa Vitengo vya Udhibiti wa Ndani.

Mheshimiwa Spika, wajibu mkuu wa Vitengo vya Udhibiti wa Ndani katika taasisi ni kuimarisha ufanisi katika utendaji na matumizi ya fedha za umma. Vitengo hivi vinatekeleza jukumu hili kwa kutoa tahadhari za mapema dhidi ya mwenendo usiofaa katika utendaji au masuala ya fedha.

Kamati imebaini kuwa Halmashauri nydingi zina changamoto ya ufanisi katika utendaji wa Vitengo hivi. Udhaifu wa Vitengo hivi unatokana na sababu mbalimbali kama vile idadi ndogo ya watumishi, uhaba wa vitendea kazi na fedha kwa ujumla au kukosa mafunzo ya mara kwa mara yanyohusiana na ukaguzi. Matokeo yake ni kwamba kunakuwa na udhaifu pia katika ufanisi wa rasilimali watu kwa ujumla, mrundikano wa hoja za ukaguzi na kushamiri kwa vihatarishi mahali pa kazi.

(g) Kulegalega kwa motisha ya Serikali kwa Watendaji.

Raslimali watu ndiyo inayopanga, hutafsiri, huratibu na kutekeleza mipango ya fedha na maendeleo katika taasisi zetu. Hivyo, kila wakati rasilimali hii inatakiwa kuwekwa katika ubora unaostahili kimafunzo na maslahi. Pale watumishi wanapokosa mafunzo ya mara kwa mara kuhusiana na majukumu yao, wanapokosa kupandishwa vyeo kwa wakati kwa mujibu wa sheria au wanapokaimu kwa muda mrefu bila kujuu hatma yao huwa wana kosa morali wa kazi ikiwemo kukusanya na kutumia vizuri mapato ya Serikali.

2.1.6 Baadhi ya Halmashauri Hazipeleki kikamilifu 40% ya Fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Uandaaji wa Bajeti ya Serikali wa Mwaka 2019/2020 na Mwaka 2021/22 unazitaka Halmashauri nchini kutenga 40% ya mapato yao ya ndani (yasiyolindwa) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Utaratibu huu unakusudia kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kama vile elimu, afya, mawasiliano na maji katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba utaratibu huu hautekelezwi ipasavyo kwani Halmashauri nyingi hazipeleki fedha hizo hivyo kuathiri nia iliyokusudiwa.

2.1.7 Baadhi ya Halmashauri hazipeleki kikamilifu 10% ya Mapato ya Ndani katika Miradi ya Makundi Maalum

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 37 (A) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, kinazitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kutenga 10% ya mapato yao ya ndani (yasiyolindwa) kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu kwa uwiano wa asilimia 4:4:2 mtawalia. Madhumuni ya kutenga asilimia hizo ni kuviwezesha Vikundi hivyo vijkwamue kiuchumi.

Kamati imebaini changmoto mbili katika eneo hili. kwanza Halmashauri zilizo nyingi hazitekelezi kikamilifu utaratibu huu.

Pili, hata pale fedha zinapotolewa kwa Vikundi, hakuna upembuzi yakinifu wa maandiko ya biashara (Business plans) yanayoenda kutekelezwa na Vikundi hivyo. Madhara yake ni kwamba fedha zinatolewa hazirejeshwi kwenye Mfuko kwa sababu biashara zinazoenda kutekelezwa siyo endelevu. Kwa kufanya hivyo, madhumuni ya Serikali kuweka utaratibu huu kwa mujibu wa Sheria yanapotea kabisa.

2.1.8 Madeni Makubwa ya Baadhi ya Halmshauri kutokana na Mikopo ya Mabenki na Madai ya Watumishi

Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (1982), mikopo ni mionganini mwa vyanzo vya mapato ya Halmashauri. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya Halmashauri kama vile Halmashauri ya Jiji la Mbeya ina daiwa na Benki ya CRDB takribani Shilingi 29 bilioni ikiwa ni mkopo, riba na adhabu.

Jiji la mbeya liliropa fedha hizi kwa ajili ya kujenga Soko Kuu la Mwanjelwa kwa dhamana ya Serikali Kuu. Mfano mwingine ni Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ambayo pia ina madeni makubwa ya aina hii. Mikopo hii sasa imegeuka kuwa mzigo mzito usioweza kuvutwa tena na Halmashauri hizo.

Aidha, zipo dalili za Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutumbukia katika mikopo ya aina hii endapo tahadhali hazitachukuliwa katika kukamilisha Jengo la Kitega Uchumi chake katika Mji wa Mtumba. Ukamilishaji wa Kitega Uchumi hicho unakadirisha kutumia Shilingi bilioni 59 ikiwa ni mapato ya ndani. Mpaka sasa kiasi kilicholipwa ni shilingi bilioni 18. Sehemu kubwa ya mapato ya ndani yanayotegemewa yanatokana na mauzo ya viwanja.

2.1.9 Malipo ya Kazi na Huduma mbalimbali kutolewa kabla ya Kuhakiki Ubora wa Kazi au Huduma

Kifungu cha 243 (2) (3) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma (2013) kinataka malipo ya kazi na huduma yafanyike baada ya taasisi nunuzi kujiridhisha na kiwango au ukubwa wa kazi au huduma iliyo tolewa. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba

utaratibu huu mara nyingi hauzingatiwi hivyo kuathiri ubora wa kazi na huduma. Kwa mfano, katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilimlipa Mkandarasi kiasi cha shilingi milioni 72 bila ya kuwepo kwa uhakiki wa kazi iliyo fanyika. Halmashauri hii imetumiwa kama mfano kuthibitisha kwamba tatizo lipo na Serikali ichukue hatua.

2.1.10 Zabuni za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutangazwa Kabla ya kupata Idhini ya Bodi za Zabuni.

Kanuni ya 185 (1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (2013), imeweka sharti kwamba zabuni za manunuzi mbalimbali zinapaswa kutangazwa baada ya nyaraka za zabuni husika kujadiliwa na kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni ya taasisi husika. Madhumuni ya kuwepo kwa Kanuni hii ni kuhakikisha kuwa mchakato wa zabuni unakuwa wa wazi, ushindani, tija na wenye kuwezesha uwajibikaji kwa wanunuzi na wazabuni wenyewe.

Katika baadhi ya Halmashauri zabuni mbalimbali hutangazwa kabla ya nyaraka zake kujadiliwa na kuidhinishwa na Bodi hizo. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, zabuni mbalimbali zenyе thamani ya shilingi bilioni 6.9 zilitangazwa bila kufuata utaratibu huu katika Halmashauri za Wilaya za Kalambo, Bukombe, Ikungi, Lushoto na Mkuranga. Hii ina maana kwamba Wazabuni walipata kazi hizo bila idhini ya Bodi za Zabuni katika Halmashauri husika.

Kamati ina maoni kwamba utaratibu huu uliwekwa kwa mujibu wa Sheria kwa ajili ya kuimarisha uwazi na ushindani wenye tija kwa mtoa zabuni na mnunuzi. Kukwepa utaratibu huo kunasababisha ukosefu wa uwazi na ushindani katika matumizi ya fedha za umma hivyo kuchochaea upendeleo na rushwa.

2.1.11 Kuwepo kwa mali nyingi chakavu (magari) katika Halmashauri

Mhesimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba katika Halmashauri mbalimbali nchini kuna mrundikano mkubwa wa

magari yaliyochakaa. Uchakavu wa gari hizo umeendelea kuwa hasara kwa Serikali kutockana na kwamba haziondolewi kwa wakati zinapokuwa zimechoka. Hoja hii inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kutoeleweka vema kwa utaratibu wa kuza mali hizo zinapokuwa zimechakaa.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA HOJA ZILIZOCHAMBULIWA

3.1 Ruzuku ya fedha za maendeleo katika Halmashauri kutopelekwa ipasavyo

KWAKUWA LAAC imetoa ushahidi usio na shaka kwamba ruzuku ya fedha za maendeleo haipelekwi ipasavyo katika Halmashauri. Zipo Halmashauri zinazopelekewa fedha nyingi kuliko kiasi kilicho ombwa, zingine zinapelekewa fedha pungufu na kwa kuchelewa au fedha hutumwa na kurejeshwa HAZINA bila maelezo,

NA KWAKUWA vitendo vilivyoelezwa hapo juu vinaathiri utekelezaji wa mipango ya Mamlaka husika katika kuboresha huduma za jamii,

KWAHIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali iwe na uhalisia katika kuandaa bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa na ipeleke fedha za maendeleo katika Mamlaka hizo kwa kuzingatia Sheria ya Matumizi inayotungwa na Bunge kila mwaka ili Mamlaka hizo ziweze kutekeleza ipasavyo miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu unakusudia kuihimiza Serikali kuongeza juhudni katika kubuni vyanzo thabiti vya mapato, kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato na kupeleka ipasavyo fedha zinazokusanywa ili zikaboreshe maisha ya Wananchi kwa wakati.

3.2 Matumizi ya “fedha mbichi” kwa namna yenyewe kukwepa kubainika katika mifumo ya kielektroniki ya mapato (LGRCIS) na matumizi (EPICOR/ MUSE).

KWAKUWA mifumo ya kielektroniki ya mapato na matumizi ya fedha za umma imewekwa na Serikali kwa ajili ya kuimarisha nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya fedha za umma nchini,

NA KWAKUWA, dhamira ya Serikali kuweka mifumo hiyo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za kijamii kwa wakati,

KWAHIYO BASI, Bunge linaielekeza Serikali kwamba ni marufuku kutumia fedha mbichi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Watendaji wote watakaobainika kutokutii agizo hili walichukuliwe hatua kali kwa mujibu wa Sheria za nchi. Pendeleko hili lina kusudia kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika kukusanya na kutumia fedha za umma.

3.3 Kufutwa kwa Miamala ya Mapato katika Mifumo ya Kielektroniki bila ya Uthibitisho.

KWAKUWA Mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato iliwekwa kwa ajili ya kusaidia ufanisi katika kukusanya na kutunza kumbukumbu za mapato,

NA KWAKUWA imebainika kwamba kuna ujanja unaofanyika katika mifumo hiyo hivyo kuathiri nia hii njema ya Serikali,

KWA HIYO BASI Bunge linaitaka Serikali:

(a) Ihakikishe kuwa mamlaka ya kurekebisha ama kufuta miamala kwenye mfumo wa mapato inabaki kwa Afisa Masuuli tu baada ya kujiridhisha na nyaraka halisi za mapendekezo ya kufanya hivyo.

(b) kuimarisha ubora wa risiti za kielektroniki zinazotolewa na mashine za kukusanya mapato nchini ili ziwe na maandishi yanayosomeka vema na yasiyofutika kirahisi kwa lengo la kutunza kumbukumbu za miamala; na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(c) kuimarisha usalama na udhibiti wa miamala katika mfumo wa mapato (LGRCIS) kwani kuna dalili za mianya mingi inayoruhusu ubadhirifu kwa njia za mtandao katika mashine za kukusanya mapato hayo maarufu kwa jina la POS.

Mheshimiwa Spika, Pendekazo hili linakusudia kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kudhibiti ulaghai wa kimtandao katika mapato hayo.

3.4 Tofauti za Mahitaji ya Mishahara kati ya Halmashauri na HAZINA

KWAKUWA Mamlaka za Serikali za Mitaa ndiyo zenye Kanzi data ya Idadi halisi ya Watumishi waliopo katika maeneo yao,

NA KWAKUWA imebainika sasa kwamba kiasi cha mishahara kinachotolewa na HAZINA katika baadhi ya Halmashauri ni kikubwa kuliko mahitaji halisi ya Halmashauri zenyewe,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba Serikali ihuishe ikama za Watumishi wa Halmashauri na ihakikishe kuwa Mfumo wa Mishahara unaotumiwa na HAZINA uwa na mawasiliano na Mfumo wa Mishahara unaotumiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini ili kupata kiasi sahihi cha mishahara inayopaswa kulipwa. Pendekazo hili linakusudia kudhibiti kuibuka upya kwa hoja ya mishahara hewa Serikalini na kuleta hasara bila sababu za msingi.

3.5 Udhafu katika Makusanyo ya Mapato ya Ndani

KWAKUWA mapato ya ndani ya Halmashauri ni muhimu kwa ajili ya kutoa huduma na miradi mbalimbali ya kijamii,

NA KWAKUWA udhaifu katika ukusanyaji wa mapato hayo huathiri huduma na miradi hiyo,

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Serikali itumie utaalami wake kutathmini upya vyanzo mbalimbali vya mapato katika Halmashauri nchini na namna vinavyoweza

kutozwa kodi iliyoendelevu huku ikidhibiti upotevu wa mapato hayo kwa njia ya mifumo ya kiasasa ya ukusanyaji na utumiaji wa mapato. Pendekazo hili linakusudia kuimarisha uwezo wa Halmashauri kifedha katika kutoa huduma ipasavyo kwa wananchi.

3.6 Kutopeleka 30% ya Miradi ya Maendeleo na 10% Uwezeshaji wa Makundi Maalum ya Kijamii.

KWAKUWA, utaratibu wa kutenga fedha ya mapato ya ndani kwa kiasi cha 30% kwenda kwenye miradi ya maendeleo na 10% kwenda kwenye makundi maalum unakusudia kuboresha huduma za jamii na kuinua vipato vyta makundi hayo,

NAWKWAKUWA inapotokea kwamba utaratibu huo hautekelezwi, nia hiyo njema ya Serikali inakuwa hajatekelezwa,

KWAHIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Serikali iweke utaratibu madhubuti kuanzia katika ngazi ya Wizara (ORTAMISEMI), Sekretarieti za Mikoa na Mabaraza ya Madiwani kwa ajili ya kuhakikisha kuwa ruzuku hii inatolewa na kutumika ipasavyo kwa kila Halmashauri.

Aidha, Vikundi vinyoyokopeshwa vipewe fedha baada ya kubainisha ama kusaidiwa mawazo ya kibashara yanayotekelozeka na kuleta faida badala ya kuzitoa fedha hizo ili mradi zimetolewa.

3.7 Zabuni za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kutangazwa Kabla ya kupata Idhini ya Bodi za Zabuni.

KWAKUWA taratatibu za utangazaji wa zabuni mbalimbali katika taasisi za umma zipo kwa mujibu wa sheria za nchi kwa lengo la kuchochera uwazi, tija na uwajibikaji kwa upande wa Watoa Zabuni na Wazabuni,

KWAKUWA imedhihirika kwamba katika baadhi ya Halmashauri kumekuwepo na ukiukwaji wa taratibu hizo kiasi cha kuchochera rushwa, ubadhirifu na ushindani usio na tija,

KWAHIYO BASI Bunge linaazimia kwamba matangazo ya zabuni zote za Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini yazingatie matakwa ya Sheria ya Manunuzi ya umma. Kwa maana kwamba ni shurti yatolewe baada ya kupata idhini ya Bodi husika za Zabuni. Pendekeso hili linadhamiria kuchochaea matumizi bora ya fedha za umma katika mazingira ya uwazi, ushindani, tija na uwajibikaji katika michakato ya zabuni hizo.

3.8 Udhafu katika Utendaji wa Vitengo vya Udhibiti wa Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

KWAKUWA utekelezaji wa dhana ya *udhibiti wa ndani* kwa njia za TEHAMA, Ukaruzi wa Ndani, Usimamizi wa Vihatarishi na, Mifumo ya Kielektroniki ya kihasibu ni muhimu kwa ajili ya kuimarisha utawala bora na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika taasisi za umma nchini,

NA KWAKUWA imebainika kwamba dhana ya udhibiti wa Ndani haitekelezwi ipasavyo katika baadhi ya Mamlaka kiasi cha kuathiri utawala bora na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma,

KWA HIYO BASI Bunge linaazimia kwamba Serikali isimike na kutumia ipasavyo mifumo ya udhibiti wa ndani hususani mifumo ya TEHAMA katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini. Usimikaji na matumizi ya mifumo hii viende sanjari na kutoa mafunzo kwa Watendaji husika kwa ajili ya kuimarisha uongozi, utendaji na matumizi bora ya fedha za umma nchini.

3.9 Stahiki za Watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoshughulikiwa Ipasavyo.

KWAKUWA ni dhahiri kwamba stahiki mbalimbali za Watumishi wa umma ikiwemo kupandishwa madaraja, kuongezwa mishahara, kupandishwa, kubadilisha kada nakupata mafunzo ya fani zao ni muhimu kwa ajili ya kuongeza ufanisi na tija katika kutekeleza majukumu yao,

NA KWAKUWA sasa Serikali imeanza vyema kushughulikia masuala haya, **KWAHIYO BASI** Bunge linaazimia kwamba *Kazi lendelee* kwa Serikali kutimiza wajibu wake katika ajira na stahili za Watumishi wa umma kama zilivyoainishwa katika Sheria za nch. Pendekazo hili linakusudia kuisaidia Serikali ili iwe na idadi stahiki ya watumishi wenye ari ya kulitumikia taifa kwa uzalendo, ufanisi na tija zaidi ya ilivyo sasa.

3.10 Mali chakavu

KWAKUWA ni dhahiri kwamba katika Halmashauri nyingi nchini kuna mrundikano wa magari chakavu yanayotakiwa kuuzwa au kutengenezwa ili yaweze kutumika,

NA KWAKUWA kuendelea kuwepo kwa magari hayo ni hasara zaidi kwa Serikali na ni uharibifu wa mazingira,

KWA HIYO BASI Bunge linaishauri Serikali kuweka wazi Mwongozo wa Uondoshaji wa Mali chakavu katika taasisi za umma na kuendesha zoezi kabambe la uondoshaji wa gari chakavu katika Halmashauri.

4.0 SHUKRANI

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa mwanzo mahiri wa Uongozi wako uliotuwezesha kuwasilisha Taarifa hii. Tunatumai utatuongoza vyema zaidi tuweze kukamilisha Uchambuzi wa Taarifa ya CAG ya Mwaka 2020/2021 mara itakapowasilishwa Bungeni.

Aidha, tunaipongeza sana Sekretarieti ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge mwenye tajiriba kubwa katika taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi. Sekretarieti imetusaidia sana katika utafiti, uratibu, upatikanji wa taarifa na ushauri katika masuala mbalimbali ya Kamati na Serikali za Mitaa. Tunawashukuru sana Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Bw. Athuman Hussen, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi katika Sehemu ya Fedha na Uchumi Ndg. Dickson M. Bisile ambaye pia ni Katibu wa Kamati ya LAAC akisaidiana na Ndg. Wilfred Magova na Ndg. Paul Chima wa kutekeleza

wajibu wao ipasavyo. Ninawashukuru Watendaji wa Serikali hususani Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kila wakati tulipohitaji ufanuzi wa hoja mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wa LAAC kwa uvumilivu, ushirikiano na uchapa kazi, na ninaomba kuwatambua kwa majina yao kama ifutavyo:-

- | | |
|--|---------------------|
| 1. Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb | - Makamu Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb | - Mjumbe |
| 4. Mhe. Mohamed Abdulrahman Mwinyi, Mb | - Mjumbe |
| 5. Mhe. Anastazia James Wambura, Mb | - Mjumbe |
| 6. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb | - Mjumbe |
| 7. Mhe. Mohammed Lujuo Monni, Mb | - Mjumbe |
| 8. Mhe. Ally Yahaya Mhata, Mb | - Mjumbe |
| 9. Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma, Mb | - Mjumbe |
| 10. Mhe. Neema Gerald Mwandabila, Mb | - Mjumbe |
| 11. Mhe. Jeremiah Mrimi Amsabi, Mb | - Mjumbe |
| 12. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb | - Mjumbe |
| 13. Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb | - Mjumbe |
| 14. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb | - Mjumbe |
| 15. Mhe. Francis Isack Mttinga, Mb | - Mjumbe |
| 16. Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb | - Mjumbe |
| 17. Mhe. Ally Mohamed Kassinge, Mb | - Mjumbe |
| 18. Mhe. Twaha Ally Mpembewa, Mb | - Mjumbe |
| 19. Mhe. Tauhid Galos Cassian, Mb | - Mjumbe |
| 20. Mhe. Asya Sharifu Omari, Mb | - Mjumbe |
| 21. Mhe. Martha Festor Mariki, Mb | - Mjumbe |
| 22. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb | - Mjumbe |
| 23. Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb | - Mjumbe |
| 24. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, Mb | - Mjumbe |

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, msingi wa Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii ni Hoja za Ukaguzi wa CAG kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na majibu ya baadhi ya Maafisa Masuuli waliohusika katika mahojiano na

Kamati. Mapendekezo haya yanakusudia kuimarisha nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa na kuleta maendeleo kwa wananchi.

Kamati inafarijika kuona kuwa Rais wa Jamhuri ya Mungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa panakuwepo na nidhamu katika mapatao na matumizi ya fedha za umma Serikalini kwa ujumla. Hatua alizochukua hivi karibuni za kutengua teuzi za Wakurugenzi wa Halmashauri za Jiji la Mbeya, Manispaa ya Iringa, Manispaa ya Singida na Wilaya ya Buchosa ni kiashiria cha kuchukia ubadhirifu wa fedha za umma. Kamati inaanmini kuwa hatua zaidi zitaendelea kuchukuliwa kwa Watendaji wabahirifupi.

Hivyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liyajadili na kuyaafiki Maoni na Mapendekezo hayo ili Serikali iweze kuyapa uzito unaostahili katika kuyatekeleza kama Maazimio ya Bunge.

6.0 HOJA

Mheshimiwa Spika, Naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuyaafiki Maoni na Mapendekezo ya LAAC juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

.....
Grace V. Tendega, Mb
MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA
MITAA**

17 Februari, 2022

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Hoja imeungwa mkono na sasa tunaendelea na utaratibu wetu.

Ninayo majina hapa ya wachangiaji. Orodha ni ndefu kidogo, lakini kila Mbunge atakayetajwa jina hapa atakuwa anachangia kwa dakika tano. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar ajiandae.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote nianze kwa kukupongeza wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa asilimia zote na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa viongozi wetu katika mhimili huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati kwa uwasilishaji mzuri wa ripoti. Nina mambo mengi ya kuzungumza, lakini nitaomba kwanza nianze na hili moja tu, na sidhani kama muda utanitosha.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba mnamo Aprili 6, 2020 CAG aliwasilisha Taarifa ya Ukaguzi wa Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka Unaoshia 30, Juni, 2020. Katika uwasilishaji wake, CAG hapa Bungeni alinitaja kwa jina na nafasi niliyokuwa nashika mpaka kufikia mwaka 2020, Desemba - nafasi ya Waziri wa Maliasili na Utalii, akinihusisha na hatua mbalimbali za upungufu wa kiutendaji uliotokea kwenye Wizara niliyokuwa naisimamia.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, CAG alisema mimi nikiwa kiongozi pale, na alinitaja kwa jina; na leo nimejiridhisha kwa kupitia ripoti hizo, kwamba niliidihiresha matumizi ya Tamasha la Urithi (*Urithi Festival*) shilingi bilioni 2.085 na haikuwa kweli. Hata leo ukienda kutazama kwenye vitabu utaona siyo

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sahihi, kwa sababu kwanza wakati tamasha hili linaandaliwa na hata linafanyika, mimi nilikuwa nimelazwa hospitali kufuatia ajali nilyoipata tarehe 4, Agosti, 2018 na tamasha lilifanyika mwezi mmoja baada ya hapo, mimi nikiwa nimelazwa Muhimbili. Akasema mimi niliidhinisha wapewe *Clouds Media*, wapewe *TBC*, wapewe *Wasafi*, pesa za kufikia kiwango cha zaidi ya shilingi bilioni mbili, taarifa ambayo haikuwa kweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, CAG alitamka hapa Bungeni wakati akiwasilisha kwamba mimi nilifanya safari binafsi kupanda Mlima Kilimanjaro mnamo Septemba, 2019 na safari ile ilitumia pesa za *TANAPA* na *NCAA* kwa kufuata maelekezo yangu, jambo ambalo pia halikuwa kweli, kwa sababu safari hiyo ilikuwa ipo katika mpango wa *marketing* wa Wizara na mambo yote haya yalikuwa yako katika Mpango wa *Tanzania Unforgettable* ambao ulikuwa unatekelezwa na Wizara...

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, ili twende vizuri kwenye huu mjadala wa taarifa zetu hizi mbili za Kamati, maana nilikuwa najaribu kufuutilia, maana hivi vitabu ninavyo hapa na kwenye kompyuta. Hii taarifa unayoizungumzia, ipo kwenye ipi katii ya hizi taarifa mbili? (*Makofii*)

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya kurahisisha rejea yako, unaweza ukapitia Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi...

SPIKA: Sasa ngoja. Leo tunajadili taarifa za Kamati za Bunge mbili ili zituongoze kwenye Bunge letu kufanya maamuzi fulani ambayo tutayapeleka kama maazimio ya Bunge kwa Serikali ili wayafanyie kazi.

Sasa nataka kuelewa vizuri, ili tuelewane tunaendaje na huu mjadala? Maana naona ulipoanzia mwanzoni na hapa ulipofika sasa, ni "*taarifa ile siyo kweli, taarifa ile siyo kweli na taarifa ile siyo kweli,*" mpaka hapa nilipokusikiliza. Sasa sijajua muda wako wa kuchangia umeamua kutumia

nafasi yako kukanusha taarifa ile au umeamua kutumia muda wako kuchangia kwenye hoja hizi zilizo mbele yetu, ili Bunge baadaye liamue kwamba linaielekeza nini Serikali cha kufanya? Hicho ndicho ninachotaka kuelewa ili Kanuni zetu zituongoze vizuri tunakotaka kwenda.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, sawa. Nashukuru na bila shaka unanitunzia muda wangu, maana yake nina dakika tano tu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naorodhesha hii mifano kwa sababu Kamati ya *PACimechambua* taarifa zinazoishia Juni, 2020. Kwenye taarifa hiyo ambayo inaishia Juni, 2020 ndimo mimi nilitajwa, lakini katika *proceeds* za kazi za Kamati, hayo madai ya *CAG* hayaingii kwenye hii ripoti kwa sababu waliyatupilia mbali kwa kuwa yalikuwa ni ya uongo.

SPIKA: Sawa. Nimekuelewa vizuri Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani maelezo ya Mheshimiwa Dkt. Dkt. Kigwangalla sote tumeyasikia hapa na mimi nimeyasikia. Nafikiri zitumike njia sahihi zinazotakiwa kukanusha Taarifa ya *CAG*. Kwa sababu sisi hapa ndani tunafahamu Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali inapoletwa hapa ndani tunaipeleka kwenye Kamati ikafanyiwe kazi. Sasa ikiwa ile taarifa inazo taarifa ambazo siyo za kweli, basi lazima tutumie njia iliyosahihii.

Kwa sababu mimi niliyekaa hapa mbele mkiniweka katika mazingira kwamba niishike ile taarifa nianze kusema nani ni mwewi na nani siyo mwewi, ili niseme Taarifa ya *CAG* siyo kweli ama ni kweli, lazima zote mbili niwe nazo na niwe na vielelezo. Kwa sababu hapa, yaani Bunge lina Taarifa moja tu ya *CAG*.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, taarifa ya kukanusha uko huru kabisa kuileta kwa Spika kwa maandishi ili ifanyiwe kazi kwa utaratibu mzuri. Ukipsema hapa ndani utalielekeza Bunge kuliambia kwamba kipengele hiki cha Taarifa ya *CAG* siyo kweli kwa sababu wewe umesimama kutoa maelezo

hana, utakuwa unaniweka mimi katika mazingira ambayo; sijaiona mimi taarifa yako ambayo inakanusha zaidi ya maelezo unayoyatoa sasa.

Kwa kuwa taarifa niliyonayo mimi ni ile ya *CAG*, basi nakuruhusu ulete maelezo yako ya kukanusha ile taarifa ili ifanyiwe kazi kwa utaratibu ulio wa kawaida. Sote tunafahamu Kanuni zetu haziruhusu Mbunge kuchafuliwa na mtu yejote wala mtu mwingine yejote kuchafuliwa na Mbunge.

Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mbunge hujatendewa haki na ile taarifa, wewe ulete malalamiko yako kwa njia ya kawaida kabisa na yatafanyiwa kazi na Bunge hili. Wala usiwe na wasiwasi, unalindwa kabisa. Ila kutumia muda huu wa kuzijadili hizi taarifa za Kamati hapo ndipo ambapo wewe sasa utakuwa unazikosea taratibu zetu za Bunge.

Kwa hiyo, ama uchangie kwenye hizi au kama ni hayo yako ya kuilalamikia ile taarifa na kueleza namna ambavyo siyo sahihi, utumie njia za kawaida ambazo unaruhusiwa kabisa Kikanuni. Kama ni hayo tu ulikuwa nayo, niite mtu mwingine, halafu wewe kama nilivyotoa maelezo, una nafasi ya kumletea Spika malalamiko yako ili yafanyiwe kazi.

Haya, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, ameonesha ishara ya kuonesha kwamba pengine atachukua hizo hatua nyingine, lakini kwa sasa hana mchango mwingine zaidi ya huo aliokuwa anazungumza kuhusu yeje na ofisi ambayo aliwahi kuihudumia.

Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembwenwe, ajiandae.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Hoja hii ya Taarifa ya Kamati ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nikupe pongezi wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuunga mkono Taarifa ya Kamati yetu ya *LAAC* kwa asilimia 100. Kamati yetu imetoa mapendelekezo, maoni na ushauri ambao tunaitaka Serikali izingatie; na lengo kuu la mapendelekezo, maoni na ushauri wetu kwa Serikali ni kutaka kupunguza idadi ya hoja za ukaguzi ambazo kila mwaka zinaibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Taarifa ya *CAG* na mahojiano ya baadhi ya Maafisa Masuuli wa Halmashauri, Kamati yetu tumebaini kwamba eneo moja ambalo linazalisha hoja nyngi za ukaguzi ni udhaifu mkubwa kwenye mifumo ya udhibiti wa ndani (*internal control system*) katika Halmashauri zetu; ziko *very weak* na ndizo zinazozalisha hoja nyngi za ukaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mifumo ya udhibiti wa ndani (*internal control system*) ni mifumo ya ki-TEHAMA, kiutawala, taratibu zinazoongoza namna gani malipo yafanyike, namna gani makusanyo yafanyike ambapo Kamati yetu baada ya uchambuzi tumebaini kwamba kuna uwepo wa udhaifu mkubwa katika mifumo hii ya udhibiti wa ndani ambavyo ndivyo vinazalisha hoja nyngi za ukaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia hoja nyngi za ukaguzi ambazo zimeibuliwa na *CAG* ambaye ni Mkaguzi wa Nje; na jambo moja ambalo ni la kufahamu ili tuwekane sawa ni kwamba Mkaguzi wa Nje (*CAG*) anafanya ukaguzi wa fedha mara moja kwa mwaka, na mara nyngi anafanya ukaguzi wa mahesabu baada ya mwaka mzima wa fedha kuwa umeshapita. Katika Halmashauri zetu tunao watu tunawaita Wakaguzi wa Ndani ambao ndio sehemu ya mifumo ya udhibiti wa ndani ambapo wao wanafanya ukaguzi kila siku katika ile Halmashauri.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, hoja ambazo zinaibuliwa na huyu Mkaguzi wa Nje ambaye anakagua mara moja kwa mwaka, zinadhidihiresha wazi uwepo wa udhaifu mkubwa katika mifumo ya udhibiti wa ndani; uwepo wa *weaknesses* kubwa mno katika *internal control systems* zetu.

Mheshimiwa Spika, nitaeleza baadhi ya hoja ambazo Mkaguzi wa Nje ameibua ambazo dhahiri zinaonesha wazi kwamba Halmashauri zetu mifumo yake ya udhibiti wa ndani ni *very weak*, yaani ina udhaifu mkubwa sana. Tulikwenda kukagua miradi katika Halmashauri ya Chemba, huu ni mfano mmojawapo.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Chemba tulibaini kuwa Halmashauri imemlipa mkandarasi zaidi ya shilingi milioni 72 kwa kazi ambayo Halmashauri kwa kutumia idara yake ya *ma-engineer* hawakuikagua wala hawakuipima. Kwa hiyo, hii dhahiri inaonesha kwamba mifumo ya udhibiti wa ndani katika Halmashauri ama haipo au ni makusudi ambayo yamefanyika ili kufanya ubadhirifu wa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi akifanya kazi, *anraise certificate*. Kabla ya kulipwa ni lazima *Engineer* wa Halmashauri aende *site*, aipime kazi, aione kama imefanyika kwa *specifications* zilizokubalika, aseme ndiyo, asaini, ndipo taratibu za kifedha zianze kufuatwa na huyu mkandarasi alipwe. Ila pale ambapo mkandarasi analipwa, kazi haijapimwa wala kukaguliwa, maana yake ni kwamba *internal control system* ni *very weak*.

Mheshimiwa Spika, pia tumekuta Halmashauri nyingi kazi zinatolewa bila idhini ya Bodi ya Zabuni. Hii dhahiri ni kwamba *internal control systems* hazipo. Unawezaje kumpa kazi mkandarasi au mzabuni bila idhini ya bodi ya zabuni kama mahali pale mifumo ya udhibiti wa ndani ipo na inafanya kazi ipasavyo?

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono taarifa ya Kamati kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, atafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembewi, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, ajiandae.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuweza kunipa fursa nami kuweza kuchangia kwenye hoja ya Kamati yetu ya *PAC*.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa neema yake ya uzima na uhai ambao anaendelea kutujalia hadi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za kishindo na kuweza kushika nafasi ambazo mko nazo. Nikuombeeni kwa Mwenyezi Mungu afya njema lakini busara na hekima ziendelee kuwaongoza katika uongozi wenu.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeza Kamati yetu ya *PAC* lakini kipekee nimpongeza Mheshimiwa Mwenyekiti mama Kaboyoka kwa namna ambavyo ameweza kuiwasilisha ripoti hii kwa ufasaha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye ripoti hii, nitaelekeza michango yangu kwenye kuanzia ukurasa wa 20–24 kwenye ripoti ya Kamati ya *PAC*. Ukurasa huo unaelezea namna ya ukaguzi uliofanyika kwenye Mamlaka ya Mapato ya *TRA*. Kwa kweli ukusanyaji wa mapato ndiyo jambo ambalo llinaiwezesha Serikali kuweza kutimiza mipango ambayo Bunge lako Tukufu inaipitisha kila mwaka. Lakini bila kukusanya mapato na mapato hata kama hayatatosheleza maana yake ni kwamba mipango ambayo tunaiipanga ndani ya Bunge hili Tukufu haitoweza kutekelezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika ukaguzi wa CAG wa mwaka 2019/2020 umebaini mambo kadhaa kwenye mamlaka hii ya mapato ambayo sisi kama Kamati tumeona kwamba tuishauri Serikali kuweza kuyachukulia hatua za haraka ili kuongeza mapato ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na *trend* ya kutokutimia malengo ya ukusanyaji wa mapato, kwa mfano; mwaka 2019/2020 mapato ambayo yalikadiriwa ni trilioni 19.6 lakini ambayo yamekusanya ni trilioni 17.1. Kutokutimia malengo ya ukusanyaji mapato kwa *TRA* kuna sababishwa na mambo kadhaa; moja wapo ni mifumo ambayo *TRA* wanaitumia kwenye kukusanya mapato haya. Kwa mfano; kuna mfumo wa *ITAX*, mfumo huu unaiwezesha Mamlaka ya Mapato kuweza kukusanya mapato ya wafanyabishara mmoja mmoja. Lakini mfumo huo umegundulika na dosari kadhaa zikiwemo zinazosababisha upotevu mkubwa wa mapato au kutokukusanya mapato inavyopaswa. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali uupitie upya mfumo huu wa *ITAX* ili kuongeza mapato yanayotokana na wafanyabiashara kila mwaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *C/MIS* pia ni mfumo mwingine ambao unamilikiwa na *TRA*. Mfumo huu unalengo la kutatua changamoto za mashauri ya kodi ambayo yanaendelea kurundikana mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka 2018/2019 mashauri haya yalikuwa 770 lakini hadi kufika 2019/2020 mashauri haya yameongezeka licha ya kuwa na mfumo huu wa kuwasaidia utatuzi wa makosa haya na kufikia makosa 1097. Kiukweli tulitegemea sana kwamba kuwepo kwa mfumo huu ungeweza kusaidia kutatua mashauri haya lakini tunaendelea kuona *trend* ya ongezeko ya makosa haya ya kikodi.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu pamoja na kusababisha ongezeko hilo la makosa lakini pia kuna trilioni 360 mpaka sasa ambazo zinasubiria kutatuliwa kwenye mashauri haya. Lakini endapo mashauri haya yataweza kutatuliwa Serikali inaweza ikaingiza fedha nydingi sana. Mbali na tatizo hili la mfumo huu, pia kuna udhaifu mkubwa kwenye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mfumo huu ambao nimezungumza wa *CIMIS* ambao unamuwezesha Meneja wa Kanda moja kuweza kuingia mashauri ya kanda nyingine. Kwa kweli kama tutaweza au kama kutakuwepo maafisa ambao siyo waaminifu wanaweza wakabadilisha nyaraka za Ushahidi na kuweza kuisababishia hasara kubwa Serikali yetu. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. BAKAR HAMAD BAKAR: Mheshmiwa Spika, naunga mkono hoja hiyo. (*Makofii*)

SPIKA: Haya ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge mkiwa mnachangia ukiangalia huku mbele ukiona tu nimewasha hiki kisemeo maana yake umalizie sentensi, kwa sababu la sivyo Taarifa Rasmi za Bunge zinakaa nusu nusu unakuwa hujamalizia sentensi yako.

Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest ajiandae.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia taarifa ambayo imewasilishwa mbele yako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia taarifa hii kwanza nilikuwa naomba nichukue nafasi hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini sambamba na hilo nimpongeze Mheshimiwa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan jinsi anavyoweza kuendelea kufanya kazi kupeleka fedha katika halmashauri zetu zote nchini na kuweza kuona maendeleo yanakwenda kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nishukuru fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwa kazi kubwa na nzuri ambazo wanazifanya ili kuweza kusimamia fedha hizo. Sambamba na hilo shukrani za dhati kabisa ziende kwa Mkuu wangu wa Mkoo wa Pwani, Alhaji

Abubakar Kunenge kwa kusimamizi wake mzuri kabisa wa fedha katika Mkoa wa Pwani na Wilaya zote kwa ujumla wake. Lakini bila kumsahau Mkuu wangu wa Wilaya Kanali Ahmed Abbas kwa kazi kubwa na nzuri wambayo anaifanya ndani ya Jimbo la Kibiti katika kuweza kusimamia halmashauri, miradi ya maendeleo na fedha vilevile ndani ya halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni mjambe wa Kamati la *LAC*, kwa hiyo, nimesimama hapa kuchangia taarifa iliyokuwa imewasilishwa na Mwenyekiti wangu mama Grace Tendega ambayo imewasilisha taarifa hiyo *in very majestic way*. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie nukta mbili tu, lakini katika nukta hiyo nitaigusa sana katika sehemu nzima masuala ya upotevu wa mapato ndani ya halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, tumeona ndai ya taarifa yetu lakini tumeona vilevile wakati tulipokuwa tunafanya suala zima la ukaguzi na kuwahoji wale maafisa masuhuli. Kuna upotevu mkubwa sana wa mapato ya ndani ukizingatia kwamba mfumo unaotumika wa *POS* unautata mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, inatokea halmashauri moja au nyingine siku karibia 254 mashine ya *POS* inakuwa iko *off*, halafu hakuna taarifa zozote za kifedha ambazo zinaweza zikasoma katika halmashauri husika au kule TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mbali ya hiyo kuna tatizo lingine la msingi ambalo linapatikana katika upotevu wa fedha, tatizo hilo ni kwamba kuna kitu kinaitwa *adjustment*. Watu wa halmashauri wanachokifanya ni sawasawa kwamba mtu amekwenda kukatiwa risiti ya shilingi milioni moja, halafu baadae anakuja kufanya *adjustment* kwamba amekata risiti ya shilingi laki moja. Katika taarifa ambayo ilikuwa imesomwa na Mwenyekiti wangu hapa fedha takriban shilingi bilioni 4.5

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zimeweza kuonekana zimefanyiwa *adjustment* katika kipindi cha mwaka 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ushauri wangu, ushauri wangu kwa Serikali kuna shida pale katika Kitengo cha TEHAMA – TAMISEMI, lazima suala hili liweze kushughulikia kwa sababu haiyumkiniki halmashauri 35 *adjustment* zilizokuwa zimeweza kufanyika bilioni 4.5 kama zingekuwa halmashauri zote 86 zingeweza kufanyika *adjustment* za kiasi gani. Kwa hiyo, pale TAMISEMI katika Kitengo cha TEHAMA kuna tatizo la msingi zaidi. Kwa hiyo, ni vema Serikali muweze kuangalia nini mnachoweza kukifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini katika eneo lingine ambalo nilikuwa naomba nitoe ushauri. Kuna shida kubwa kidogo kwa wataalam wetu katika suala zima la kuweza kuwasilisha mahesabu au kuandaa mahesebu. Wataalam hawa tunajua wana *professional* zao, lakini nilikuwa naomba kuishauri Serikali waendelee kuwafanya *training* kwa sababu wanachokuwa wanakifanya zile *financial statement* ambazo zinakuja zinakuwa na mapungufu mengi sana; na kwa tafsiri hiyo hiyo maana yake ni nini? Inakwenda kusababisha madhara kwa watumizi wengine wa *financial statement*. Kwa hiyo, nilikuwa naishauri Serikali waweze kuangalia uwezekano ni jinsi gani watakavyoweza kufanya *training* kwa wataalam wetu amba wanafanya shughuli hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo lingine la msingi zaidi ambalo nilikuwa naomba nilichangie, halmashauri zetu nyangi sana zina madeni. Na madeni haya yanasaababishwa na suala zima la uandaaji wa *financial statement*. Kwenye *accounts* kuna kitu kimoja kinaitwa *massaging the figure* au *window dressing*, wanachokuwa wanakifanya ni kwamba *financial statement* inaandaliwa inakwenda kuwa-*impress other users* amba wanakuwa kama vile *financial institution*. Halmashauri inatoka inakwenda kuomba mkopo, lakini kutokana na kwamba ile *financial statement* imechezewa, kinachofanyika pale ni kwamba wanakwenda kupata mkopo, ambapo mkopo huo hawawezi kuumudu. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo maana yake ni nini? Tunaziweka

halmashauri katika matatizo mengi sana ya msingi. Halmashauri nyingi sana zinakuwa zinakesi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu kabisa naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mheshimiwa Ally Mohammed Kasinge ajiandae.

MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kipekee nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema. Nitajielekeza moja kwa moja kuchangia mifuko ya hifadhi na muda ukitosha nitachangia Shilika la *NIDA*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika, mifuko ya hifadhi ya jamii imebeba maisha ya watanzania, wafanyakazi na wakulima kutokana na umuhimu wa mifuko hii. Lakini ripoti ya CAG imeonesha uwepo wa deni kubwa ambalo ni la muda mrefu. Tukiangalia taarifa ya Kamati ukurasa wa 28 & 29 napenda kunukuu. "*Hoja kubwa ambayo imepewa msisitizo na CAG katika mifuko ya hifadhi ya jamii ni uwepo wa deni la muda mrefu ambalo mifuko inadai kwa Taasisi mbalimbali na hasa Serikali.*" Deni hili limekuwa likikwamisha sana wastaifu kupata mafao yao kwa wakati. Na nikilitaja deni hili ambalo Shirika la *NSSF* linadai ni shilingi trilioni 1.1 ambalo hadi sasa limefikisha miaka 10 deni hili halijalipwa na Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati mwininge tunailaumu mifuko hii hailipi mafao kwa wakati lakini inakuwa na mzigo mzito wa deni hili ambalo sasa inafanya kutowalipa wastaifu kwa wakati. Kwa upande mwininge wa Shirika letu la *NHIF* Serikali inadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 209.7. Ningehauri Serikali iweze kulipa fedha hizi kwani zinaharibu mizania ya hesabu na kufanya utendaji wa shirika kutokufanya kazi ka ufanisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni Shirika letu la *NIDA*. Nielezee kwa masikitiko makubwa sana. Upatikanaji wa vitambulisho vya *NIDA* umekuwa na usumbufu mkubwa na hasa kwa wananchi wangu wa Mkoa wa Singida na Kagera. Nikielezea tu mfano mdogo, Wilaya ya Manyoni ina halmashari mbili, halmashauri ya Itigi na Manyoni. Lakini kituo kinapofanyikia usajili wa vitambulisho hivi vya *NIDA* ni Wilaya ya Manyoni. Mwananchi kutoka Rungwa anatembea kilomita 200 kufuata kitambulisho cha *NIDA* ambapo sasa kituo cha kusajili kipo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, niiombe sana Serikali iangalie uwezekano wa kupata vituo vingi vya kuweza kusajili vitambulisho hivi na wote tunatambua kwamba vitambulisho hivi vina umuhimu sana na vinamtambulisha mtanzania. Mfano tu, ukitaka kufungua akaunti, kusajili line, kufungua biashara au kupata mkopo ni lazima uwe na kitambulisho cha *NIDA*. Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba, umuhimu mkubwa wa vitambulisho hivi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya *PAC* ukurasa 31 imeonesha ukaguzi uliofanywa na *CAG* kwa mwaka 2020/2021; na umebaini uwezo mdogo wa kuzalisha vitambulisho hivi. Pamoja na kununua mashine mbili mpya ambazo zilianza kufanya kazi Januari, 2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *NIDA* inatakiwa kujitathmini je, inayo uwezo wa kutoa huduma kwa wananchi? Mpango kazi wa *NIDA* wa 2020/2021 uliitaka *NIDA* kuzalisha vitambulisho milioni 13.7 lakini hadi kufikia Juni, 2021 lengo hilo halikufikiwa. Ni vitambulisho milioni 3 tu ndivyo vilivyoweza kuzalishwa na kufanya jumla ya vitambulisho milioni 9.4 ambavyo vyote vilikuwa vimezalishwa. Unaweza kuona ni jinsi gani huduma hii inavyosuasua na jinsi wananchi wanavyotaabika kupata vitambulisho hivi.

Mheshimiwa Spika, niishauri Serikali, ihakikishe vitambulisho hivi vinapatikana kwa wakati. Lakini pia ripoti

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya CAG imebaini kwamba mkandarasi hakulipwa madeni yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mohammed Kassinge, Mheshimiwa Deus Clement Sangu ajiandae.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, awali ya yote nianze kwa kukupongeza wewe binafsi kwa kuteuliwa kuwa Spika wa Bunge. Lakini njielekeze kwa sababu muda ni mchache. Ni dhahiri kwamba maendeleo ya nchi yoyote yanahitaji umeme, ni dhahiri kama tunahitaji kufikia uchumi wa katiba ambao tumekuwa tukiusema, tunahitaji upatikanaji usiosuasua wa nishati ya umeme. Wabunge wenzangu wamekuwa wakichangia mara kadhaa hapa wakiongelea changamoto ya umeme. Nitaiongelea hususan kutokana na taarifa ya Kamati ilivyoileza hasa suala zima la *TANESCO*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, *TANESCO*ina changamoto kubwa ya fedha, inakabiliwa na madeni makubwa, inadai na inadaiwa. Ukitosha taarifa ya CAG inaeleza si tu kwamba inachangamoto ya fedha lakini pia ina mtaji ambao ni *negative* yaani *working capital* ni *negative*. Ukiangalia uwiano nasoma kwenye taarifa Kamati ya *PAC* na nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti mwana mama amewasilisha vizuri sana. Ahsante sana Mwenyekiti wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukisoma ukurasa wa 26 wanaeleza uchambuzi wa vigezo mbalimbali vya tathmini ya hali fedha *TANESCO*. Anaeleza uwiano wa mali na madeni ya *TANESCO*. Anaeleza kwamba uwiano wa mali ambayo kwa kulipa zile fedha ambazo zinaweza kuwa zimeiva *current ratio* yake, mali ni trilioni 1.4, madeni ni trilioni 2.7. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hiyo ni fedha ambazo zinahitaji kama zikiwiva kwa muda mfupi illipe, kwa hiyo *automatic*

TANESCO haiwezi ku-meet expense zake za mwaka lazima ipeleke mwaka unaofuata au illipe riba au *interest*. Lakini siyo hiyo uwiano wa ukwasi *liquidity*. *Liquidity* ya *TANESCO* mali za muda mfupi trillioni 1.4, madeni trillioni 2.761 hiyo ni *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, lakini tunakwenda kwa mtaji *working capital*, uchukue zile *current asset* kwamba zile fedha walizonazo fedha zake na mali inakuja ni trillioni 1.27, ije kwenye madeni trillioni 2.76 kwa hiyo, unakuja kupata *TANESCO* inajientesha kwa *negative trillion* 1.296. kwa hiyo tunakata ifanye nini? Tunawenza kuwa na mipango mikubwa ya kuongeza nishati na tumeona juhudhi zikifanywa na Serikali lakini shirika ambalo limekasimiwa mamlaka ya kununua na kusambaza umeme kama inajientesha kwa hasara tujue kwamba changamoto ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, siyo hiyo tu, nimepitia nimeona madeni *TANESCO* inadaiwa na *Songas Capacity Agency* zaidi ya bilioni 293 ameeleza hapa Mwenyekiti wa Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini siyo hiyo tu na kwa sababu hajjalipa kwa wakati hivyo imepigwa riba ya zaidi ya bilioni 62 hiyo hiyo *TANESCO* ila cha kushangaza *TANESCO* hiyo hiyo inaidai taasisi mbalimbali za Serikali zaidi ya bilioni 422. Kwa hiyo, yenyewe ipo ina *suffer* lakini na wadeni wake ambao hawaii. Kuna taasisi mbalimbali za Serikali ambazo zimekuwa zikitumia huduma na hazilipi kwa wakati. Nitoe rai kwa Serikali, hebu hizo taasisi kwa sababu zinakuwa zinapewa ruzuku walipe fedha ili *TANESCO* iweze kuijientesha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama tunataka kuona hayo mabadiliko na mabadiliko chanya ya usambazaji wa umeme tuiwezeshe *TANESCO*. Tuhakikishe kwamba ina-*working capital* ya kutosha tuhakikishe kwamba inaweza *ku-meet obligation* zake za *day to day*, kwa sababu, mwisho wa siku changamoto kubwa inatokana na riba ambayo imekuwa inapigwa mara kwa mara kwa sababu haiwezi kulipa fedha

zake kwa wakati. Hiyo nitaongelea bila kusahau *TANESCO* na yenyewe imekuwa na madudu yake.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* illingia mkataba mwaka, 2007 na Kampuni moja ambayo ni ya Madini ambayo sasa katika huo mkataba *TANESCO* ilipaswa kuwa inakusanya fedha, kutoka kwenye hiyo Kampuni ya Buzwagi inaweka kwenye *a certain account* kwa ajili ya kufanya *maintenance*. Imekuwa haifanyi hivyo *for over ten years*, ina maana wewe ukaona kwamba mbali na kwamba ina changamoto ya fedha lakini pia, kuna changamoto ya uzembe ambayo *TANESCO* lazima wasemwe na mamlaka lazima zisimamie kuona inaweza kutimiza vigezo na masharti yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hayo ni machache ambayo naweza kuyasema na kwa sababu ya muda niongelee kidogo *Issue* ya *NIDA*.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Muda umekwisha nakushukuru. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Mohamed Kasinge atafuatiwa na Mheshimiwa Deus Clement Sangu NA Mheshimiwa Conchesta Leons Rwamlaza ajiandae.

MHE. ALLY M. KASSINGE: Mheshimiwa Spika, ahsante awali ya yote niungane na wenzangu kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa na Bunge hili kuwa Spika wetu na kwa kweli sisi Wabunge tuna imani kubwa. Tunaomba Mungu akusimamie. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo ambazo pia zimfikie Mheshimiwa Zungu Naibu Spika, nianze sasa kwa kuchangia hoja au taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) kama ambavyo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu, mama Grace Tendega, ikiwa ni hesabu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali katika Mamlaka za

Serikali za Mitaa kuishia mwezi Juni, 2020. Ni ukweli kwamba Serikali imekuwa na juhudhi za dhati kabisa kupeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ikiwemo sekta ya afya, sekta ya elimu na sekta nyinginezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na utaratibu wa kupeleka fedha kwa utaratibu wa *flat rate* kwa kila halmashauri, kwa mfano, Serikali imekuwa ikiipeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni kwenye shule zetu za sekondari. Hapo awali ilikuwa ni Shilingi milioni 75 na baadaye ikawa ni shilingi milioni 80, lakini kumekuwa na namna tofauti tofauti katika utekelezaji wa eneo hili.

Mheshimiwa Spika, katika baadhi ya halmashauri Shilingi milioni 80 imetosheleza kabisa kujenga bweni moja la wanafunzi kukaa idadi ya watoto 80 ikiwemo *facilities* za ndani ya bweni hilo, kwa maana ya vitanda, lakini katika baadhi ya halmashauri shilingi milioni 80 hazijatosha na hakuna ambacho kimefanyika na kazi haina viwango. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika hili nina maeneo mawili ya kuzungumzia. Eneo la kwanza ni kuwapongeza wale ambao kwa dhati kabisa wamefanya vizuri ikiwemo, halmashauri ya Wanging'ombe ambayo ni Jimbo la Mheshimiwa Festo Dugange. Wamejenga shule, wamejenga mabweni kule katika Sekondari ya Wanging'ombe, wamejenga bweni katika Sekondari ya Wanike kwa Shilingi milioni 75 na imetosheleza hakuna namna yoyote ya harufu ya ubadhirifu wa fedha. Hata hivyo, katika halmashauri zingine shilingi milioni 80 imezama, mabweni hayajakamilika, vitanda hakuna na bado fedha haitoshelezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hiki ni kiashiria tosha kabisa kuna mazingira ya dalili ya matumizi mabaya ya fedha hizi za umma. Katika hili niseme pia kwamba Serikali imekuwa ikiipeleka fedha hizi bila kufanya tathmini ya kina. Katika maeneo mengine ni kweli kumekuwa na dalili za ubadhirifu lakini katika mazingira mengine ambapo *facilities* zote

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ikiwemo bidhaa za madukani, zinapatikana kwa urahisi na zile bidhaa ambazo zinapatikana kwenye mazingira halisi ikiwemo mchanga, mawe, kokoto zinapatikana, bado fedha hizi hazijatosha.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme tu kwamba wakati Serikali ili kuzipunguzia mzigo wa hoja halmashauri zetu, zinapeleka fedha hizi kwa utaratibu huu wa *flat rate*, zingefanya kwanza tathmini ya kimazingira ili kujua kila halmashauri na kila maeneo yanahitaji shilingi ngapi? Kwa mfano, katika baadhi ya halmashauri zimekuwa mbali na maeneo ambayo bidhaa za viwandani zinapatikana. Huwezi ukapeleka utaratibu wa *flat rate* na wakafanya kama vile ambavyo wangeweza kufanya vingine kwa vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa ushauri huu, niunge mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Ameshamaliza, kwa hiyo hawezu kupewa taarifa.

Mheshimiwa Deus Clement Sangu atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Leons Rwamlaza na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos ajiandae.

MHE. DEUS C. SANGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja zillizopo hapo mezani. Kwanza kabisa niungane na wenzangu kukupongeza kwa nafasi hii ya kuwa Spika wa Bunge pia nimpongeze Naibu Spika. Lakini kwa namna ya pekee nizipongeze *oversite committee* zote kwa maana ya *PAC* na *LAAC* kwa *presentation* ya Wenyeviti wake wamefanya *presentation* nzuri sana niwapongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo nitajikita kuchangia hasa kwenye benki zetu za Serikali nataka nielezee *going concern* ya benki zetu za Serikali. Serikali kuwa na benki zake yenywewe

ni jambo muhimu sana, lakini kuanzia mwaka, 2017 Serikali ilichukua uamuzi wa kuunganisha benki zake. Kwanza, ilianza kuichukua TWIGA kuunganisha na Benki ya Posta; baadaye ikaja kuchukua Benki ya Wanawake ikaiunganisha mwaka, 2018 na Benki ya *TPB*. Shida kubwa hizi *major* mbili hazikuwa na tatizo kubwa shida kubwa ilikuja pale ambapo, Serikali iliamua kuchukua benki ya *TIB Corporate* na kuiunganisha na Benki ya *TPB* ili kuunda Benki ya *TCB* ambayo ni Benki ya Biashara ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lengo ilikuwa ni zuri labda tulikuwa tuna-*revert will yetu* ya kubinafsisha Benki ya *NBC* ili tuwe na Benki ya Biashara ya kwetu ya Serikali, lakini kitendo cha kuileta *TIB Corporate* tayari ilikuwa na mikopo chechefu ya Shilingi bilioni 130, hii imekuja kuharibu mizania ya vitabu vya, Benki hii ya *TPB* ambayo ilikuwa tayari ipo kwenye *top ten* ya benki zinazofanya vizuri hapa nchini. Kwa sababu, tuna benki sasa zaidi ya 50 lakini benki yetu ya Serikali ya *TPB* ilikuwa *inaperform* vizuri. Kuleta kwa mikopo chechefu na pia ikaleta mzigo wa wastaafu kwa maana ya *staff management team* ile ambayo ilikuwa na mishahara mikubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mpaka leo kutokana na ofisi ya *Treasurer kuto-solve huu mtanziko* pale ndani ya benki ni kama kuna *management* mbili. Kuna wale waliotoka *TIB Corporate* ambao *wage bill* yao kwa mwezi inakwenda, 1.7 *billion shillings* ambao kazi kubwa inayokwenda pale ni kusoma magazeti. Unalipa shilingi 1.7 *billion* kwa mwaka fedha za walipa kodi hawajapangiwa majukumu, sasa inaonekana Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina hawakujipanga wakati wanafanya hii *merger*. Iilitakiwa watumie *approach* ile waliyofanya wakati wanabinafsisha ile Benki ya *NBC*, walichukua madeni na mali zile ambazo, wale makaburu hawakuzitaka, wakaunda Shirika pembedi tanzu la *CSC* kwa ajili ya ku-*deal*/na yale mambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa huku *approach* ilikuwa wakapeleka madeni mabaya Shilingi bilioni 130 na *Treasurer aliji-commit* kwamba huu mzigo nitaubeba. Tangu Juni, 2020 ameweza ku-*recover* Shilingi bilioni tatu tu, kwa hiyo

itamchukua zaidi ya miaka 40 *ku-recover* ile mikopo chechefu. Ile mikopo mingi, ukiona haina *future* yoyote, mikopo ile yote yawezekana hata Serikali isiweze *ku-recover* zile fedha. Sasa, naomba kuishauri Serikali kuna *approach* mbili ambazo unaweza kutumia kuisaidia benki hii, ambayo ina matawi 83 na ina wakala wa benki zaidi ya 3,500 nchi nzima na ni benki ambayo tunaitegemea kama Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza; wakubali kuchukua ile mikopo iondoke kwenye mizania ya vitabu vya Benki ile ya *TCB*. Pili, hawa *management* ambao wanalipwa Shilingi 1.7 *billion* na wapo tu wanasoma magazeti, watafutiwe sehemu nyingine ndani ya Serikali, kuna mamlaka nyingi, wakafanye kazi, kuliko kutumia fedha za walipa kodi hawafanyi kazi yoyote. Hii *contradiction* tu ni basi tu katika *making decision*, illitakiwa siku ile tu ya *merger* wawe wameamua hili jambo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tatu, tuna benki yetu nyingine kubwa kabisa Benki ya Maendeleo ambayo ni *TIB Development* katika nchi yoyote ile kwa mfano China *Development Bank*. Hii *China Development Bank* ndio ina-finance miradi yote mikubwa ya kimkakati ndani ya nchi ya China, lakini sisi hii *TIB Development* alipoianzisha Mwalimu Nyerere mwaka 1970 alikuwa na nia njema. Kukaingia ulaghai na ujanja ujanja mpaka ninaposema leo hii mikopo chechefu imefika Shilingi bilioni 327 na kila mwaka wakijitahidi wanakusanya labda shilingi bilioni mbili au tatu. Maana yake hata benki hii leo hii ukienda *wame-stop lending* hawakopeshi, kwa sababu, fedha ina *liquidity crisis* maana yake ni nini kinachoweza kutokea hapo?

Mheshimiwa Spika, wamesema watatoa *non cash bond*. *Noncash bond* ni kwenda tu kuweka mizania ya vitabu ikae vizuri, lakini *hai-address* tatizo la mtaji la benki hii. Ina mtaji wa Shilingi bilioni 38, lakini *requirement* ya Benki Kuu inatakiwa Benki aina ile ya *TIB Development* iwe na mtaji wa shilingi bilioni 50. Sasa, leo hii unakwenda kufanya *non cash bond* ambayo pia inakwenda na *impact* kwenye deni la

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Taifa, tayari hata *TCB*wanasema, wanakwenda kuweka *non cash bond*, yes ni *initiative* ya kuweka mizania ya vitabu, isome vizuri, lakini hai-*address* matatizo ya benki zetu hizi za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali kama inataka kweli twende mbele kwenye *financial sector* na hapa sijaongelea Benki ya Maendeleo ya Kilimo nayo hali ni hii hii. Maana yake sisi ndio *tuna-prove failure*; Benki Kuu inasema asilimia tano ya *non-performing loan against assets* zako ndio inatakiwa, lakini sisi kwa mfano, *TIB* leo mikopo chechefu ni zaidi ya asilimia 50 wakati inatakiwa iwe asilimia tano, tunakwenda wapi tumeamua kuua benki zetu wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa sababu ya muda nilishie hapa. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nasikiliza huku kuna watu wanasesma, mwongezee dakika tano.

WABUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, ndio. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge atakuwa amemaliza hoja yake.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, bado. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa ahsante sana, naona hadi Daktari Msukuma amesimama kabisa kuashiria anakubaliana na hoja za msingi na Serikali wameshasikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhidha Cassian Gallos na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Kamati yetu ya *LAAC*, mimi ni Mjumbe wa *LAAC* ya taarifa yetu ya mwaka ya ukaguzi wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue fursa hii kukupongeza mimi nimeulizwa maswali mengi kwamba, kura nilimpigia nani nikasema mimi nampigia mwanamke lakini mwanamke mwenye uwemo. Kwa hiyo, kura yangu haipigwi holela, kwa hiyo nakupongeza sana Mungu akubariki, ubarikiwe sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, halmashauri hizi zina kazi kubwa. Kazi yake kwanza ni kutoa huduma kwa wananchi, lakini pia, halmashauri hizi zinatekeleza maagizo, sera, maelekezo ya Serikali Kuu. Ukiyatazama majukumu hayo ni majukumu makubwa ambayo yanataka udhibiti na usimamizi mkubwa na udhibiti huu unapaswa ufanywe ndani ya halmashauri zenyewe, lakini pia kupitia Serikali Kuu, Wizara ya TAMISEMI lakini pia na hata Sekretarieti za Mikoa chini ya *RAS* na Mkuu wa Mikoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ya *LAAC* tunafanya kazi ya uchambuzi wa taarifa za *CAG* lakini mengi tumeyaandika katika taarifa yetu, lakini hatuwezi kuandika maneno yote, kuna mengine ambayo tutachangia kidogo kulingana na muda.

Mheshimiwa Spika, nitaongea kuhusu miradi inayotekelawa kwa mfumo wa *force account*. *Force account* ni kitu kizuri sana, Serikali inatekeleza miradi yake kwa bei nafuu na tunapata miradi mingi ambayo inatekelezeka. Ipo miradi ambayo inatekelezwa na *force account* ambayo sio mizuri na sio imara ambayo inaleta hofu kwamba, inawezekana huko mbele baada ya miaka fulani tunaweza kuleta *crisis* za majengo haya kutoendelea kutumika vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba ifikirie sasa kuwa na ukomo wa kiwango cha fedha zitakazotumika katika *force account*. Kwa mfano, tulikwenda kutembelea Mradi wa Machinjio kule Vingunguti katika Wilaya ya Ilala Dar es Salaam; wanao mradi mzuri sana ambao umetekelawa kwa zaidi ya Shilingi bilioni 12, lakini wameweka mkandarasi ambaye ni *National Housing Corporation*. Kwa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiyo, unaweza kuona ule mradi ulitekelezwa kwa sababu una fedha nyingi na waliweka mkandarasi ndio aliweza kutekeleza. Kwa hiyo, miradi kama hii haiwezi kutekelezwa kwa *force account*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali iweze kutenga kwamba fedha hizi kama mwisho ni Shilingi bilioni tano iende kwa *force account*; na kama ni zaidi ya hapo basi wasiogope kuweka wakandarasi ili kuwe na ufanisi wa miradi. Nayasema hayo kwa sababu gani? Ukienda katika miradi hii ambayo inatekelezwa kwa *force account*, zipo Kamati za Ujenzi, Kamati hizi zina watu ambao sio wataalam hata kidogo ni wachache. Hakuna *ma-engineer* katika halmashauri, kwa hiyo, unakuta hizi kazi zinafanywa bila kuwa na usimamizi ambao unaleta ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda niihauri Serikali kwamba sasa umefika wakati kwa vile hatuna *ma-engineer*, basi kuwepo na Mpango, wa kufundisha watoto wetu kuititia VETA tupate *technicians* ambao wanaweza kwenda kufanya kazi hizi katika ngazi za chini. Kwa sababu, kule tumegundua kwamba wakati mwingine *wana-pick* Walimu tu, mtu yejote ambaye anajua kuweka tofali tu, wala hajawahi kujenga chochote katika maisha yake ambacho ni mradi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunashauri Serikali itazame ni namna gani ya kuweza *ku-train technicians*, wapo vijana ambao wamemaliza *form six* wamechukua masomo ya kisayansi. Wanaweza kupelekwa wakafundishwa, yaani huo ni mpango mkakati halafu tukawaajiri vijijini kule, wakaenda kusaidia katika kusimamia majengo hayo. Pia waajiri *ma-engineer*, halmashauri haina *ma-engineer*, *ma-engineer* wote walihamia *TARURA*, kutoka halmashauri kwa sababu *TARURA* wana *package* nzuri za mishahara. Kwa hiyo, ni vyema tukahakikisha kwamba *ma-engineer* wanaajiriwa sambamba na *ma-technicians*, ambao wanaweza kusaidia kazi hizi zikaendelea kule vijijini na sehemu nyingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nikimaliza hiyo nije kwenye Mfuko wa Wanawake pamoja na kwamba muda ni mfupi. Mfuko

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Wanawake ni Mfuko mzuri sana na nimekuwa nikiusema kwamba una malengo mazuri sana ya kusaidia vijana wetu kusaidia wanawake na watu wenye ulemavu. Hata hivyo, ukiangalia katika ripoti ya CAG ya mwaka, 2019/2020 amesema, fedha ambazo zimekopesha ni zaidi ya Shilingi bilioni 27, hazijarejeshwa. Jana Mheshimiwa Kimei aliuliza swali Na. 136 ambalo alitaka kuona ufanuzi wa fedha hizi, katika miaka mitatu mfululizo na nashukuru kwamba TAMISEMI walitoa taarifa na nafikiri ni *latest*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwamba mwaka, 2018/2019 halmashauri zote Tanzania nzima zilikopesha Shilingi bilioni 42.06; mwaka, 2019/2020 Shilingi bilioni 40.73; mwaka, 2020/2021 Shilingi bilioni 51.81. Fedha zilizorudishwa katika fedha hizo ambazo ni Shilingi bilioni 135 ni Shilingi bilioni 48 tu. Kwa hiyo, unaweza kuona taswira ikoje ya fedha hizi kama tunaweza kuwa na zaidi ya Shilingi bilioni 50 kwa miaka mitatu mfululizo, ziko hazijarudishwa, ina maana hizi fedha ambazo ni fedha za walipakodi, ambazo ni fedha za watu wanaochanga ndani ya halmashauri hazirejeshwi, taswira ya Mfuko huu ni nini hasa inacholenga. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, naona dakika tano ni kidogo naomba kuunga hoja Kamati hii. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

MHE. TAUHIDA C. GALLOS: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia. Kwanza kabisa, nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuteuliza na chama chako, Chama cha Mapinduzi, lakini vilevile kuweza kupata kura za kishindo kwa Wabunge.

Sambamba na pongezi hizo nimpongeze Naibu wako ambaye ni msaidizi wako kwa kuchaguliwa pia naye na Wabunge kwa kura nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitajielekeza kwenye matumizi ya miradi ya halmashauri. Halmashauri imekuwa na kipindi cha utekelezaji wa fedha. Kulikuwa na mambo kadhaa sugu ambayo yanaisumbua halmashauri. Kwanza, tulikwenda na tulipita kwenye awamu ya Wanasheria ambao walikuwa wakisababisha matatizo makubwa ndani ya halmashauri zetu. Tulipotoka hapo tukaja na ugonjwa wa Mfuko wa asilimia 10 ambao haukuwa na usimamizi mzuri; kwa sehemu haujapona moja kwa moja, lakini kwa sehemu kidogo kuna unafuu si asilimia 100 lakini asilimia zaidi ya 60 kidogo mabadiliko yapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna ugonjwa ambao kwa sasa unasumbua Halmashauri zetu. Ugonjwa huo ni matumizi mabaya ya fedha; kuchukua fedha za Halmashauri kuwekeza kwenye majengo na kutokuyamaliza. Ugonjwa huu umekuwa tatizo ndani ya Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi za wananchi zinazokusanywa kwa kodi zinaenda kutengenezwa miradi ambayo haiishi, inakaa zaidi ya miaka mitatu mpaka mitano bila ya kumalizika. Nitoe mfano kama wa Halmashauri Tatu ya toka mwaka 2012; kuna Bwalo la Chakula, Chamwino; mradi wa Babati Mjini - nyumba za Waganga; mradi wa ukumbi - Mpwapwa. Hiyo ni baadhi ya miradi ambayo ndani ya Halmashauri zetu zimetumia fedha nyingi lakini miradi haikumalizwa.

Mheshimiwa Spika, kuna aina za miradi ndani ya Halmashauri zetu; kuna miradi ya Serikali, kuna miradi ya wananchi na miradi ya watendaji. Miradi ya Watendaji mara nyingi huwa haiishi, kwa sababu huwa na miradi yenye fedha nyingi ambayo haihitajiki na wananchi, siyo malengo ya wananchi, siyo mtazamo wa Serikali; nao huianzisha miradi ile iwe ni njia au kichochoro cha kufanikisha mambo yao. Zinachukuliwa fedha kwa mamilioni lakini bado unakuta

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zimeenda kutumbukizwa sehemu toka mwaka 2012 na ipo miradi mingine zaidi ya mwaka 2012 haimalizwi.

Mheshimiwa Spika, imebidi sasa tuiwekee mkazo. Mheshimiwa Rais wetu amekuwa mfano kwenye miradi. Tuchukulie mfano wa reli ambao sasa hivi unamaliziwa na Mheshimiwa Rais na bado anapeleka fedha kumaliza miradi hii. Kama ni miradi ambayo ina malengo na inahitajika kwa wananchi sielewi kuna tatizo gani la Halmashauri kila mwaka wanatenga fedha kuanzisha miradi mipya na miradi mingine kuendelea kubaki ikiwa ni miradi ambayo haifanyiwi kazi na pesa ya wananchi inapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miradi mikubwa inayohitajika kwa wananchi ni hospitali, shule; hiyo ndiyo miradi wanayoihitaji wananchi. Leo unaenda kuchukua fedha unaipeleka Mpwapwa unaenda kuweka *hall* unategemea mtu wa Mpwawa kumkodisha *hall* akafanye shughuli kwa shilingi milioni tatu, itaingiza wapi fedha hizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, chukulia inaenda kujengwa nyumba ya Mganga vyumba vitatu, inachukua miaka minne bila kwisha, lakini fedha ya wananchi ipo pale tayari imeshakaa. Tunaishauri Serikali kuondokana na matumizi mabaya ya fedha ambapo wananchi wanazihitaji na wanahitaji zifanyiwe kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja ya Kamati yetu ya *LAAC*. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga na Mheshimiwa Venant Protas Daud ajiandae.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, nami niungane na wachangiaji wengine kukupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana. Naipongeza sana Kamati ya *PAC* na *LAAC* kwa taarifa ambayo wametuletea hapa inayoleta taswira kwa nchi. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, leo ninaomba niishauri Serikali jambo moja. Serikali inapotaka kuingia kwenye uanzishwaji wa mifumo kwa ajili ya ukusanyaji wa fedha, naomba ifanye upembuzi yakinifu ili mifumo inayotengenezwa ije kuwa na tija kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Bandari mwaka 2010 iliingia mkataba wa miaka minne na *Softech*, mpaka 2014, kwa ajili ya kutengeneza mfumo wa ukusanyaji wa fedha. Mfumo huu ulikuwa unachukua gharama ya shilingi milioni 694, lakini mpaka kufikia mwaka 2014 mfumo haufanyi kazi na tayari Mkandarasi alikuwa amelipwa shilingi milioni 600 sawa na 87%. Inasikitisha kwa sababu fedha hizi ni za Watanzania, lakini mradi ule haukufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa *Softech* waliongezwa mkataba wa thamani ya shilingi milioni 55 kwa ajili ya kufundisha watumishi wa *TPA* ambapo mfumo haukufanya kazi. Pamoja na hayo, walilipwa shilingi milioni 55 zote na katika zile shilingi milioni 55 zilitakiwa kulipwa kwenye mkataba wa awali wa shilingi milioni 694. Serikali ikaingia hasara ya shilingi milioni 600 ya kwanza na ikaingia hasara ya shilingi milioni 55 ya pili. Hizi fedha ni za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, bado haitoshi, mwaka 2015/2016 kampuni ya *23rd Century System* iliingia mkataba na Serikali ya kutengeneza mfumo pale *TPA* ambao ungegharimu shilingi bilioni 14, lakini mpaka mwaka 2019 mfumo huu haufanyi kazi, Serikali imelipa shilingi bilioni tisa; hasara kwa Serikali na hizi ni fedha za walipa kodi. Bado haitoshi fedha zililipwa shilingi bilioni tisa, lakini Mkandarasi hakulipa kodi ya zuio (*Withholding Tax*), akatoroka na fedha za wananchi sawa na shilingi milioni 874. Ni lazima Serikali ichukue tahadhari inapoanzisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado haikutosha kampuni ya *SAP* mwaka 2020 ikaajiriwa; kazi yake ni kuangalia kama huyu *23rd Century System Limited* alifanya kazi ambayo ilistahili kulipwa zile fedha. Naye akalipwa dola za Kimarekani 433,000 sawa na shilingi milioni 874. Hizi ni fedha za walipa kodi na

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

bado mifumo haikufanya kazi. Tunavyozungumza sasa hivi, ule mfumo haukufanya kazi tena pale *TPA* na fedha za walipa kodi zililipwa. Katika mifumo hii ni shilingi bilioni 17 zilitumika na mfumo haukufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, siyo *TPA* peke yake, ukienda pale *GSPA* wamenunua mfumo wa shilingi bilioni 1,087, sasa wamekuja kugundua ule mfumo hautoi yale mahitaji ambayo walikuwa wanayahitaji. Wamekuja kugundua ule mfumo hautawasaidia tena. Sasa wameshindwa kuutumia ule mfumo na fedha za Serikali zililipwa shilingi bilioni 1,087. Wameandika kibali kwenda Wizara ya Fedha, wabadilishe watumie mfumo mwengine na Wizara ya Fedha imewakubalia na hasara tayari imepatikana katika fedha za walipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika,...

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Mheshimiwa Lusengekile, kuna taarifa. Nani anatoa taarifa?

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Spika, ni hapa.

SPIKA: Aah, Mheshimiwa Humphrey Polepole.

TAARIFA

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mzungumzaji anateremsha taarifa muhimu sana, nilitaka kumpa taarifa kwamba *TANESCO* mwaka jana 2021 mwishoni wameingia mkataba na kampuni ya kutoka India kwa zaidi ya shilingi bilioni 69 kwa ajili ya mifumo ya TEHAMA na watu wengi tunajiliza kama uwezo huo wa kampuni kutoka India haupo nchini Tanzania licha ya kwamba mifumo mingine ya Kiserikali inatengenezwa hapa Tanzania?

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Simon Lusengekile unapokea taarifa hiyo.

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, ninapokea taarifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa tuone ni namna gani Serikali inaingia hasara katika mifumo ambayo haina tija na haileti matokeo chanya kwa Taifa. Wahasibu wanaita *this is nugatory expenditure. The Government incur some expense that cannot generate economic benefit.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kwa wale wote ambao wamesababisha hasara kwa Taifa. Watumishi ambao wapo ofisini wamesababisha hasara kwa Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, tayari ameshaanza kuchukua hatua na kumwelekeza *DG* wa Bandarikuhakikisha kwamba wafanyakazi waliopo pale waliosababisha hasara hii wanachukuliwa hatua za haraka.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ichukue hatua kwa makampuni haya ambayo yalilipwa fedha nyngi na Serikali shilingi bilioni 17 na mfumo haukuleta tija ikiwepo na hii *23rd Century System Limited* iweze kulipa fedha za *TRA* ambayo ilikuwa ni *Withholding Tax*, shilingi milioni 877. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo naomba pia nichangie kidogo kuhusu kiwanda cha sukari pale Mbigiri. Serikali iliingia mkataba wa kusimika kiwanda cha sukari cha kisasa pale Mbigiri, lakini mpaka sasa tunapozungumza, kiwanda kile hakijawahi kusimikwa na Serikali imepata hasara ya fedha kwa sababu walilima miwa wakijua kwamba kiwanda kitawahi kuja, miwa ile imeharibika, tayari Serikali imepata hasara ya zaidi ya shilingi milioni 300. (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, haitoshi...

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Simon Lusengekile, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

T A A R I F A

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nampa taarifa jirani yangu wa Busega kwa mchango wake mzuri. Siyo Serikali tu, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imelazimishwa kuwekezwa hapo, PSSSF miaka mitatu imetengeneza hasara ya shilingi billioni 11; na ukiuliza sababu, Serikali haijapeleka mashine.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Simon Lusengekile, unapokea taarifa hiyo?

MHE. SIMON S. LUSENGEKILE: Mheshimiwa Spika, pale Mbigiri NSSF ina 96% na Magereza wana 4%, tunazidi kudidimiza taasisi zetu. Wallingia mkataba wa kununua miwa ya *outgrowers*; wakulima wa mazingira ya pale. Wakulima wamekopa fedha benki kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo cha miwa wakijua kwamba baada ya kiwanda kuja watauza ile miwa. Kiwanda hakijasimikwa mpaka sasa hivi, wananchi wanateseka, wanashindwa kulipa mikopo kwa sababu kiwanda hakijapatikana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara husika sasa iharakishe kusimika kiwanda hiki ili kiweze kuleta tija kwa Watanzania. Ninaamini kitaleta ajira nyngi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. (*Makof!*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, taarifa!

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, mzungumzaji ameshakaa. Kwa hiyo, hawezikupewa taarifa. Ameshamaliza mchango wake. Ahsante sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Venant Protas Daud na Mheshimiwa Francis Isaac Mtinga, ajiandae.

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami kama Mjumbe wa Kamati ya *LAAC* naunga mkono Taarifa ya Kamati kwa asilimia mia moja. Nasi kama Wabunge wa Bunge hili la kwanza tunaendelea kujifunza kwa Mwenyekiti wetu na Katibu wetu wa Kamati ya *LAAC* Bwana Bisile, mambo mazuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema wenzangu, nami nakupongeza wewe na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa; na siku ile tumekuchagua tukakutana na Waandishi wa Habari, wakaniliza kwa mic mdomoni ghafla: “*Unafikiri Dkt. Tulia atakuwa Spika wa namna gani?*” Basi mimi nikasema atakuwa Spika wa STK; kwa maana ya Sheria, Taratibu na Kanuni. Tumeshaanza kuona humu sasa, sheria, taratibu na kanuni zikishughulikiwa vya kutosha. Uzuri wa hiyo STK ni kwamba inatujali sisi manjuka, haitubani sana. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea kuchangia kama walivyochangia wenzangu kwa haraka nikijumuisha vipengele vinne ama vitano ambavyo Mwenyekiti amevisema katika taarifa yake. Uttagundua kwamba karibu tunazungumzia upotevu au watu kuchezea karibu shilingi bilioni 64.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika taarifa yake, matumizi ya fedha mbichi, anazungumzia shilingi bilioni 18.7; kufutwa kwa miamala ni shilingi bilioni 4.5; kurekebishwa kwa miamala ni shilingi bilioni 4.8; na mawakala fedha ambazo wamezikusanya, hawajazipeleka katika Hazina za Halmashauri ni shilingi bilioni 35. Hii ni karibu shilingi bilioni 64,

ukiigawanya shilingi milioni 500 kwa Vituo vya Afya, ni karibu Vituo vya Afya 13.

Mheshimiwa Spika, katika kuzunguka na Kamati ya LAAC kwenye Halmashauri mbalimbali nimejifunza vitu vingi sana. Kutohana na ufinyu wa muda, ukweli ni kwamba kama tunataka maendeleo ya nchi hii, ni lazima kutazama Halmashauri zetu vizuri. Vinginevyo fedha zitakuwa zinatafutwa na Mheshimiwa Rais Samia duniani kote, zinaletwa, tunapeleka Idara za Kilimo, Elimu, lakini watu wanazichezea fedha hizo. Ni jambo la hatari sana. Nasi kama Wabunge siku hizi tunalalamika hapa.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti amesema, kwa miaka mitatu *trends* zinaonesha bajeti yako katika Bunge hili haipelekwi karibu kwa *fifty percent*. Amesema tunaidhinisha shillingi billioni 977 inapelekwa shillingi billioni 497 kwa sababu ya fedha hizi kutokukusanywa vizuri na fedha zile ambazo tunatakiwa tupate kama mapato, hazikusanywi. Wabunge wamesema kuhusu *POS* na kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza, ni lazima tuishauri Serikali yetu, nami mwisho nitashauri. Nimeona juzi Mheshimiwa Rais Samia amechukua hatua tu, amepeleka fedha za madarasa, watu wamecheza nazo, akaondoka na Wakurugenzi Wanne. Tumeona Mkuu wa Mkoa wa Mara alivyozungumza kuhusu Wakuu wa Idara na changamoto katika Halmashauri. Lile siyo tatizo la Mara peke yake, ni karibu tatizo la nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, ushauri wetu, hivi katika yote haya yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge katika malalamiko, kweli tuko *serious* katika nchi hii, kuna Halmashauri haina Mkuu wa Idara ya Ununuzi? Kweli kabisa! Yaani, tunazungumza hapa, fedha zinaenda mabilioni na mamillioni ya fedha kwenye Halmashauri; Halmashauri Mweka Hazina anakaimu. *Serious!* Tunazungumza fedha zinaliwa, unaenda unakutana na Afisa Mipango anakaimu; au unakuta mtu anayelalamikiwa ni Mkuu wa Idara miaka 20, ana malalamiko yake mpaka wananchi wanajua upungufu

wake na miradi anayoifanya katika Halmashauri ile, anaachwa.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi hata kidogo kuendelea. Kupanga ni kuchagua. La kwanza, ni muhimu sana kujaza ikama ya Watumishi muhimu. Tunajua Serikali haiwezi kuajiri watu wote, Serikali ya nchi hii inashindwa kuajiri Wakuu wa Idara wa kila Halmashauri wakapatikana watu *smart*, wenye sifa walio-*perform*, wakasimamia fedha zetu katika Idara! Haiwezekani hata kidogo. Tupange, tuchague tuhakikishe tunapata watumishi wa kutosha. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwezesha kitengo cha Ukaguzi wa Ndani. Sisi katika taarifa ya CAG, tunayopata kwenye Kamati, kwenye Halmashauri zote kuna Wakaguzi wa Ndani; na Wakaguzi wa Ndani ni kama *indicator* kwa Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi ambao tulikuwa ma-DAS, anamwambia, Mama utaratibu huu wa kufanya manunuzi hapa haujafuatwa; utaratibu upo hivi, na hivi na hivi. Mkurugenzi asiyesikia, unamkuta kwenye taarifa ya CAG.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hivi huyu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Halmashauri, gari yake mbovu, anaazima gari kwa Mkurugenzi; akitaka kwenda kwenye ukaguzi wa miradi anachukua mafuta kwa Mkurugenzi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hili suala linasemwa. Nimeangalia *video*, *Youtube* ya hotuba za Mabunge ya miaka kumi nyuma, wanalamikia hili jambo. Hivi mtu unayemkagua na kumshauri halafu unaenda kumwomba mafuta, atazingatia ushauri wako? Akiona unamsumbua, anakukanyagia tu, mafuta hakupi. Ndiyo malalamiko kila sehemu ukienda Wakaguzi wa Ndani wameshindwa kwenda kukagua miradi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Venant Daud Protas, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mttinga na Mheshimiwa Aida Khenani ajilande.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami niungane na Wabunge wote kukupongeza kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuwa Spika wa Bunge letu, nasi kama Wabunge tupo tayari kukupa ushirikiano wa asilimia mia moja. Ondoa shaka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi zote hizi, nirudie maneno yako ambayo nilikunukuu siku umekalia Kiti hicho kwa mara ya kwanza. Uli sema, sisi Wabunge ni daraja kati ya wananchi na Serikali. Tunapokuja humu, tumeleta mawazo ya Watanzania zaidi ya milioni 60 kwenda 70 waliopo nje. Tunayaleta matatizo katika Serikali yetu. Nami niseme, nina imani nawe, ninaamini kwenye daraja hilli utakuwa kiungo kizuri cha kuweza kutufikishia maendeleo kwa wananchi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hakuna asiyejua kwamba lengo la kuja humu kusema ni kuishauri Serikali na Serikali kupokea mawazo yetu. Leo tunaposema huko nje Watanzania wote wanafahamu tuna changamoto kubwa ya ukatikaji wa umeme, hakuna asiyejua. Kila mahali umeme ni changamoto. Kwa hiyo, tunapokuja humu kuishauri Serikali, basi isitokee mtu akaona kama tunamwonea, hapana. Tunatoa tu maelekezo ayafuate mawazo yetu ili tukatatue tatizo na kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimeanzia hapo kwa sababu gani; leo tumekuja hapa kuchangia ripoti ya kamati mbili za *PAC* na *LAAC*. *TANESCO* wana matatizo makubwa sana, leo tukisema *TANESCO* kwenye ripoti ya *CAG* inasema imetengeneza faida mwaka 2019/2020 walitengeneza faida ya bilioni 45, kama waliweza kutengeneza faida kwa nini bado kuna changamoto?

Mheshimiwa Spika, nimnukuu Mheshimiwa Waziri alisema hapa, tuna matatizo mengi. Mchangiaji mmoja hapa

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

amesema ukiangalia *assets* na madeni ya *TANESCO* ukiyalinganisha hakuna *TANESCO*. Kwa hiyo, tumekuja kutoa changamoto zilizoko katika Shirika letu la *TANESCO* watusikilize na changamoto ni kuipitia hii Ripoti ya *CAG* itawaonesha nini changamoto inayoikabili *TANESCO* kuliko kuanza kukimbia. Kama hukunitaka kwa nini unataka nini?

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu ambaye anataka cheo cha mwenzake hapa. Kwa hiyo, tunapokuja humu tunaleta mawazo ya wananchi. Tunapokuja humu tunaishauri Serikali iende ikafanyie kazi. Kwa hiyo, nilitaka niseme *TANESCO* bado changamoto ipo na tusipokwenda vizuri bado tutaendelea kuwa na changamoto.

Mheshimiwa Spika, *CAG* amebainisha baadhi ya changamoto, lakini sasa ukija kuangalia inawezekana wamepikapika tu hesabu kuonesha wana faida, ili waturidhishe watanzania, lakini hakuna kinachoendelea katika shirika letu ndio maana hata wanaongeza ghamra za kuunganisha umeme. Kwa hiyo, Serikali ichukue hatua ikiwemo kusikiliza na kufuatilia nini *CAG* aliandika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto za *TANESCO*, lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana. Wote sisi Wabunge kuna miradi inayoendelea ya *REA*, hii miradi inayoendelea ya *REA* fedha zinazotumika ni za watanzania wote, tumeongeza fedha kwenye tozo za mafuta kwa lengo la kufikisha huduma za umeme katika vijiji vyetu.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Venant Daudi, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

TAARIFA

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, nataka nimpe Taarifa mchangiaji anayechangia sasa kwamba, anatoa mchango mzuri sana unaohusu nishati,

lakini hapo najua ni hoja ya kamati, lakini Waziri wa Nishati wala Naibu wake hayupo. Kwa hiyo, wakati unachangia ufahamu hilo, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nilishawahi kutoa ufanuzi huko nyuma, nirudie tena; Serikali iko Bungeni. Serikali iko Bungeni na kwa kuwa, Serikali iko Bungeni tusiwe na wasiwasi mawazo yetu tunayoyatoa yote yanapokelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Venant Daudi malizia mchango wako.

MHE. VENANT D. PROTAS: Mheshimiwa Spika, nikushukuru, ninafahamu watapitia hata kumbukumbu za Bunge, watayakuta haya.

Mheshimiwa Spika, kuna kiradi inayoendelea katika maeneo yetu, miradi hii gharama inayotumika au fedha zinazotumika ni za watanzania. Leo, kama kamati, tulikwenda kutembelea miradi mitatu katika mikoa mbalimbali, tuliyoyakuta huko Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda kukuta mkataba unasainiwa, labda mradi utatekelezwa kwa bilioni 30, wamefanya tathmini *TANESCO*, anakuja *REA* anabadilisha tena anasema mlikosea kufanya tathmini nitatekeleza kwa bilioni 37, inaongezeka bilioni saba zaidi ya asilimia 20. Kama yule wa kwanza alibaini biloni 30 kwa nini huyu anakuja miezi mitatu baadaye bilioni saba zaidi?

Mheshimiwa Spika, mimi nikuombe, dakika moja kwa kumalizia, nikuombe kuititia Bunge lako iundwe kamati maalum ambayo itakwenda kuchunguza miradi ya *REA* tangu tumeanza na ilete ripoti katika Bunge lako tukufu. Ahsante nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa sababu ya muda shukrani zote zimeshakutosha. Nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia katika Kamati yangu ya *LAAC*.

Mheshimiwa Spika, uhai na uchumi wa nchi yetu umelalia kwenye halmashauri zetu na Ushahidi ni fedha zinazopelekwa huko ni mabilioni ya fedha za watanzania zinapelekwa kwenye halmashauri. Kwa sababu, fedha nydingi zinakwenda huko tunategemea kwamba, usimamizi mkubwa wa fedha na wa makini sana ufanyike huko na watu wanaohusika na usimamizi huu ni maafisa masuuli wakuu katika halmashauri zetu ambao ni wakurugenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, tumeoji wakurugenzi wengi takribani 40 kwa mfano, lakini wakurugenzi hawa wanatofautiana kwa kiasi kikubwa sana katika uwezo wao pale wanapojobu maswali yetu na wanapowakilisha halmashauri zao. Sitaki kuwa na mashaka na uteuzi na mchakato wa jinsi wanavyopatikana, lakini ningependa kushauri kwa sababu, ya umuhimu sana wa watu hawa wanaoitwa wakurugenzi wa halmashauri, maafisa masuuli wa fedha nydingi za watanzania, ningeshauri kwamba, uteuzi wao uanzie kwenye usaili.

Mheshimiwa Spika, wako watanzania wengi sana wana uwezo mkubwa, wafanyiwe usaili wa kutosha, wafanyiwe *vetting*, baada ya hapo Mheshimiwa Rais sasa akabidhiwe kundi kubwa la watu kama 300 hivi afanye mamlaka yake ya uteuzi ndani ya watu ambao wamefanyiwa usaili, ili tupate watu watakaosimamia fedha hizi. Watu ambao ni makini kwa sababu uhai wa watanzania uko kule kwenye halmashauri ambako kuna fedha nydingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upungufu wa watumishi kwenye halmashauri. Kama nilivyosema fedha nydingi ziko kule, lakini watumishi ni wachache sana, watu wanakaimu nafasi wanapewa fedha za *acting allowance*, kuna watumishi wanadai mpaka bilioni 80 tumewahoji kwa ajili tu ya ku-*act*,

fedha hizi ni sawa na *pensionya* mtu mwengine. Kwa nini watu wasiajiriwe na watu wenye uwezo wapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Serikali inadhani inaepuka mzigo wa ajira ikumbuke kwamba, inapoteza fedha nyngi zaidi kwa kutokuajiri watu ambao wana uwezo na kuweka watu wanao-*act* kwa kufanya maamuzi ya mabilioni ya watanzania ambayo yako kule. Kwa hiyo, niishauri Serikali, fedha nyngi inapeleka, isikwepe mzigo wa kuajiri watu wenye uwezo ili wasimamie fedha hizi tuweze kuona tija ambayo ya fedha hizi Mheshimiwa Rais anazipeleka kila siku kule katika halmashauri zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la watumishi pia kukaa maeneo, sehemu moja. Unakuta mkuu wa idara ana miaka kumi katika eneo moja; ameshakuwa sawa na wakulima, ameshakuwa saw ana wafanyabiashara wa eneo husika, amejisahau kabisa kwamba, yeye ni mtumishi wa umma kwa sababu, ameshakaa muda mrefu. Matokeo yake anaingia kwenye migogoro ya ardhi, anaingia kwenye migogoro mingine, matokeo yake kunakuwa kuna matatizo mengi kwenye halmashauri ambayo yanakuja kama hoja kwa CAG. Kwa hiyo, ningeomba tatizo hili Serikali pia, iliangalie kwa macho mawili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja zangu hizi sasa nikupongeze kwa sababu, muda bado ninao, kwa kuchaguliwa. Na tunakushukuru ni Spika wa viwango, taratibu na kanuni zimejaa kwenye kichwa chako. Tuna hakika mambo yatakwenda vizuri katika Bunge letu. Ahsante sana, naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, Mheshimiwa Annastazia James wambura ajiandae.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Namshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia uzima kuweza kufika siku hii ya leo, lakini niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote mbili wakiongozwa

na wewe Mheshimiwa Spika kwa kweli, nimewaona *super woman*, mambo yanavyokwenda ni moto tukiongozwa na Mama yetu Samia Suluhu Hassan, Rais wa nchi yetu. Na Wabunge wanaume wanaona mambo yanavyokwenda, nchi iko kwenye mstari. (*kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu umesema Serikali ipo nitajikita zaidi kwenye Wizara ya Kilimo. Sitazungumza kwa sababu siwaoni, lakini kwa sababu umesema Serikali ipo naendelea.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi kwenye mradi wa ujenzi wa vihenge na maghala ya kuhifadhi nafaka. Kwenye mradi huu Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliingia kwenye mkopo na Serikali ya Jamhuri ya Poland, mkopo wa dola za kimarekani milioni 55, ni jambo jema kwa sababu, lengo liliikuwa ni kwenda kujenga hayo maghala. Tulipata wakandarasi wawili kwenye huo mkataba. Wakandarasi hao wanatoka Poland, masharti yaliyopo kwenye mkataba vifaa vyote vitoke Poland. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mkopo huu ulikopwa lini; tarehe 28 Septemba, 2015, nataka Wabunge tuangalie hapo hicho kipindi ni cha uchaguzi na mara nyingi mambo yanaharibika sana hapo kuanzia kwenye halmashauri, ukifuatilia hiyo *trend* utaona kuna jambo fulani hapo. Mikataba hii inatufundisha nini; kabla sijaenda kwenye kushauri tunamuona Mheshimiwa Rais anazunguka huko kwa ajili ya kutumia *resources* tulizonazo kwenye nchi zitusaidie kama Taifa. Lakini asiposhauriwa vizuri kwenye mikataba ya hovyo lazima ataingia chaka kama hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nini wajibu wetu kwenye hili jambo; mkandarasi kati ya hao wawili ambaye alikuwa anatekeleza mradi Dodoma, Shinyanga, Makambako, Songea na Mbozi, ambaye alipata dola za kimarekani milioni 33.14 amefika asilimia 73 akaja kuomba nyongeza ya dola za Kimarekani milioni 12. Hakuna nyongeza ya aina hiyo! (*Makofi/Kicheko*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Waziri wetu wa Kilimo pamoja na *NFRA* waligoma baada ya kuona hilo jambo, lakini wao hawakuingia kwenye huo mkataba, walioshiriki ni Wizara ya fedha. Nawashukuru kwa busara yao waliyoifanya, lakini huyu bwana kwa sababu anajua kuna nini nyuma ya pazia na yeye ameweeka mguu chini kwamba, hataendelea na hiyo kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa nini kinatokea; amegoma akaondoka, leo mkitaka mumchukulie hatua yoyote fedha hizo ambazo tulikopa ziko Poland. Ni kitu gani hiki kwenye Taifa letu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni mambo ambayo hayafurahishi hata kidogo. Kuna haja sasa ya *CAG* kwenda kufuatilia vizuri nini kilitokea kwenye huo mkataba. Na mikataba ya aina hii lazima sasa kuna haja ya kuwa wazi tulangalie mapema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nashauri kabla ya kuingia kwenye mikopo ya aina hii kwanza waangalie sifa za hiyo nchi. Na huko nyuma iliwhahi kufanya hivyo kwa nchi ngapi?

Je, imefanya vizuri au imefanya vibaya? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, wote tunajua sifa za nchi ya Poland, lakini hayo mengine hatutaspera, tuache hapo, lakini tunaamini huu mkataba ulipitiwa na wasomi wetu tena wanasheria. Unakubalilje mkataba wa aina hii kuliingiza Taifa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, leo umenikopesha fedha halafu fedha unazo wewe mwenyewe. Vihenge havijaisha mpaka leo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye haraka iwezekanavyo kumaliza mgogoro huu unaoendelea kati ya huyo mkandarasi, ili kazi imalizike. Tofauti na hapo tutaiingiza nchi kwenye Mahakama za kimataifa. Hamuwezi kujua kiburi cha huyu mtu kinatoka wapi? (*Makof!*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya dakika tano, nitazungumzia tena deni la bilioni 166 kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu ambalo *NFRA* wanadai. Tuliomba fedha kile kipindi imetokea tafrani kwa ajili ya zao la mahindi. Serikali ikaja hapa kuititia Waziri Mkuu kwamba tumepeewa fedha bilioni 50, tukaona ni jambo jema, lakini kumbe ule ni mkopo amekopa *CRDB*. Kukopa *CRDB* sio jambo baya, sasa kama *NFRA* wanadai Ofisi ya Waziri Mkuu bilioni 166 kwa nini wasingelipa sehemu ya deni badala ya kwenda kukopa benki ya *CRDB*? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nakushukuru. Mengine tutaendelea kushauri, ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote niungane na Wabunge wenzangu kukupongeza wewe pamoa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwa asilimia 100, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati hizi mbili ambao kwa kweli, wamefanya kazi nzuri sana katika kuwasilisha taarifa, lakini pia kamati zimechambua kwa kina sana mambo mbalimbali ambayo yanaonekana na haya ndio machache ambayo yameweza kuja ambayo mimi naamini kwamba, yana vitu vya msingi ambavyo Serikali inatakiwa iende ikavifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuunge mkono maazimio yaliyoko katika taarifa hizi, ili Serikali iende ikayafanyie kazi. Na ikiyafanya kazi ituletee mrejesho namna ilivyotekeleza haya maazimio. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama taarifa zilivyobainisha, yapo maeneo ambayo yamekuwa yana matumizi yasiyordhisha. Maeneo ni mengi, lakini katika Serikali ukichukua Wizara, ukachukua mashirika, ukachukua idara zinazojitegemea, ukachukua wakala, maeneo mbalimbali yanaonekana kuwa na viashiria vya matumizi yasiyordhisha. Na maeneo hayo ni pamoja na maeneo ya utengenezaji wa mifumo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mifumo mingi imekuwa ni kichaka ambacho kinatumika katika matumizi mabaya ya hela za umma. Kwa hiyo, nitaliomba Bunge lije liangalie katika taasisi zote mifumo yote ambayo tumeitengeneza kwa muda wa miaka mitano au kumi mpaka tulipofika tumetumia fedha kiasi gani? Na hiyo mifumo imeleta nini kwenye Taifa hili? Hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo lilmekuwa ni shida ni kwenye eneo la manunuzi na usimamizi wa mikataba. Kwa sababu ya muda, sitaweza kuyazungumza kwa undani. Lakini katika hili eneo ndio maana tumeona kwa mfano bandari peke yake, hiyo tumeweka ni mfano tu, bandari peke yake mifumo bilioni 17 na kitu zimetumika, lakini mifumo ile haina tija. Sasa hivi wameondokana na mifumo hiyo, mifumo haionani, sasa wanakuja na mfumo mwengine, tena zinahitajika hela nytingine, sasa hii kwa kweli haikubaliki. Na taasisi nytingine nydingi ambazo mimi kwa sababu ya muda sitaweza kuzisema. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini hebu tuje kwenye hali halisi, *TRA* wanaonekana kwenye makusanyo wana triliuni 360 ambazo ziko kwenye Bodi ya Rufaa ya Kodi. Hivi ni sura gani inayoonekana kwenye Serikali?

Mheshimiwa Spika, yani tunaposema Serikali inadai hizo hela, nimeliangalia hili deni mwaka 2015 mpaka 2016 deni lilikuwa ni *1.3 trillion*. Mwaka 2017 deni lika-*shoot* mpaka triliuni 360; nazungumzia triliuni ambazo ukizigawa ni bajeti ya nchi hii ya miaka 10 hizo hela kama zingekusanya, lakini hebu tujiulize hivi hili deni lina uhalsia? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kwenye vitabu vyote vya *TRA*, vitabu vya Serikali, vitabu vya kiuhasibu, hili deni halipo. Na hili deni linatokana kwa kiwango kikubwa na makinikia, lile deni la makinikia. Sasa kama tumefanya majadiliano na zile kampuni zinazohusika tumemaliza, hili deni nashauri Serikali iangalie uwezekano ilifute linachafua taswira nzuri ya Serikali. Kwa hiyo, nafikiri hili lazima waliangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili; yapo mashirika mengi ambayo yanaonekana yana upungufu mkubwa, yana shida ya fedha. Nianze kwa mfano Shirika la Ndege linaonekana lina upungufu mkubwa, lina madeni bilioni 246 ambazo tunafikiri Serikali iangalie uwezekano wa kuiongezea ili mizania ya hesabu ikae vizuri, lakini kuna *TANESCO*. *TANESCO* kuna bilioni 493.6, lakini *TANESCO* hiyo inadai kwa wateja bilioni 422, sasa mizania yake haijakaa vizuri. Ukienda *TPDC* wanaidai *TANESCO* fedha nyngi sana, lakini kwenye *TPDC* pia kuna deni la ujenzi wa bomba la mafuta ambalo Serikali inalipa tayari, lakini kwenye vitabu halifutiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Serikali, haya yanachafua. Ni vizuri mkaangalia namna ya kusafisha vitabu vikae vizuri, mizania zile zikae vizuri, kuliko hali iliyoko sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, waliunganisha kweli benki wakaamua kuunganisha, hivi Serikali unapochukua benki inayofanya vizuri unaunganisha na benki isiyofanya vizuri, lengo linakuwa ni nini? Halafu unawachukua wale wafanyakazi walioshindwa kuiendeleza benki, walioharibu, unawaleta kwenye benki inayofanya vizuri. Hii haijakaa vizuri kabisa. Halafu unachukua madeni chechefu yaliyoshindikana kulipwa huko, unayaleta kwenye benki inayofanya vizuri, maana yake sasa mizania ya benki inayofanya vizuri sasa inaharibika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri hili siyo lengo, lengo la Serikali inawezekana lilikuwa zuri, zile benki zenyé madeni chechefu waziundie kampuni yao huko zinazofanya vizuri

waziache zifanye vizuri. Hiyo itasaidia sana na naona kuna hizo sitaki kuzitaja kwa sababu ya muda, naona mambo karibu yamekwisha, lakini nataka niseme moja kwa dakika moja.

Mheshimiwa Spika, kuna benki zinazodaiwa, kuna Serikali inadaiwa trillioni 1.1 na *NSSF*, lakini Rais wetu amefanya kazi nzuri. Toka miaka nenda rudi tunadai ule Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali zaidi ya trillioni mbili na kitu, ametoa *non cash bond* kwenye hiyo, amenusuru.

Mheshimiwa Spika, sasa tunamwomba na *NSSF* aangalie na haya mashirika mengine nayo aangalie, lakini hii tume ya madini ya bilioni 156 wafanye ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa sasa hapo tena muda umetuacha kidogo.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, naomba wafanye *reconciliation*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote na Mungu awabariki. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana upande wa Serikali nadhani kuna haja ya kutuelimisha sisi Wabunge kwa ujumla tu, hii *non cash bond*, kwa sababu hapa kuna mchangiaji aliyeppita ambaye mchango wake tulivyouelewa ulikuwa kama unaonesha hii *non cash bond* haiondoi tatizo bado linakuwa palepale. Saa hizi Mheshimiwa Mbunge mwininge anasema tutumie huo utaratibu kupunguza hizo changamoto.

Kwa hiyo, nadhani kuna tatizo la uelewa mahali kuhusu hizo *non cash bond*. Hivyo, Serikali mwangalie namna Wabunge hapa tunavyoweza kupata uelewa wa namna hizo *non cash bond* zinavyofanya kazi.

Mheshimiwa Anastazia James Wambura atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mollel na Mheshimiwa Patrobas Katambi ajiandae.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii. Nianze kwa kukupongeza wewe pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuaminiwa na Kamati Kuu, lakini pia kwa kupitishwa kwa kishindo na Bunge lako hili Tukufu. Nimwombe Mwenyezi Mungu aendelee kuwasimamia na kuwaongoza katika majukumu yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nipongeze pia *CAG* pamoja na ofisi yake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, lakini pia nadhani wajumbe wa Kamati ya *LAAC*, *PAC* na *PIC* wanafahamu namna ambavyo mafunzo yake yametusaidia na sasa tumekuwa kama ni ma-*CAG*wadogo. Niwapongeze pia Wenyeiti wetu wa Kamati hizi mbili, wame-*present* vizuri sana hoja za Kamati. Kwa hiyo nimesimama hapa kuunga mkono hoja za Kamati zote, hizi mbili kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa na machache sana ya kuongezea katika taarifa ya *LAAC*. Nianzie na ubora wa majengo; kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* tumekuwa tukipata taarifa mara kwa mara na hasa kwa hii taarifa ya mwisho aliyoileta *CAG*, kuna baadhi ya majengo ambapo akikagua utakuta kuna nyufa katika kuta na katika sakafu na hii haileti afya katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, ukichunguza sana utakuta sababu mojawapo ni kwamba baadhi ya halmashauri hazina Wahandisi wa kutosha, lakini hata wale Wahandisi ambao wapo wanakuwa hawana vitendea kazi, kwa mfano, usafiri. Kwa hiyo utakuta kwamba, hasa kwenye hii miradi ambayo inatumia *force account*, kwa kweli ni shida kwa sababu wanajenga tu wale mafundi ambao wameaminiwa, lakini Wahandisi wetu wanapokuwa wakihitajika kukagua, hawana usafiri, kwa hiyo hawafiki pale kwa wakati. Unakuta *order* imetolewa kwamba tunataka ndani ya mwezi mmoja

wanafunzi wawe wameshaingia darasani, kwa hiyo wanaamua tu leo ameweka msingi, anapandisha tofali, moja kwa moja anaendelea lenta na kupaua, kwa hiyo yanakuja kutokea madhara kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nitoe ushauri tu kwa Serikali kwamba sasa ihakikishe kwamba kunakuwa na Wahandisi wa kutosha, lakini vile vile wapatiwe vitendea kazi kama usafiri ili waweze kwenda kwa wakati, wafanye ukaguzi kwa wakati na vilevile kutoa ushauri ili kuweza kupata majengo yenye ubora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo tena hoja yangu ya pili ambayo ni ya mikopo ambayo inatokana na asilimia kumi ya fedha za ndani kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu. Niseme tu maswali ya jana na leo katika eneo hili ni *Indication* tosha kabisa kwamba kuna tatizo katika eneo hili la mikopo. Tatizo lipo na panahitajika ufuutiliaji wa karibu.

Mheshimiwa Spika, zipo halmashauri ambazo zinafanya vizuri katika eneo hili kwa upande wa marejesho ya mikopo na utakuta kuna wengine wanaorodhesha vizuri kabisa kwamba mikopo iliyorejeshwa kuna kiasi kadhaa ambacho kimepelekwa tena kwenye vikundi vingine. Hata hivyo, kuna baadhi ya halmashauri ambazo zinahitaji uangalizi na ufuutiliaji wa karibu kabisa ili kuweza kujua hizi fedha ambazo zimerejeshwa zinakwenda wapi na zinakopeshwa vipi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe tu Ofisi ya CAG kwa sababu mpaka sasa hakuna utaratibu wa kuzikagua hizi fedha ambazo zimerejeshwa, hatujaona utaratibu huu. Kwa hiyo niombe Ofisi ya CAG ifanye ukaguzi kuangalia hizi fedha ambazo zimerejeshwa zinakopeshwa na zinakopeshwa kwa namna gani na atoe taarifa ili kusudi Kamati iweze sasa kupata msingi wa kuhoji hizi halmashauri na kujua nini kinachoendelea. Niombe pia mamlaka husika itoe *format* katika halmashauri, namna bora ya kuweza kuzitolea taarifa hizi fedha ambazo zimekopeshwa.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa halmashauri niombe halmashauri zijifanyie tathmini zenyewe, je, hii mikopo wanayotoa ina tija? Niseme tu kwamba, kama mikopo hairejeshwi, ina maana kabisa na ni *indication* moja wapo kwamba hakuna tija katika hii mikopo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi tuna watumishi wa aina mbalimbali katika halmashauri kuna Maafisa Biashara, lakini utakuja kushangaa kwamba, unaona wanawake wengi na vijana na watu wenye ulemavu, ambao wamekopa wanajikita kwenye biashara za uchuuzi wa bidhaa ya aina moja katika eneo moja na utaona kwamba hawafuati zile *principle* za *demand and supply* na matokeo yake ni kwamba wanakosa wateja na mwisho wa siku wanakuwa wameshindwa kurejesha mikopo.

(Hapa kengele illia kuashirilia kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Kengele ya pili ya kwanza?

SPIKA: Kengele ni moja tu Mheshimiwa.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba niombe halmashauri zetu ziwe *intergreted*, zishirikiane ili kusudi kuweza kuwasaidia hawa wanaochukua mikopo tuweze kutimiza malengo ambayo tunayakusudia katika utoaji wa hii mikopo.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.
(Makof)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Mollel Godwin atafuatiwa na Mheshimiwa Patrobass Katambi na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, ajiandae.

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, nijikite kwenye ripoti ya Kamati kwenye eneo la Bohari ya Dawa. Kwanza

niwashukuru kwa sababu wameonyesha kwamba hali ya dawa imeboreka na hasa baada ya Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kupeleka bilioni 333.8, lakin kuweka utaratibu ambao kila mwezi bilioni 15 zinakwenda Bohari ya Dawa na sasa hali inaendelea kuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, vile vile wamezungumzia kutokuwepo na viwanda vyta kuzalisha dawa. Kwa rekodi nzuri ya Bunge kwa hii miezi ambayo Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan amekuwepo madarakani tumekwenda sasa kujenga Kiwanda cha Kuzalisha Dawa kule Njombe na kimefikia asilimia 70 ya ujenzi na kitaenda kuzalisha vidonge vyta kutosha nchi nzima kwa siku mbili. Pia kinajengwa kiwanda cha kuzalisha *gloves* ambacho kitakidhi 85% ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Kiwanda chetu cha Keko kimeenda kufufuliwa na sasa kinafanya kazi na kinazalisha zaidi ya dawa 12 kwa sasa. Wakati huo huo kimeanzishwa Kiwanda cha Kuzalisha Mionzi Dawa ambacho kiwanda hicho kwa Afrika Mashariki ni sisi peke yetu tutaenda kuwa nacho na kwa Afrika kuna nchi tano tu ambazo zinamiliki kiwanda hicho. Maana yake ni nini, tulikuwa tunaagiza dawa kutoka Afrika Kusini, sasa tutakuwa tunapata dawa hapa hapa Tanzania na Nchi za Afrika Mashariki zitakuwa zinaagiza hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia suala la deni la *MSD*, ni kweli kulikuwa na deni la bilioni 281 na kulikuwa na kazi inayoendelea ya kuhakiki deni hilo. Kwa sababu kila wakihakiki wanakuta kuna kiasi kikubwa cha fedha ambacho kilikuwa siyo halali, kimeshahakikiwa kama milioni 90 na tayari zimelipwa bilioni 39. Wakahakiki tena bilioni 126 wakakuta kuna madeni feki bilioni 4.7 na hii bilioni 126 sasa inaenda kulipwa ambazo zimehakikiwa tayari.

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia eneo la Bohari ya Dawa kwa maana nyingine huwezi kuzungumzia bila kuzungumzia uwajibikaji na utendaji mzuri kuanzia juu mpaka kufika chini. Nakumbuka Wabunge tuliripoti hapa kwenu na

tukawaeleza jinsi ambavyo kulivyokuwa kuna upotevu wa dawa kwenye maeneo yetu. Tukitaka kweli tufike mahali dawa zipatikane kwa wingi, ni muhimu sana hili suala la kusimamia dawa liwe ni shirikishi, maana yake sasa tunatakiwa twende kujua vyanzo ambavyo vinafanya dawa zipatikane kwenye hospitali zetu za halmashauri na sehemu zingine na vyanzo kuna *basket fund*, kuna *own source* na *MSD*.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati mwingine tulivyowaelezea upatikanaji wa dawa hapa kwetu jinsi tulivyoibowi, tulichotaka ni kwamba tunataka tushuke mpaka chini Baraza la Madiwani na hata vituo vyetu kule chini watendaji na Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani wawe ni sehemu ya kusimamia uadilifu huo na kupata ripoti zote zinazotokana na dawa ili tuweze kusimamia kwa umoja wetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwa upande wetu hayo ndio ambayo yalikuwa yanatuhusu sisi na majibu yake ni hayo. Niseme tu kwenye eneo hili la kuzalisha dawa maana yake tiba mionzi, Kamati yetu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliomba ikifika asilimia 80 ya ujenzi wa hicho kiwanda watembelee na asilimia 80 ya hicho kiwanda imefika na tumeshaandika barua kwako kwa ajili ya Kamati ya Bunge kutembelea kukiangalia kile kiwanda.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Patrobas Katambi atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwanza nikupongeze kwa sababu baada ya wewe kuchaguliwa kwa kishindo na Chama cha Mapinduzi, lakini pia kwa kuidhinishwa na Bunge hili Tukufu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja katika eneo la hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa

Wabunge. Nzungumzie kuhusu suala la Kiwanda cha Mbigiri, niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba katika uwekezaji ambao unafanya na Serikali katika mifuko hii kuna sera ambayo inaongoza uwekezaji wa Mifuko lakini pia tunayo sera ya uwekezaji ambayo ndiyo msimamizi mkuu wa Mifuko hii. Miongozo kabla ya uwekezaji ni lazima ipitishwe na Benki Kuu ya Tanzania na taratibu zinaelezwa na nini kinafanyika kabla ya uwekezaji. Mwongozo unaeleza lazima ufanyike utafiti na upembuzi ili kubaini au kugundua kama kuna *economic viability* yaani kuangalia faida katika uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili linaangaliwa ni katika sasa kufanya uamuzi wa kwamba uwekezaji ufanyike au usifanyike na kwa kuzingatia *required rate of return* ambayo inaelezwa kwenye mwongozo huo na kwa mujibu wa maelekezo mazuri yanayofanyika na Benki Kuu ya Tanzania na kigezo cha kufanya hivyo kama itaonekana kutakuwa na tija ndipo uwekezaji unaweza ukaendelea kwa kuzingatia pia miongozo ambayo inatolewa na *Social Security Investment Guidelines*.

Mheshimiwa Spika, sasa *Social Security Investment Guidelines* ndiyo zingatio la usimamizi wa Serikali katika kuhakikisha chochote kinachowekezwa kinachotoka katika Mifuko hii kiende kuleta tija. Kwa kweli niishukuru sana Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, ya Awamu ya Sita, amekuwa akitupa miongozo kwa wakati wote kuweza kuhakikisha kwamba, tunayatekeleza majukumu kama jinsi ambavyo ilikusudiwa. Nini kilitokea katika kiwanda hiki cha Mbigiri? Changamoto zilizojitokeza baada ya tafiti hizo na kuruhusiwa kuanza, kiwanda hiki ndani ya miezi 16 kilikuwa tayari kilishaanza kufanyakazi by mwaka jana mwezi Agosti kingekuwa kimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu sote ni jambo la janga la dunia nzima, baada ya kuanza *procurement procedures* zilifika zikachelewa kwa sababu ya uwepo wa janga la *Covid* mashine zikachelewa kuingia na kufikia mwezi Agosti na sasa hivi tunavyozungumza tayari

mashine zimekwisha kuingia. Kwa hiyo tunasubiri by mwezi Agosti mwaka huu pengine tayari waende kwenye hatua ya *mobilization* na *installation* kwenye eneo hilo la kiwanda.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo mkataba huu tumeendelea kuhakikisha kwamba tunasimamia ili uweze kutekelezwa kwa kadri agizo na ni siku tatu zilizopita Mheshimiwa Waziri wangu Profesa Ndalichako alikuwa kwenye kiwanda hicho na kuangalia tija namna gani Serikali itaenda kupata faida zaidi. Kwa hiyo tunalisimamia kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa ni kuhusiana na hasara ambayo wakulima waliipata katika kilimo walichokifanya cha miwa. Sambamba na hilo tukumbuke Serikali pia nayo ililima mashamba, miwa hii yote kwa pamoja kwa maelekezo mazuri ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan na uongozi wetu katika Wizara na usimamizi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ilibidi Serikali ifanye uamuzi wa kutafuta soko na kwenda kuuza katika viwanda vingine na miwa hii ilinunuliwa na faida ilipatikana zaidi ya bilioni moja. Kwa hiyo ilikuwa ni katika hatua ya kupunguza hasara ambayo ilijitokeza kutokana na changamoto tulizozipata.

Mheshimiwa Spika, hoja nyngine ilikuwa ni kuhusu madeni ya Serikali katika Mifuko. Katika hili turudi katika hoja za CAG, tulizichukua hoja 12 za Ofisi ya CAG na tayari Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu wamekwisha kuanza utekelezaji wake na moja ya utekelezaji wa hoja hizo 12 za CAG, tayari zaidi ya shilingi trilioni mbili zimelipwa kwenye Mfuko wa PSSSF na Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan katika kupitia hiyo *cash bond*.

Mheshimiwa Spika, pia kulikuwa kuna hoja nyngine kwa kadri ya maelekezo ambayo umetupa kwamba tujielekeze katika hoja. Suala la fedha ambazo Ofisi ya Waziri Mkuu zinazosemekana bilioni 56 zinazodaiwa kwa kile alichokisema Mheshimiwa Mbunge kwamba zinadaiwa. Ni kweli fedha hizo zilichukuliwa kwa utaratibu wa kuokoa hasara ambayo kubwa walikuwa wanaenda kuipata

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wakulima. Ndipo Serikali ikalazimika kuchukua hatua za makusudi kuweza kuhakikisha wakulima hawa mazao yao hasa yale mahindi yananunuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, utaratibu kama jinsi ambavyo mikopo mingine inalipwa, Serikali inaendelea kulipa deni hili na Mheshimiwa Aida Khenani atakuwa shahidi hata yeye mwenyewe kuna maeneo ambayo pengine atakuwa na mkopo na mkopo unategemeana na masharti na vigezo. Kwa hiyo huwezi ukalipa kwa mkupuo, kwa hiyo hili suala tayari Serikali inalipa na niwaondoe shaka Serikali ya Awamu ya Sita katika kila hoja zinazotolewa na Wabunge na hoja zinazotolewa na Kamati za Bunge, tunazitekeleza usiku na mchana kuhakikisha kwamba maagizo ya Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan yanatimizwa. Ahsante sana. (Makofii)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Mheshimiwa George Simbachawene ajiandae.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya LAAC na Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni, mapendekezo na michango muhimu sana. Serikali imeichukua michango yote na tumeipokea kwa mikono miwili tutakwenda kuitekeleza moja baada ya nyininge. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nikianza na hoja ya matumizi ya fedha mbichi. Serikali ilishaweka utaratibu na miongozo kwamba ni marufuku taasisi yoyote ya Serikali kutumia fedha kabla ya kupeleka benki na tumeendelea kuboresha mifumo ya kielektroniki kuhakikisha mapato yote yanapelekwa benki na kutumika baada ya kupelekwa benki.

Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya watumishi bado wamekuwa na utaratibu wa kutumia fedha kabla ya

kupelekwa benki na tutaendelea kuchukua hatua kuhakikisha tunadhibiti matumizi ya fedha mbichi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kufutwa kwa baadhi ya miamala. Serikali hivi sasa tumewekeza sana kuboresha mifumo ya kielektroniki, lakini tunakwenda kuiboresha kuweka *system* ambazo zitadhibiti wale *operators* wasiwe na *access* ya kufuta miamala kwa manufaa yao binafsi. Kwa hiyo, hili Serikali tumelichukua, tunakwenda kuweka mifumo hiyo kudhibiti wale ambao wana nia mbaya ya kutumia vifaa hivyo kufuta miamala.

Mheshimiwa Spika, pia tutaweka *bureaucracy* ili Maafisa Masuhuli wawajibike kufuta miamala na siyo kila *operator* awe na *access* ya kufuta hiyo miamala.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na *Force Account* kuweka kiwango, ni kweli tuliweka utaratibu majengo ya ghorofa yanakwenda kwa Makandarasi, yale ya chini tunatumia *Force Account*. Hata hivyo, wazo ni zuri, tumelipokea, tutakwenda kuweka kiwango ambacho kitakuwa cha *Force Account* na kiwango ambacho kitakuwa lazima kitumie *contractors*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Wahandisi, Rais wetu ameajiri kwa dharura Wahandisi 246 mwezi Oktoba, 2021 kwa ajili ya Halmashauri zote 184 na mikoa yetu yote na zoezi hili ni endelevu, tutaendelea kuboresha ikama ya Wahandisi ili wasimamie vizuri miradi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na udhahifu wa makusanyo ya mapato ya ndani, ni wajibu wa Halmashauri zote kuhakikisha wanakusanya mapato ya ndani kwa 100% na kuhakikisha fedha zile zinapelekwa kwenye miradi ya maendeleo ya wananchi yenyе tija na kukamilisha miradi ile kabla ya kuanza miradi mingine. Kwa hiyo, tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge na Kamati na Serikali tumeanza kutoa maelekezo hayo kuhakikisha hili linatekelezwa na fedha hizo zinapelekwa kwenye miradi ya maendeleo ikiwemo 40%, 60%, na 10%. (*Makofi*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la Wakuu wa Idara kukaa kwa muda mrefu katika Halmashauri zetu; tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeanza kufanya tathmini nchi nzima kwa Wakuu wa Idara wote waliokaa kwa muda mrefu na tumeanza na Waweka Hazina, Maafisa Utumishi, Wakaguzi wa Ndani pamoja na Maafisa Mipango. Utaratibu huo ni endelevu. Tunataka tuhakikishe Wakuu wa Idara hawa *overstay* kwenye vituo vyao ili kuepusha kuwa na mazoea kufanya kazi na baadaye kuwa na mianya ya upotetu wa fedha za Serikali. Kwa hiyo, suala hili tunakwenda kulifanyia kazi na tutahakikisha tunafanya hili zoezi kuwa endelevu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake niseme Serikali tumepokea maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge na tutakwenda kuyafanyia kazi ili kuhakikisha mamlaka ya Serikali za Mitaa zinatoa huduma na kupeleka miradi ya maendeleo kwa wananchi kwa kadri ya malengo ya Serikali kwa manufaa ya wananchi wenzetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, namshukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa George Bonifance Simbachawene, watoa hoja mjiandae.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa nafasi na pili naishukuru Kamati ya PAC kwa maoni. *Specifically*, kwenye eneo la kilimo kulikuwa kuna hoja kubwa mbili. Moja ni hoja ya vihenge na pili ni kuhusu NFRA.

Mheshimiwa Spika, Serikali baada ya kuona mradi wa vihenge umeanza kusuasua na kumekuwa sintofahamu, Serikali iliunda *Government Negotiating Team* na mwaka 2021 mimi mwenyewe nilishiriki; na wakati huo, Mheshimiwa Kitila akiwa Waziri wa Viwanda ndio alikuwa *leader* wa ile Kamati na mpaka sasa hivi ile Kamati ipo kazini, tumekutana na wenzetu wa Poland, tumekaa kujadiliana nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kutakuwa hakuna *overspending* juu ya *framework* iliyokuwepo awali. Siyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wala *beneficiary* ambaye ni *NFRA* haaja-violet mkataba kwa namna yoyote. *Part* ya *YUNA*, wenye wanaendelea na ujenzi. *Sites* zao tatu zimeshavuka 90%, wanaenda bila matatizo. Theorem ambaye ndio alikuwa na *sites* tano, alileta *demand* ya kuongezewa dola milioni 12 kwa sababu mbalimbali alizozitaka. Serikali imemwomba alete *justification*, ameshindwa, ameleta barua, anataka kujitoa kwenye ujenzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba Serikali haitaenda kuingia *additional cost* kwenye mradi huu. Huu ni mkataba wa kukopa, hatupewi sadaka. Kwa hiyo, mkopo una *framework*, nasi tutausimamia kwa maslahi ya nchi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu *NFRA*. Serikali ina njia nyingi ya kutoa fedha kuikabidhi taasisi. Moja, wanaweza wakatoa fedha ambazo wamezibajeti na vile vile unaweza ukachukuliwa mkopo. Mkopo wa *NFRA* ultolewa *under guarantee* ya *TR*, ni mkopo wa Serikali. Ili usiwe mzigo kwa *NFRA* baada ya ile *maturity* ya *OD* kwisha, *interest* inabebwa na Serikali na wala siyo *NFRA*. Kwa hiyo, kutakuwa hakuna *burden* yoyote kwa *NFRA* kwa ile shilingi bilioni 50

Mheshimiwa Spika, nasi kama Serikali tumeamua badala ya ile *15 billion* ikifikia *ku-mature*, kuoandoa ile *capital* mkononi mwa *NFRA*, Wizara tutakuwa tunatenga kwenye bajeti yetu ile *cost of financing*, hii *50 million* itaendelea kubaki *NFRA* na kuifanya *NFRA* kuwa na *liquidity*, wakati huo tunaiwekea bajeti ya kila mwaka na kufanya uwezo wa *NFRA* kuwa mkubwa (*aggregative*). Kwa sababu kuna njia mbili za *NFRA* anafanya; pale ambapo tunakuwa na dharura kama nchi, *NFRA* ndiyo ina jukumu la kutoa chakula cha msaada.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo wakulima wanapata shida kuuza mazao, tunaitumia *NFRA* na *CPD* kama *stabilizing instrument* kuweza kwenda kuchukua mazao

kwa *subsidize rate*. Kwa hiyo, naomba niwatoe hofu kwamba maamuzi ya Serikali baada ya Bunge kushauri kununua mazao ya wakulima ya mahindi na *model/iliyochukuliwa* na Serikali ni njia sahihi ambayo haina hasara yoyote na ni njia salama ya *capitalize taasisi* nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kusema tunashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maoni yao, sisi tutapokea ushauri hasa kwenye eneo la mikataba. Mikataba yoyote tunayoingia hasa kwenye sekta ya kilimo niwahakikishie itakuwa ni mikataba kwa maslahi ya wakulima na wananchi na huu ndiyo mwelekeo na maagizo ya Mheshimiwa Rais, lazima kuwe na *value for money* kwenye any mkataba tunaingoingia nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, atafutatiwa na Mwenyekiti wa Hesabu za Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi. Niseme tu kwa niaba ya Serikali, maoni ya kamati hizi mbili ambazo ni muhimu sana, ambazo zinafanya kazi ya kufuatilia (*over site function*) zimefanya kazi zao vizuri sana na ninawapongeza sana. Nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya PAC, Mheshimiwa Kaboyoka, taarifa yake nzuri na Wajumbe wote wa Kamati hiyo. Kipekee sana nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Grace Tendega kwa ripoti nzuri sana. Nawapongeza pia Makatibu wa Kamati, wamefanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yamesemwa mambo mengi makubwa yenye nia ya kuishauri Serikali, kama ambavyo wajibu wa Bunge umesemwa kwa mujibu wa Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nasi kama Serikali, kazi yetu kwa muktadha huu ni kupokea taarifa hizi ambazo baadaye kupitia kitie chako zitapitishwa na kuwa maazimio

ya Bunge; kwa hiyo, Serikali kazi yake itakuwa ni kwenda kuyapitia na kuyatekeleza kwa kadri kanuni za Bunge zinavyotaka, ambapo huko tutakutana Serikali pamoja na Kamati na kujaribu kutekeleza na kuteta taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge kwa mujibu wa utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wangekuwepo Mawaziri wote na pengine wangepata fursa ya kusema hapa, wangeweza kupunguza mzigo ambaa umesemwa, lakini tunafahamu ziko taratibu. Nakushukuru na kukupongeza pia wewe kwamba umetuongoza vizuri na Serikali tumepata kusikia, lakini kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge, unazo Kamati makini. Kwa kweli ni watu makini na wamefanya kazi yao vizuri; nasi upande wa Serikali tutajitahidi kufanya nao kazi vizuri ili tuhakikishe kwamba tunamsaidia Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Rais wa Awamu ya Sita hayuko tayari kuona fedha za Serikali zinachezewa, hayuko tayari kuona Serikali inaingia mikataba mibovu. Amesema ukitaka kujua *true colors* zake, chezea fedha ya umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tutafanya kazi hii kwa uaminifu mkubwa upande wetu wa Serikali kwa kadri kila sekta ilivyoguswa ili kuhakikisha kwamba ripoti hizi za Kamati zinatendewa haki ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nirudie tena kuwapongeza Kamati zote mbili kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa George Simbachawene. Nimwite sasa mtoa hoja mojawapo ili haje aitimishe hoja yake. Nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*Public Accounts Committee*) Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, aje ahitimishe hoja ya Kamati yake.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja ya Kamati yangu. Natambua kwamba umenipa dakika tano tu; pamoja na kwamba ningependa ni-*respond* kwa kila mmoja aliyesema, kwa muda wa dakika tano sitaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitambue tu kwamba waliochangia upande wa hoja za *PAC* ni Mheshimiwa Bakar Ahmad, Mheshimiwa Aysharose Mattembe, Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Venant Daudi, Mheshimiwa Aida Khenani, Deus Sanga, Mheshimiwa Samuel Songe na Makamu wangu, Mheshimiwa Japhet Hasunga.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia yale yote ambayo Mheshimiwa Japhet Hasunga ameyasema, ni kama ame-*summarize* hoja yote, tunataka Serikali ikaifanyie kazi. Kwa kutambua kwamba Serikali imeweza kujibu hayo machechi ambayo waliweza kuyajibu; na kwa kuwa tunajua kwamba sisi *PAC* *hatu-rely* kwa majibu ya mdomo, ni mpaka tena *CAG* aende a-*verify* hayo miliyosema, napenda kusema kwamba nitambue michango yote ya Waheshimiwa Mawaziri ambayo Kamati tumeipokea. Ni imani yetu kwamba Serikali itatimiza wajibu wake ili sasa katika kaguzi zijazo Kamati ifanye ufuatiliaji wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hoja ya Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali maoni na mapendekezo yалиyotolewa na Kamati ili yawe maazimio ya Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mwenyekiti ahsante sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji; Wabunge wanaoafiki Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*Public accounts Committee*) kuhusu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021 ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Ahsanteni sana. NimWite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*Local Authorities Accounts Committee*), Mheshimiwa Grace Tendega aje akamilishe hoja yake. (*Makof*)

MHE. GRACE V. TENDEGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru sana wewe na wote waliochangia hoja hii na Mawaziri wote ambao wamechangia kwa namna moja au nyingine katika kujibu hoja hizi. Nawashukuru sana kwa sababu wameunga mkono hoja zote za Kamati ambazo tumezitoa na ndiyo maana tulizitoa katika maoni yetu na pia nimepokea pongezi zenu zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wengi wamejikita kujengea tu hoja zile namna ya kutoa maelekezo, basi nitambue michango ya waliochangia katika Kamati yetu ya LAAC. Kwanza Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Twaha Mpembewi, Mheshimiwa Ali Kasinge, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Tauhida Gallos Nyimbo, Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Francis Mttinga,

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Anastazia Wambura; na Mawaziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange na Mheshimiwa George Simbachawene, tunawashukuru kwa michango yenu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, yale yote ambayo wameyasema, basi tunaomba yakawe katika utekelezaji kwa sababu tunafanya kazi kwa mujibu wa taarifa ya CAG. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa yale ambayo wameji-*commit* lakini katika mifumo, lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Festo Dungage tuwaombe basi Ofisi ya Rais, TAMISEMI mharakishe kuleta mifumo kama huo mfumo wa tausi ili kuweza kudhibiti hizo fedha ambazo zinatumika fedha mbichi. Hii itasaidia Serikali iweze kupata mapato ya kasaidia wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pia hii ya kufuata miamala, mmesema mtaangalia ile *bureaucracy the way ilivyo kuhakikisha Maafisa Masuhuli wanakuwa responsible*, itasaidia sana kwa sababu yeye ndio *accounting officer* atatusaidia kuweza kuona kwamba fedha zile zinakuwa katika mikono salama.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa watumishi na watu wengine kama walivyosema Waheshimiwa wa Bunge katika kuchangia kwao, Serikali iweze kutoa mafunzo kama tulivyosema katika taarifa yetu, itasaldia sana watendaji kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu 10%, hilo tunaomba Serikali iweze kufanya kazi kwa umadhubuti kabisa kwa sababu fedha zile zikirudi kuna baadhi ya Halmashauri zitakuwa zimefikia ukomo wa kutenga tena; na zile fedha zitatosha kuwakopesha wananchi wetu wengi zaidi wakawenza kunufaika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kukushukuru na nishukuru watendaji wote wa meza yako.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. ABUBAKARI D. ASENGA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mwenyekiti.

Waheshimwia Wabunge, sasa nawahoji, wanaoafiki Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu ya Serikali za Mitaa (*Local Authority Account Committee*) kuhusu taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021 ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunbe, kwanza nichukue fursa hii kusema rasmi kwamba Hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu ya Serikali ambayo nimeshawahoji hapa na mmekubali maana yake ni kwamba mapendekezo yote yaliyowekwa kwenye taarifa hii ambayo sasa baada ya kuwahoji yanakuwa ni maazimio ya Bunge ili Serikali ikayafanyie kazi, yote yamepita hakuna upande wa Serikali ulioonesha kwamba kuna mahali pengine pakae namna hii; kwa hiyo, yote yamepita kama yalivyo. Nasi matarajio yetu kama Bunge ni kwamba mtayafanya kazi kama mlivyoahidi hapa ndani na pia kadri utaratibu wetu kisheria unavyowataka mfanye. Kwa sababu lengo la Taarifa hizi za Kamati ni kuonesha wapi kuna changamoto na Serikali mchukue hatua.

Kwa hiyo, tunatarajia taarifa ijayo ya Kamati ya Hesabu za Serikali, itaonyesha tofauti kwamba kuna mambo ambayo yamebadilika na mambo ambayo Serikali mmeshayafanya kazi kwa kadri Waheshimiwa Wabunge

walivyozungumza hapa ndani na pia kwa mujibu wa mapendekezo ambayo Wabunge wameshahojiwa.

Kwa namna hiyo hiyo, hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu ya Serikali ya Mitaa na mapendekezo yake yote yaliyoko mle, hakuna mapendekezo ambayo yamebadilishwa na upande wowote ama na Mbunge yejote. Kwa hiyo, yamepita kama yalivyo. Kwa hiyo, upande wa Serikali baada ya hayo mapendekezo kuhojiwa, maana yake ni maazimio ya Bunge, maana yake Bunge limeshaazimia yale ambayo Kamati imesema imekubaliananayo.

Kwa hiyo, tunatarajia kwamba upande wa Serikali mtayatilia maanani yale yote ambayo Wabunge wamependekeza hapa ili mkayafanyie kazi kwa sababu sasa Bunge limeshayapitisha hayo kama maazimio.

Kwa hiyo, tunawatikia kila heri katika kuyafanya kazi. Ni mambo mengi lakini yote ni ya muhimu sana ili kuhakikisha nchi yetu inapiga hatua. Upotevu wa mapato uliooneshwa, mwingine ni wa dhahiri kabisa, kama hiyo ya mishahara, inaendaje sehemu ambako wafanyakazi kwanza watu wanatafuta ajira, hawajapewa, halafu fedha zinaenda; kumlipa nani sasa? Fedha zinaenda nydingi, wakati tunasema pengine tunasubiri utaratibu fulani kwa ajili ya kujazia nafasi hizi na hizi ambazo watumishi hawapo, halafu kumbe fedha zipo, zinaenda na haziwakuti watu wa kuwalipa kule. (*Makofii*)

Kwa hiyo, mazingira kama hayo yanaonesha kwamba kuna kazi ya kufanya na ndiyo maana Serikali mpo hapa Bungeni kwa ajili ya kusikiliza mawazo ya Waheshimiwa Wabunge ili pale wanapowashauri, ni kwa ajili ya kuonesha kwamba sote tunataka nchi isonge mbele; na ushauri wa Wabunge kama mnavyofahamu kikatiba ni muhimu mkauzingatia na kama hamkuizingatia, basi kuwe na sababu. Tunaamini haya yaliyotajwa; udhaifu ambaao upo kabisa ndani ya uwezo wenu, myafanyie kazi kwa haraka ili safari ijayo tusikute hizo changamoto ambazo zimeainishwa na Kamati.

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Nilitaka kusititiza jambo moja kabla sijaahirisha, nalo ni la mahudhurio ya Mawaziri na Naibu Mawaziri, Bungeni. (*Makof*)

Mnadhimu wa Serikali, mimi nafahamu na ndiyo maana huwa siku zote nasema hapa, hata Mbunge akisema Waziri simwoni, Serikali ipo Bungeni; ni kweli Serikali ipo Bungeni, lakini sote tunafahamu, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mbunge na ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, huwa anahudhuria Bungeni na anakaa hapa Bungeni kusikiliza hoja za Wabunge. Kama hakuonekana hapa, basi ujuwe yupo kwenye kikao au amesafiri. (*Makof*)

Sasa kuna Mawaziri wapo Dodoma, lakini hawapo kwenye kikao na hayupo Bungeni. Pia tunao Naibu Mawaziri ambao wako Dodoma, lakini hawapo kwenye kikao na hawapo Bungeni. Sasa tunalikosea heshima Bunge. Wale ambao wako kwenye vikao, *Government Chief Whip* unakuwa na taarifa nao. Hao inaeleweka, Serikali haiwezi kufanya kazi kwa wote kukaa hapa, hapana. Wapo ambao watasafiri na Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Rais atawaita akakae nao kikao; wataitwa na Waziri Mkuu, wataitwa na Makamu wa Rais, lakini wale ambao wanakuwa huko kote hawapo, wawepo Bungeni. (*Makof*)

Pamoja na kwamba watapelekewa taarifa na utaratibu uko mzuri kabisa, ila lengo la Serikali kuwa sehemu ya Bunge ni pamoja na wao kuwepo Bungeni wakati hoja za Wabunge zikzungumzwa; na hoja za Wabunge ni hoja za wananchi wanaowawakilisha. Kwa hiyo, ni vizuri Waziri akisikiliza mwenyewe, atajua hata yule Mbunge hoja kule alipoitoa ni wapi na mambo kama hayo, kuliko anapopelekewa kwamba shughulika na jambo hilli.

Kwa hiyo, naomba sana hilo lisisitizwe. *Chief Whip* kwenye vikao vyenu Mawaziri, Naibu Mawaziri tunawatarajia Bungeni kama ambavyo nimesema, Mheshimiwa Waziri Mkuu anaonesha mfano mzuri na kama Waziri Mkuu anaweze kukaa Bungeni, basi hakuna Waziri wala Naibu Waziri ambaye

NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hayupo kwenye kikao anayetakiwa kuwa nje ya Bunge.
(Makofii)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niwakumbushe tu baada ya kutoka hapa tunaelekea kwenye tafrija ya kupokea makombe yetu na kuwapongeza wale waliofanya vizuri. Nawatakia jioni njema.

Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 8.00 mchana.

*(Saa 1.05 Usiku Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 18 Februari, 2022 Saa Nane Mchana)*